# MTAZAMO LINGANISHI WA ITIKADI KATIKA *UTENZI WA MWANAKUPONA* NA MASHAIRI YA MUYAKA

**(COMPARATIVE ANALYSIS OF IDEOLOGIES IN THE EPIC OF MWANAKUPONA AND POEMS OF MUYAKA)**

**DOREEN NKATHA MUTEMBEI**

**C50/20038/2021**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2025**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi wasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

Sahihi.................................... Tarehe 14/11/2025..............................

DOREEN NKATHA

C50/20038/2021

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi wa shahada ya juu aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi.................................... Tarehe 14/11/2025..............................

DKT. JESSEE MURITHI

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA



## TABARUKU

Utafiti huu nautabaruku kwa wavyele wangu wapendwa, Amos Mutembei Mutegi na Sabina Kanana Kaburu na hata mpenzi wangu Lewis Mwenda Kinyua. Mola awamiminie baraka tele. Nisingefaulu bila mchango wenu.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa maarifa na pia hekima ya kupata mada hii ya utafiti, kuifanyia pendekezo hadi kufanya utafiti huu. Namshukuru kwa dhati msimamizi wangu Dkt. Jessee Murithi kwa jinsi alivyonielekeza, kujitolea kuipitia tasnifu na kunikosoa, kunipa ushauri na kunitia moyo. Mwenyezi Mungu akupe maisha marefu yenye baraka tele na mafanikio.

Pia nawapa shukrani wahadhiri wote walionifunza na kunikuza kitaaluma: Prof. Ngugi Pamela, Dkt. Osore Miriam, Prof. Kitula Kinge'i, Prof. Wafula Richard, Dkt. Masinde Edwin, Prof. Leonard Chacha Dkt. Eunice Nyamasyo na Dkt. Stephen Kamau. Mungu awabariki sana. Pia shukrani ziwaendee wanafunzi wenzangu wa uzamili: Stephen Njuguna na Samuel Kioko, walionihimiza nikaze kamba kila wakati. Nawatolea shukrani za kipekee pia kwa kunipa fursa ya kujumuika nanyi wakati nilihitaji msaada wenu na pia kuelimishana darasani.

Vilevile, nawashuruku wavyele wangu; Amos Mutembei Mutegi, Sabina Kanana Kaburu, John Kinyua na hata Dorothy Kinyua kwa kuniombea na kunitia moyo katika utafiti wote. Mungu awape maisha mema yenye baraka tele na neema nyingi. Namshukuru pia mpenzi wangu Lewis Mwenda Kinyua kwa kunitia nguvu, kunitia moyo na pia kuwa katika kipaumbele ili kuhakikisha kuwa nimemaliza utafiti huu. Mungu akubariki na akuzidishie maisha yenye baraka.

## YALIYOMO

**IKIRARI** ..... **ii**
**TABARUKU** ..... **iii**
**SHUKRANI** ..... **iv**
**YALIYOMO** ..... **v**
**UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU** ..... **x**
**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... **xi**
**IKISIRI** ..... **xii**
**ABSTRACT** ..... **xiii**
**SURA YA KWANZA** ..... **1**
**UTANGULIZI** ..... **1**
1.0 Utangulizi ..... 1
1.1 Usuli Wa Mada ..... 1
1.2 Suala La Utafiti ..... 4
1.3 Malengo Ya Utafiti ..... 5
1.4 Maswali Ya Utafiti ..... 5
1.5 Sababu Za Kuchagua Mada ..... 6
1.6 Upeo Na Mipaka Ya Utafiti ..... 7
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..... 8
1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Itikadi ..... 8
1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Utenzi Wa Mwanakupona ..... 12
1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mashairi Ya Muyaka ..... 13
1.8 Misingi Ya Nadharia ..... 15
1.8.1 Nadharia Ya Itikadi ..... 15
1.9 Mbinu Za Utafiti ..... 20
1.9.1 Muundo Wa Utafiti ..... 20
1.9.2 Mahali Pa Kufanyia Utafiti ..... 21
1.9.3 Uteuzi Wa Sampuli ..... 21
1.9.4 Ukusanyaji Wa Data ..... 22
1.9.5 Uchanganuzi Wa Data ..... 22

1.9.6 Uwasilishaji Wa Data ........ 23
1.9.7 Maadili Ya Utafiti ........ 23
1.10 Hitimisho ........ 23
**SURA YA PILI ........ 25**
**ULINGANISHAJI WA ITIKADI KATIKA UTENZI WA MWANAKUPONA NA MASHAIRI YA MUYAKA ........ 25**
2.0 Utangulizi ........ 25
2.1 Itikadi Katika Mashairi Ya Muyaka ........ 25
2.1.1 Itikadi Ya Mapinduzi Ya Nguvu ........ 26
2.1.2 Itikadi Ya Ukandamizaji ........ 30
2.1.2.1 Mapenzi Na Ndoa ........ 30
2.1.3. Itikadi Ya Uhuru ........ 32
2.1.3.1 Mapenzi Na Ndoa ........ 33
2.1.3.2 Mfumo Wa Kiuchumi ........ 36
2.2 Itikadi Katika Utenzi Wa Mwanakupona ........ 39
2.2.1 Utangulizi ........ 39
2.2.2 Itikadi Ya Taasubi Ya Kiume ........ 39
2.2.2.1 Dini Inavyothihirisha Itikadi ........ 40
2.2.2.2 Usafi Unavyothihirisha itikadi ........ 43
2.2.2.3 Ndoa Inavyothihirisha Itikadi ........ 44
2.2.3 Itikadi Ya Utiifu. ........ 47
2.2.3.1 Dini Kama Njia Ya Udhibiti Wa Itikadi ........ 47
2.2.3.2 Utamaduni Unavyothihirisha itikadi ........ 56
2.2.3.3 Fasihi inavyothihirisha itikadi ........ 64
2.2.4 Itikadi Ya Ukawaida ........ 65
2.2.4.1 Utamaduni ........ 65
2.2.5 Ulinganishaji ........ 68

**SURA YA TATU ........................................................................................................ 70**
**ATHARI YA ITIKADI KATIKA USAWIRI WA MAUDHUI KATIKA UTENZI WA MWANAKUPONA NA MASHAIRI YA MUYAKA....................................... 70**
3.0 Utangulizi.................................................................................................. 70
3.1 Itikadi Zinavyoathiri Uwasilishaji wa Maudhui katika Mashairi Ya Muyaka ..... 70
3.1.1 Maudhui Yaliyopelekewa na Itikadi Ya Ukandamizaji ................................ 70
3.1.1.1 Maudhui ya Tamaa .................................................................................. 70
3.1.1.2 Maudhui ya Utabaka................................................................................. 72
3.1.1.3 Maudhui ya Magonjwa na Kifo............................................................. 75
3.1.2 Maudhui yaliyopelekewa na Itikadi Ya Mapinduzi Ya Nguvu ..................... 79
3.1.2.1 Maudhui ya Uzalendo na vita................................................................. 79
3.1.3 Maudhui Yaliyopelekewa na Itikadi Ya Uhuru Wa Mtunzi .......................... 83
3.1.3.1 Maudhui ya Utamaduni ........................................................................... 83
3.1.3.1.1 Chakula .................................................................................................. 83
3.1.3.1.2 Mavazi ................................................................................................... 85
3.1.3.1.3 Maudhui ya Usafiri ................................................................................ 86
3.1.3.2 Maudhui ya Dini........................................................................................ 87
3.1.3.3 Maudhui ya Ndoa na Mapenzi ................................................................ 91
3.2 Itikadi za Mwanakupona zilivyopelekea uwasilishaji wa Maudhui ..................... 96
3.2.1 Jinsi itikadi ya Itikadi Ya Utiifu ilivyopelekea maudhui ............................... 96
3.2.1.1 Maudhui ya Dini........................................................................................ 96
3.2.1.2 Maudhui ya Utamaduni ...................................................................... 100
3.2.1.3 Maudhui ya Uhusiano wa Wanajamii ................................................. 106
3.2.2 Itikadi ya Taasubi Ya Kiume pamoja na Itikadi ya Ukawaida Zilivyopelekea Uwasilishaji wa Maudhui ..............................................109
3.2.2.1 Ndoa na familia ...................................................................................... 109
3.2.2.2 Maudhui ya Utamaduni ...................................................................... 115
3.2.2.3 Maudhui ya Dini..................................................................................... 116
3.3 Ulinganishaji wa jinsi itikadi za watunzi zilivyopelekea uwasilishaji wa Mitindo vitofauti..........................................................................................119

**SURA YA NNE ........................................................................................................ 122**

**JINSI ITIKADI ZILIVYOATHIRI MTINDO KATIKA MASHAIRI YA MUYAKA NA UTENZI WA MWANAKUPONA ................................................. 122**

4.0 Utangulizi............................................................................................................ 122

4.1 Jinsi Itikadi Zilivyopelekea Uwasilishaji wa Mitindo Katika Mashairi Ya Muyaka..............................................................................................123

4.1.1 Itikadi ya Uhuru Wa Mtunzi ilivyopelekea Mitindo .................................... 123

4.1.1.1 Mtindo wa matumizi ya Kipokeo ......................................................... 124

4.1.1.2 Mtindo wa Ugonganishaji wa Wahusika Kihalisia .............................. 130

4.1.1.3 Mtindo wa Matumizi wa Lugha ya Picha na Taswira. .......................... 130

4.1.2 Jinsi Itikadi Ya Mapinduzi Ya Nguvu ilivyopelekea mitindo ..................... 134

4.1.2.1 Matumizi ya lugha iliyosheheni Maneno ya Kilahaja na Kuchanganya Lugha za Kigeni. ...................................................................134

4.1.2.2 Mtindo wa Udokezi wa Dhana Mahususi katika Mstari wa Mwisho wa Ubeti............................................................................. 141

4.1.2.3 Mtindo wa Matumizi ya Mashairi Mafupi. ........................................... 142

4.1.2.4 Matumizi ya Tamathali Mbalimbali za Usemi ..................................... 145

4.1.2.5 Mtindo wa Maneno katika Ukwapi kugeuzwa katika Utao. ................. 150

4.2 Mitindo katika Utenzi Wa Mwanakupona Ilivyojitokeza Kusababishwa na Itikadi za Mtunzi...........................................................................152

4.2.1 Jinsi Itikadi ya Utiifu Wa Mwanakupona ilivyopelekea Mitindo ................ 152

4.2.1.1 Mtindo wa Mawaidha au Didatiki ....................................................... 152

4.2.1.2 Uradidi .................................................................................................. 154

4.2.1.3 Matumizi ya Vina na Mizani ................................................................ 155

4.2.2 Itikadi Ya Taasubi Ya Kiume Na Itikadi ya Ukawaida ............................... 158

4.2.2.1 Lugha ya Kinaya.................................................................................... 158

4.2.2.2 Matumizi Ya Taswira ............................................................................ 162

4.3. Ulinganishaji wa jinsi itikadi za watunzi zilivyopelekea mitindo vitofauti....... 165

**SURA YA TANO** ........ **168**
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI** ........ **168**
5.0 Utangulizi ........ 168
5.1 Muhtasari Wa Tasnifu ........ 168
5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 171
5.3 Mapendekezo ya Utafiti ........ 172
5.4 Hitimisho ........ 173
**MAREJELEO** ........ **174**
**VIAMBATISHO** ........ **179**
Kiambatisho A: Kibali Cha Kukubalika Kwa Pendekezo ........ 179
Kiambatisho B: Kibali Cha Idhini Ya Kutekeleza Utafiti ........ 180
Kiambatisho C: Kibali cha NACOSTI ........ 181

## UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

| | |
|---|---|
| Itikadi : | Imani ambazo huelekeza matendo ya binadamu yeyote ulimwenguni. |
| Utenzi: | Tungo pana za ushairi zinazotoa maelezo kuhusu mambo fulani na huwa na vina vya kati tu. |
| Mtindo: | Upekee unaopatikana katika kazi za fasihi na huwa tofauti kati ya waandishi sababu ya hisia, mazingira, tajriba na hata itikadi za mwandishi. |
| Hejemonia: | Hali ya kikundi fulani kukubaliana kutawala kikundi kingine bila kutumia mabavu. |
| Ulinganifu: | Hali ya kuwiana kwa watu au vitu |
| Shairi: | Tungo lenye lugha ya kisanii, vina na mizani, urari na muwala maalumu katika uelezeaji wa jambo kwa kuzingatia kanuni za ubunifu wa mashairi yanayohusika |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKITA : | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| K.M: | Kwa Mfano |
| K.V: | Kama Vile |
| N. K : | Na Kadhalika |

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kulinganisha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Dhana ya itikadi ni dhana changamano na pana na imeibua mijadala mingi baina ya wataalamu mbalimbali. Itikadi ni muhimu kwa sababu huelekeza matendo yote ya mtunzi kuhusu yale atakayowasilisha na namna atakavyowasilisha kazi yake. Kwa hivyo, itikadi ndio huongoza misimamo, mielekeo na imani ya mtunzi. Vitabu teule vya kufanikisha utafiti huu ni mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Vitabu hivi viliteuliwa kwani ingawa kazi hizi ziliandikwa katika kipindi kimoja, ni tofauti kimtindo na kimaudhui. Hivi ni kusema kuwa watunzi hawa waliongozwa na itikadi tofauti. Kwa hivyo, ni muhimu kuchunguza na kuzilinganisha zile itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* na jinsi itikadi husika zinazowaongoza watunzi hao zinavyolingana na kujitokeza katika kazi zao. Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo: kubaini itikadi katika *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka, kutathmini jinsi athari za itikadi zinavyopelekea uwasilishaji wa maudhui kwenye *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka na kuchunguza athari za itikadi katika uwasilishaji wa mtindo katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Nadharia ya itikadi, mikabala ya Karl Marx (1977 na 1979), Louis Althusser (1981) na Antonio Gramsci (1985) ilitumika. Mkabala wa Karl Marx umetumika kwani unashikilia kuwa itikadi ni 'ungamuzi potoshi.' Mkabala wake Louis Althusser umetumika kwani aliorodhesha vyombo vya kiitikadi ambavyo alivigawa katika vikundi viwili. Vinavyo endeleza itikadi moja kwa moja kama vile polisi, jeshi, mahakama na serikali. Pia, vyombo visivyo vya moja kwa moja kama dini, elimu, vyombo vya habari na familia. Mwisho, mkabala wake Antonio Gramsci umetumika kwani Gramsci anaieleza dhana hii ya itikadi kama fikra, mitazamo na mielekeo ambayo binadamu huchukulia kuwa za kawaida hivyo kujikandamiza kwa hiari yake mwenyewe. Data husika ilitolewa maktabani ambapo shairi, beti, mishororo na vipande vya mishororo vilivyo na dhana za kiitikadi zilikusanywa. Mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ilitumika katika uteuzi wa sampuli. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo ili iweze kueleweka. Kutokana na data ya utafiti huu, imebainika kuwa Muyaka na Mwanakupona waliongozwa na itikadi tofauti ingawa walikuwa watunzi wa kipindi kimoja cha kirasimi. Itikadi hizo zilipelekea uwasilishaji wao wa maudhui na mtindo vitofauti.

**ABSTRACT**

This study aimed to compare ideologies in the poems of Muyaka and *Utenzi wa Mwanakupona*. The concept of ideology is complex and broad, and it has generated extensive debates among various scholars. Ideology is important because it guides all the poet's actions regarding what they choose to present and how they present their work. Therefore, ideology directs the poet's positions, orientations, and beliefs. The selected texts for this research are Muyaka's poems and *Utenzi wa Mwanakupona*. These works were chosen because, although they were written during the same historical period, they differ in both style and thematic content. This implies that the two poets were guided by different ideologies. Hence, it is important to examine and compare the ideologies expressed in Muyaka's poems and Utenzi wa Mwanakupona, and to determine how those ideologies influence and manifest in their respective works. This study was guided by the following objectives: to identify the ideologies in *Utenzi wa Mwanakupona* and Muyaka's poems; to evaluate how ideological influences affect the presentation of themes in these works; and to examine the impact of ideology on stylistic presentation in both *Utenzi wa Mwanakupona* and Muyaka's poetry. The study was anchored on the theory of ideology as presented in the perspectives of Karl Marx (1977, 1979), Louis Althusser (1981), and Antonio Gramsci (1985). Karl Marx's approach was used because he viewed ideology as a form of "false consciousness." Louis Althusser's approach was applied because he classified ideological apparatuses into two categories: those that directly enforce ideology—such as the police, military, judiciary, and government—and those that do so indirectly, such as religion, education, the media, and the family. Finally, Antonio Gramsci's perspective was adopted because he described ideology as the ideas, attitudes, and orientations that individuals accept as normal, thereby subjecting themselves to self-imposed domination.The relevant data were collected from library sources, where poems, verses, lines, and excerpts containing ideological concepts were gathered. A purposive sampling method was employed in selecting the samples. The data were analyzed and presented descriptively to ensure clarity and comprehension. Findings from the study revealed that Muyaka and Mwanakupona were guided by different ideologies, despite being poets from the same classical period. These ideologies influenced the ways in which they presented both thematic content and stylistic features in their works.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, nafasi ya nadharia katika utafiti, mbinu za utafiti na hitimisho.

### 1.1 Usuli Wa Mada

Kwa mujibu wa Mulokozi (1986), ushairi ni mpangilio mahususi wa maneno fasaha yenye muwala, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuelekeza jambo fulani. Vilevile, hutumia lugha ya mkato katika usemi na hutumika kueleza au kufunza suala au hisia zinazohusiana maisha ya binadamu. Njogu na Chimerah (1999) kwa upande mwingine, wanasema kuwa ushairi ni sanaa ya lugha inayofafanua jambo kwa njia ya mvuto na vilevile kwa namna inayoteka hisia za msikilizaji au msomaji. Isitoshe, Wamitila (2010), anasema kuwa ushairi ni utungo wa sanaa ya lugha ambao huwa na mpangilio maalum wa mishororo au wa kisauti na huwa na maneno mateule.

Kwa mujibu wa wanazuoni wa kale na wa mwanzo wa taaluma ya Kiswahili kama Hichens (1939), Allen na Thomas (1939) na Abdilatif Abdalla (1973), utenzi ni aina ya shairi refu la Kiswahili lenye mpangilio maalum wa vina, mizani, na mtiririko wa kimaudhui unaosimulia tukio. Hadithi au fundisho. Kwa urasimi wa kale, utenzi ulizingatiwa kuwa diwani ya kishairi yenye dhamira nzito za kidini, kifalsafa, au kihistoria. K.m Utenzi wa Tambuko (karne ya 18) uliotungwa na Mw. Hemedi Abdalla unaeleza vita vya Waarabu Waislau dhidi ya Warumi, ukiakisi ulimwengu wa imani ya Kiislamu na maadili ya ujasiri,

uaminifu na imani.

Finnegan (1970) naye, anatoa maelezo kuwa utenzi ni shairi refu lenye beti nyingi ambazo huwa na mizani michache au mishororo mifupi.  Mara nyingi hukosa vina vya kati. Kulingana na Finnegan, utenzi mara nyingi hubeba maudhui kama ushujaa, dini na matukio yoyote ya kihistoria. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) katika historia ya fasihi ya Kiswahili, utenzi ni shairi refu linalosimulia matukio ya kishujaa, kihistoria, au kidini, lililoandikwa kwa bahari ya utenzi, na lenye ubeti wa mishororo minne yenye mizani ya tarakimu nane kwa kila mshororo.

Kwa mujibu wa Mazrui na Syambo (1992) utangulizi wa utenzi mara nyingi huanza kwa kuomba mungu, kutafuta vifaa kama vile, karatasi, kalamu na wino. Sehemu ya mwili hubeba maudhui ya utungo wenyewe na mwishowe katika kimalizio, mtunzi hudhihirisha jina lake. Mazrui na Syambo wanaendelea kusema kuwa tenzi hazifai kuzidi mizani kumi na miwili kila mshororo. Huwa na mishororo minne kila ubeti. Isitoshe, Maudhui huwa ya kihistoria, kidini au kueleza tukio la kishujaa. Vilevile Masinde (2003) anasema kuwa katika tenzi nyingi, watunzi hujitambulisha na pia hutaja jina la ukoo wao au mahali walipozaliwa. Hii huwa sifa ya nguvu mali. Mwishowe, tenzi humalizika kwa kushukuru mungu na kuomba msamaha kama mtunzi alifanya makosi katika utenzi au utunzi huo.

Kwa mujibu wa Hegel (1977), itikadi ni mawazo ambayo hujumuisha malengo, matamanio na matarajio na matendo ya mtu. Ni mtazamo ambao humuongoza binadamu kutenda anayotenda katika jamii. Mawazo haya husababishwa na haja ya mabadiliko yanayotokea kutokana na mpito wa wakati mpaka kufikia mpaka na kutaka uhuru wa mawazo. Kadri wakati unavyobadilika nayo mawazo hubadilika, maoni na mielekeo ya mwanadamu hugeuka ili kufikia kiwango cha mawazo kutokana na jinsi alivyopevuka

kiroho na kupata uhuru wa kimawazo. Hivyo, binadamu hutumia fikra au mawazo yake ili kujaribu kuelewa jamii au ulimwengu wake.

Dhana ya itikadi pia imefasiriwa kama matamanio, fikra, malengo na maelezo ya mtunzi kuhusu masuala ya kisiasa, kidini, kijamii na kiuchumi kwa ujumla wake (Chuachua, 2011). Kulingana na Gramsci (1985), itikadi hupata nguvu za kuweza kutawala kutokana na binadamu kuzoea na kukubali bali si kwa kutumia nguvu wala kulazimisha. Katika ufafanuzi wake, suala au jambo la kawaida linamaana kuwa binadamu huzoeshwa kukuza na kupokea maoni, mawazo na mitazamo katika jamii kupitia waliyoyazoea akilini mwao kama vitu vya kawaida. Binadamu hujipata amezoea jambo au mambo kuwa jinsi yalivyo ilhali kiasilia, mielekeo, mawazo na mitazamo hii iligunduliwa na kukuzwa na tabaka tawala la mabwanyenye ili kuendeleza maslahi yao wenyewe. Kwa mfano, watu kuchukulia ni kawaida wanaume kupewa kipaumbele ikilinganishwa na wanawake katika jamii.

Wafula (2015) anaongeza kuwa mara nyingi itikadi hujitokeza palipo na mivutano ya kijamii na huweza kubadilika na kukuzwa upya ili kulandana na matakwa, matarajio na malengo ya wanajamii ya wakati husika. Wafula anaendelea kusema kuwa itikadi kwa kiasi kikubwa inaweza kuipondoa nadharia ili nadharia husika ichukue msimamo maalum. Kupitia kazi yake Wafula ni dhahiri kuwa dhana hii ya itikadi inaendelea kuchangia namna ya utunzi, usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi.

Haya pia yanapatikana katika kazi yake Mohammed (1995). Mohammed anasema kuwa itikadi ndiyo humwongoza mwandishi kuhusu atakayoshughulikia katika kazi yake. Itikadi hiyo hutokana na mazingira, mahali alipozaliwa na kukulia, hali ya kichumi na mitazamoya mtunzi katika kipindi chake. Kutokana na hayo, ni muhimu kufahamu

historia ya mwandishi wa kazi ya fasihi na muktadha wake wa kihistoria kwani mazingira anamozaliwa na kukulia huenda pamoja na itikadi atakayoridhia ili kukidhi mahitaji ya jamii yake.

Kazi hii ilinuia kuzilinganisha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Itikadi huwa imani, fikra, mawazo na mielekeo ya mtunzi ambayo humfanya kuwasilisha ulimwengu wake kupitia dhamira, mtindo, maudhui na wahusika. Hivyo, itikadi huathiri watunzi wanavyosawiri mitazamo yao kuhusu maendeleo ya kijamii, teknolojia na kiuchumi. Kwa hivyo, utafiti huu ulieleza itikadi katika *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka.

**1.2 Suala La Utafiti**

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza itikadi katika mashairi ya Muyaka na Utenzi wa Mwanakupona. Itikadi kama imani ambazo huelekeza matendo ya binadamu yeyote ulimwenguni zimewaathiri Muyaka na Mwanakupona kwa namna wanavyosawiri mitazamo yao kuhusu yanayowasilishwa. Tafiti mbalimbali kuhusu itikadi zimeweza kushughulikiwa hapo awali na wataalamu kama vile Evans (2015) ambaye alitafiti kuhusu mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab. Wafula (2015) alitafiti kuhusu itikadi kama kiunzi cha ufunzaji wa nadharia zinazotumika kuchambua kazi za fasihi. Pia, Murithi (2017) ametafiti kuhusu itikadi katika riwaya za Said, A. Mohamed, miongoni mwa watafiti wengine. Ila kipengele cha itikadi katika mashairi, hasa mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* hakijafanyiwa utafiti bado katika taaluma ya fasihi sababu Evans alikita utafiti wake kwa nyimbo, Wafula alishughulikia itikadi katika ufunzaji wa nadharia za fasihi na Murithi alitafiti itikadi katika riwaya. Upekee mwingine ni kuwa utafiti wetu umetumia mikabala ya Karl Marx, Louis Althusser na Antonio Gramsci

kama kiunzi cha uchambuzi wa kazi teule.

*Utenzi wa mwanakupona* na mashairi ya Muyaka, kazi zote mbili ziliandikwa katika kipindi kimoja cha urasimi (Mwanakupona 1790 - 1860 na Muyaka 1776 - 1840). Lakini tofauti zinajitokeza katika usawiri wa watunzi hawa wa maudhui na mtindo. Hivyo, ilibainika kuwa Muyaka aliongozwa na itikadi ya uhuru, ukandamizaji na hata mapinduzi ya nguvu. Ndiposa anashughulikia maudhui kama tamaa, vita, jinsi mapenzi yalivyomwendea kinyume na haya vita vya kiserikali. Mwanakupona naye aliongozwa na itikadi ya utiifu, taasubi ya kiume na hata ukubalifu na ukawaida. Itikadi hizi zilipelekea maudhui ya utiifu wa dini, utiifu wa tamaduni na hata utiifu katika ndoa bila kujua anaendeleza ukandamizaji hasa wa jinsia moja katika jamii.

Utafiti huu una nafasi ya kuchangia katika nadharia ya itikadi kwa uelewa zaidi kuhusu itikadi. Pia, utafiti huu uliongeza maarifa kuhusu itikadi katika taaluma ya fasihi na Kiswahili, haswa katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona.*

### 1.3 Malengo Ya Utafiti

Malengo ya utafiti yatakuwa:

1. Kubaini itikadi katika *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka.
2. Kutathmini jinsi athari za itikadi zinavyoathiri uwasilishaji wa maudhui kwenye *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka.
3. Kuchunguza jinsi athari za itikadi zinavyopelekea uwasilishaji wa mtindo katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*.

### 1.4 Maswali Ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo:

1. Ni itikadi zipi zinazojitokeza katika *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya

Muyaka?

2. Ni kwa jinsi gani athari za itikadi zinavyoathiri uwasilishaji wa maudhui kwenye utenzi wa Muyaka *na Utenzi wa Mwanakupona*?
3. Ni kwa jinsi gani athari za itikadi zinavyopelekea uwasilishaji wa mtindo kwenye mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*?

**1.5 Sababu Za Kuchagua Mada**

Kwa mujibu wa Creswell (2014), mada huchaguliwa baada ya kutafakari iwapo inaweza kutafitika. Mtafiti alichagua mada hii sababu utafiti huu utachangia na kukuza taaluma ya fasihi haswa mashairi. Utafiti huu ulichanganua na kulinganisha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* na pia kuona athari za zile itikadi katika uwasilishaji wa maudhui na itikadi. Hivyo vipengele hivi vilituwezesha kuona ule utofauti wa kiitikadi, kimaudhui na hata kimtindo katika kazi hizi teule ingawa zilikuwa kazi za kipindi kimoja.

Kulingana na Rossiland (1990), itikadi ndio humuongoza binadamu yeyote katika masuala yanayohusu dini, siasa na nyanja zote za maisha. Vilevile, maoni ya Mohamed (1995), yanaoana na ya Njogu (1997) kwa kuwa itikadi ya mtunzi humuongoza mtunzi katika uchaguzi wa mambo muhimu katika jamii husika ili ayashughulikie katika utunzi wake na kuepuka mambo ambayo ni potofu. Itikadi hizo hutokana na mazingira, mahali alipozaliwa na kulelewa, hali ya kichumi na mitazamo katika jamii yake. Hivyo inamaana kusema kuwa watunzi hawa waliadhirika vitofauti na masuala katika mazingira yao. Kwa kufanya hivi, nadharia ya itikiadi na pia mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* yataeleweka na pia kupelekea tafiti tofauti na zaidi za siku zijazo.

Dhana ya itikadi imeweza kufanyiwa tafiti mbalimbali na wanafalsafa kama Gramsci

(1985), Karl marx (1977 na 1979), Eagleton (1976), Stoika (1971) na Althusser (1981), mingoni mwa wengine. Pia, Chuachua (2011), Evans (2015), Murithi (2017) na Wafula (2015) wameshughulikia itikadi katika kazi za Shaaban Robert, nyimbo za taarab, kazi za Said A. Mohammed na itikadi kama kiunzi cha ufunzaji wa nadharia zinazotumika katika uchambuzi wa fasihi ipasavyo. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa kipengele cha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*: mtazamo linganishi hakijashughulikiwa na mhakiki yeyote wa fasihi.

Kwa hivyo, utafiti huu utakuwa faafu kwani utawaongezea wasomi uelewa zaidi kuhusu itikadi haswa ile mikabala mitatu ya Karl Marx, Antonio Gramsci na Loius Althusser, ambayo imetumika kuzichambua kazi teule. Vilevile kazi hii itawafaa wasomi na wataalamu wa lugha ya Kiswahili sababu utasaidia katika uelewa zaidi wa mashairi ya Muyaka na pia *Utenzi wa Mwanakupona*. Pia data na matokeo ya utafiti yatapelekea kuongeza maarifa katika taaluma ya fasihi.

## 1.6 Upeo Na Mipaka Ya Utafiti

Kazi hii ililenga kushughulikia itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka zinawakilisha kipindi cha urasimi mkongwe wa fasihi ya Kiswahili. Mashairi ya Muyaka yaliibuka katika kipindi cha utawala wa Omani (1730 – 1890), katika upawa wa Afrika mashariki ulioambatana na migogoro ya kisiasa. Hiyo migogoro ilisababisha kuwe na wanaopinga utawala wa Omani. Pia, ustawi wa tabaka la juu la watawala wenyeji wa Waarabu lililoiga na kusisitiza utamaduni wa kiarabu na mafunzo ya dini ya kiislamu katika maswala mengi ya kimaisha. Tabaka hilo lilikuwa na wasomi wengi ambao waliandika kazi nyingi za tenzi za kidini zilizorejelea matukio muhimu ya kihistoria ambayo husishwa na dini ya

uislamu huko Arabuni, tungo za falsafa, mawaidha na utamaduni.

*Utenzi wa Mwanakupona* uliteuliwa sababu ni utenzi unaotambulika kwani ulioandikwa na mwanamke mzaliwa wa Pate katika kipindi kimoja na Muyaka. Mwanakupona aliangazia mambo yanayohusu utiifu kulingana na utamaduni, sharia za Kiislamu na sheria za arudhi katika utunzi wake.

Muyaka Bin Haji (1776 – 1840) ni miongoni mwa waasisi wa utungo wa ushairi wa Kiswahili, hasa utanzu wa bahari za 'shairi' (King'ei, 2007). Mtafiti aliteuliwa mashairi ya Muyaka kwani Muyaka anabadili maudhui yake kutoka ushairi unaoshughulikia dini na kuegemea katika mambo mengi katika mazingira yake ambayo waandishi wengine hawakuwa wanashughulikia. Katika kazi zake, uhuru wa mtunzi wa kiakili unapatikana. Lakini tunapata kuwa watunzi wa kazi hizi wanaangazia maswala kwa namna tofauti kufuatia msukumo wa itikadi ambazo ziliwafanya kushughulikia maswala kwa njia tofauti.

Kulingana na Mugenda na Mugenda (1999), sampuli ya kimaksudi huandamana na kundi ambalo mtafiti atalitumia katika utafiti wake. Tenzi hizi ziliteuliwa kimaksudi ili kuwakilisha mashairi ya kipindi cha urasimi mkongwe wa fasihi ya Kiswahili.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

### 1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Itikadi

Dhana ya itikadi ilishughulikiwa kwanza kwa jumla na Karl Marx. Mwanafalsafa huyu alikuwa wa kwanza kushughulikia dhana ya itikadi kwa mtazamo wa kuwa ni 'ungamuzi potoshi.' Anaifafanua dhana hii kama mawazo yote ambayo kimsingi ni mfumo wa uzalishaji mali na teknolojia. Fikra hizi huwa jumuisho la mitazamo na mielekeo ya watu katika siasa, sheria, maadili, dini la falsafa (Marx na Engels, 1977). Mitazamo hii

hubadilika kadri mfumo husika unavyobadilika kutokana na mpito wa wakati. Hivyo, itikadi na jamii huendelea kubadilika pamoja. Dhana hii ya itikadi ndio ambayo hueleza na kuhalalisha mifumo ya kijamii, kidini, kisiasa na kiuchumi. Kulingana na Marx, itikadi ni imani ya uongo. Mawazo ya Marx yalitufaa katika utafiti huu hasa katika kuelewa mrengo wa kwanza wa dhana ya Itikadi kwani alikuwa wa kwanza kushughulikia dhana hii.

Mhakiki wa Kifaransa, Louis Althusser (1918- 1990) pia anaendeleza dhana ya itikadi kwa kutumia mtazamo tofauti. Althusser anatilia mkazo vyombo vya kiitikadi vya kiutawala na kiudhibiti. Anaukataa mkabala wa marx na kisha anaibuka na mrengo mwingine mpya ili kutoa ufafanuzi bora wa nadharia ya itikadi. Anasema kuwa ili kuendeleza itikadi, vyombo viwili vya kiudhibiti na kiutawala hutumiwa. Kwanza, kuna vyombo ambavyo hupelekea kuwepo kwa itikadi kwa njia isiyo ya nguvu. Hivi ni; shule, dini, familia, siasa na pia utamaduni. Pili, vile ambavyo huendekeza utawala na udhibiti kwa matumizi ya nguvu nipolisi, serikali, jeshi, magereza na mahakama. Hivyo, imani za wanajamii hupitishwa kwa matumizi ya nguvu au kwa hujitakia yao wenyewe bila kujua (Althusser, 1981). Kwa hivyo, kila binadamu mwishowe hutawaliwa na itikadi ambazo humwezesha kufanya yote anayoyafanya katika wakati fulani. Kwa mfano, mtu kuenda shuleni kujifunza mambo mbalimbali na kuwa mtu mwenye manufaa katika jamii. Humo shuleni, mtu hushauriwa kutii walio kwenye mamlaka, kuwa na tija na kuepuka uhalifu. Kutokana na mifumo mbalimbali ya kiitikadi katika jamii, haswa itikadi ya utawala, elimu hapa inatumika kuwafanya matajiri kubaki kuwa matajiri zaidi bila kupinga. Kwa hiyo, itikadi tawala inazalisha watu ambao hawataipinga. Mtazamo huu wake hata hivyo ulitufaa kuelewa mrengo wa pili katika kuielewa dhana yaitikadi.

Mkabala mwingine unaotumika katika kufafanua dhana ya itikadi ni mrengo wa Antonio Gramsci (1985). Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu, itikadi hupokea nguvu za kimsingi kutokana na ukubalifu na ukawaida wala si kwa kutumia nguvu. Hapa, ukawaida unamaana kuwa wanajamii hurithishwa na kufanywa kupokea mawazo, mitazamo, mielekeo na matamanio fulani kutokana na waliyozoea kuzama akilini mwao. Binadamu hapa huchukulia na kuzoea kuwa suala ni jambo la kawaida ilhali kimsingi mawazo, mitazamo, mielekeo na matamanio hayayalitokana na tabaka tawala ili kujinufaisha wao wenyewe. Kwa mfano ambapo watu huchukulia ni jambo la kimsingi kwa wanaume kuwa na mamlaka dhidi ya wanawake. Mitazamo hii hujitokeza kama vigeu vya kiitikadi kama vile dini, utamaduni, vyombo vya habari, familia, miongoni mwa mambo mengine. Hivyo, mtu hutawaliwa na imani hizo kwa hiari yake mwenyewe na kupelekea kushughulikia maswala yanayohusu dini, siasa, uchumi, miongoni mwa mengine, kwa namna fulani. Mrengo huu ulitusaidia kuelewa dhana ya itikadi.

Mirengo yote mitatu ilitumika kuelewa itikadi kwa undani ili mirengo yote iwe kama dira katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu dhana ya itikadi kama 'ungamuzi potoshi', vyombo vya kiitikadi na ukubalifu na ukawaida, zinapatikana katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*.

Dhana ya itikadi imeshughulikiwa na watafiti mbalimbali. Chuachua (2011) amefanya utafiti kuhusu itikadi katika riwaya za Shaaban robert. Utafiti wake unaonyesha kuwa mtunzi ameongozwa na itikadi ya ujamaa uliokuwa umeenea sana. Haya yanajitokeza kupitia maswala kama mapinduzi ya kilimo na kishoshalisti, utangamano na mikinzano ya kitabaka. Anaeleza kuwa mtunzi aliathiriwa na uandishi wa wakati wa ukoloni, mivutano kati ya Ulaya mashariki na Magharibi na utetezi wa jinsia ya kike na haki za

wananchi dhidi ya walowezi. Isitoshe, anaeleza kuhusu kuwepo kwa matabaka na njia ya maadili, ugumu wa kufanya mapinduzi na ulazima wa kutafuta ukweli, miongoni mwa maswala mengine. Utafiti huu ulitufaa katika kuielewa dhana ya itikadi na athari yake kwa mtunzi huyu. Unahitilafiana na utafiti wetu kwani hajajikita katika utanzu wa ushairi na pia hajalinganisha watunzi ambao ni wa kipindi kimoja na kuona jinsi Muyaka na Mwanakupona walivyoathirika.

Evans (2015) katika utafiti wake amechunguza nyimbo za Taarab. Imedhihirika kuwa nyimbo teule za taarab na maudhui yanayotawala nyimbo husika yamesheheni ubabedume. Haya yanatokana na ukweli kuwa wasanii wengi wa nyimbo hizi huwa ni wa jinsia ya kiume. Hivyo, jinsia hii ya kiume hutaka kuendeleza mahusiano yao na jinsia ya kike, kwa nia ya kuipembeza jinsia ya kike. K.m, watunzi wa kiume wanapogundua kwamba baadhi ya wanawake wanakinza swala kama vile ukewenza, huweza kutunga nyimbo hizo kwa lengo la kuwakumbusha suala hilo lipo na limekubaliwa katika dini ya Kiislamu ambayo ndiyo dini tawala katika utamaduni wa jamii. Utafiti wetu unatofautiana na wake kwani ameshughulikia tu itikadi ya ubabedume hasa katika nyimbo za taarab. Lakini hajatafiti mashiari ya Muyaka waka *Utenzi wa Mwanakupona* na kuibuka na itikadi zozote. Utafiti wake utatufaa kuelewa kipengele cha ubabedume.

Mwishowe, Murithi (2017) katika tasnifu yake amechunguza itikadi katika kazi za Said. A. Mohamed. Alibaini mtunzi alibadilisha itikadi katika kazi zake ili kazi zake ziweze kuifaa jamii husika na katika kujisahihisha na kujirekebisha ameiratibu mielekeo na mawazo yake ya awali katika kazi zake. Kadri historia ilivyobadilika katika vipindi tofauti vya utunzi wa mwandishi, ndivyo itikadi zake zilivyobadilika. Vilevile, msimamo wake pia ukazidi kubadilika kwa sababu msimamo husababishwa na itikadi. Utafiti wetu

unahitilafiana na wake kwani tulitafiti jinsi itikadi zilivyowaongoza Muyaka na Mwanakupona katika kazi zao. Utafiti wake unajikita katika mabadiliko ya kiitikadi yanayojitokeza katika riwaya za S.A Mohammed ila wetu unashughulikia itikadi ambazo ziliwawaongoza Muyaka na Mwanakupona, kuwasilisha kazi zao kwa namna tofauti. Isitoshe, katika utafiti wetu tunalenga kuonyesha jinsi ambavyo ule utofauti unavyojitokeza katika kazi husika ilhali walikuwa watunzi wa kipindi kimoja cha urasimi.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Utenzi Wa Mwanakupona

Swaleh (1993) katika utafiti wake ameshughulikia maudhui katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Amebaini kuwa maudhui ya dini huwa na mafunzo ya Kiislamu ambayo huipa jinsia ya kike hadhi katika jamii. Haya yanamaana kuwa, hadhi hiyo inatumika katika jamii ili kuikandamiza jinsia hii. Vilevile, anabaini kwamba majukumu yanayopewa jinsia husika, hupelekea unyanyasaji na udunishaji katika jamii. Maoni yake yalitusaidia kuelewa maudhui yanayojitokeza katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Utafiti wetu unatofautiana na wake kwani tunatumia itikadi kama mwongozo wa kuyashugulika maudhui yanayopatikana katika utenzi huu.

Momanyi (2012) katika makala yake ameshughulikia jinsi jinsia ya kike ya Waswahili katika dini ya Islamu inavyosawiriwa katika kazi za: Muyaka Bin Haji, Shaaban Robert na Mwanakupona Binti Mshamu. Uchanganuzi wake umeweza kubainisha jinsi mwanamke anavyojitokeza kutokana na majukumu anayopewa. Jambo hili linatusaidia kuelewa na kuona taswira ya jinsia ya kike haswa katika kipindi cha Mwanakupona. Hapa, mwanamke anaonekana kama kiumbe duni na mwenye majukumu mengi sana katika ile jamii. Utafiti wetu unatofautiana na wake kwani anashughulikia usawiri wa mwanamke Muislamu katika kazi husika. Ila, katika utafiti wetu, tunabaini itikadi

zilizowaongoza Muyaka na Mwanakupona na jinsi itikadi husika ziliwaathiri katika uwasilishaji wa kazi zao.

Munyole (2017) ameshughulikia jinsi *Utenzi wa Mwanakupona* unavyofasiriwa sasa. Hapa, inadhihirika kuwa usomaji na ufasiri wa utenzi husika unabadilika kutoka na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Utungo huu ulitokana na mazingira ya wakati ule na ulionekana kama mawaidha ya mtoto wa kike ili kutunza ndoa yake kwa kufuatilia dini ya Kiislamu na Maadili. Lakini kutokana na mpito wa wakati, fasiri mbalimbali zinaiubuka na konekana kama utungo huu ulitumiwa kumkandamiza mwanamke. Maoni yake yalitusaidia kuuelewa *Utenzi wa Mwanakupona* kwa undani kupitia fasiri mbalimbali zinazotokana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na hata kijamii.

Pembe (2019) naye alitafiti kuhusu ufeministi katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Utafiti wake umebaini kuwa Mwanakupona aliendeleza ubabedume kwa kutaja majukumu mengine ambayo yanasawiri jinsia ya kike kama kifaa dhaifu kisicho na ruhusa wala uhuru wa kufanya jambo lolote bila jinsia ya kiume. Mfano pale ambapo Mwanakupona anaonyesha kuwa jukumu la kusimamisha ndoa ni la mwanamke na kuwa mwanamume hutoa hukumu ya mwanamke ya kuingia peponi au la. Vilevile, inabainika katika kazi yake kuwa *Utenzi wa Mwanakupona* uliathirika kwa kiwango cha juu na mfumo uliokuwepo, yaani ule wa Kimwinyi ambao kwao, mwanamume aliinuliwa zaidi kuliko mwanamke. Uwiano wa utafiti wake na wetu ni maudhui ya ufeministi ambayo tunanuia kubaini maudhui hayo na mengine, yalisababishwa na itikadi zipi.

### 1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Mashairi Ya Muyaka

Kuhusu Mashairi ya Muyaka, King'ei (2007) ameshughulikia jinsi washairi wa kipindi cha urasimi walivyowaathiri washairi wa kipindi cha usasa katika makala yake. Alitoa

mfano wa mashairi ya Muyaka kwa kulinganisha na kazi za Ahmad Nassir. Makala yake yamebaini kuwa washairi wakongwe mfano wa Muyaka, waliathiri washairi wa kisasa katika vichwa au mada zilizopewa mashairi, maudhui, mtindo na umbo na pia msamiati. Inabainika kuwa Muyaka ameweza kuathiri washairi kwa anwani anazopea mashairi yake kama vile oa, panda, jinga, kimya, miongoni mwa anwani zingine. Pia, aliathiri matumizi ya msamiati uliosheheni lahaja ya kimvita, kingozi na hata maneno yenye asili ya kiarabu. Muyaka aliathiri jinsi Nassir alivyoshughulikia maudhui ya hali ya vita kati ya miji ya Mombasa, Pate, Lamu na Unguja. Kwa mfano; maisha ya kibinafsi, falsafa kuhusu mawaidha ya aina mbalimbali, mapenzi na uhusiano kati ya mume na wake, miongoni mwa maswala mengine. Kinyume na kazi yake King'ei, tunadhamiria kuonyesha kuwa itikadi zilizomwongoza Muyaka katika mashairi yake. Isitoshe, tunadhamiria kuonyesha jinsi itikadi husika zilivyomfanya mtunzi kusawiri maudhui na mtindo wake kwa namna tofauti. Itikadi hizi tutazilinganisha na itikadi zilizomwongoza Mwanakupona ambaye aliongozwa na itikadi tofauti ila walikuwa watunzi wa kipindi kimoja cha urasimi.

Murithi (2021) ameshughulikia mtazamo linganishi wa muundo na maudhui ya Tenzi Mbili za Kale na ushairi wa Muyaka katika makala yake. Hizi ni utendi wa Al-Inkishafi na utenzi wa Liyongo. Alitaka kujua ikiwa kuna sifa za kimuundo na kimaudhui zinazofanana katika tenzi hizi na pia kutofautiana. Hii ni kutokana na kuwa watunzi wa tenzi hizi walitunga katika kipindi kimoja na Muyaka Bin Haji. Utafiti wetu utaangazia mashairi ya Muyaka na utenzi mwingine tofauti. Isitoshe, aliangazia muundo na maudhui katika mashairi ya muyaka ila katika kazi yetu tunashughulikia mtindo na maudhui kwa mtazamo wa kiitikadi kwani itikadi huelekeza matendo ya binadamu.

## 1.8 Misingi Ya Nadharia

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), nadharia ni maelezo ya suala ambalo huambatana na vigezo vilivyowekwa au vilivyotokana na jaribio la jambo hilo. Ngoju na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa nadharia husaidia kubaini uhusiano kati ya matukio na wahusika, matumizi ya lugha na maana inayoyojitokeza katika kazi husika. Hivyo, nadharia huwa mwongozo unaomwelekeza msomaji wa kazi kuifahamu kazi husika katika vipengele vyake vyote. Nadharia, huwa kama dira inayomwongoza mtafiti katika utafiti wake. Katika sehemu hii, mtafiti alieleza nadharia ya itikadi, mirengo yake mitatu na mihimili. Pia, alionyesha jinsi mihimili hiyo ilivyomsaidia kuhakiki kazi yake.

### 1.8.1 Nadharia Ya Itikadi

Kulingana na Murithi (2018), mwasisi wa nadharia hii ni Cabanis Destute de Tracy mnamo mwaka 1796. Mtaalam huyu aliieleza kama mfumo wa mawazo. Baadaye, kuliibuka waitifaki kama vile Karl Marx (1977 na 1979), Eagleton (1976), Louis Althusser (1981) na Antonio Gramsci (1985), miongoni mwa wengine. Katika utafiti huu, tumejikita katika mirengo mitatu.

**Kwanza, mrengo wa Karl marx (1977 na 1979).** Kulingana na Karl Marx, itikadi ni ung'amuzi potoshi ambao hutumika kuhalalisha mfumo wa siasa na kiuchumi katika jamii. Kulingana na Karl Marx (1977), itikadi ni imani na mitazamo yote ambayo msingi wake hutumika kuendeleza mfumo wa kiuchumi na siasa baina ya watu. Haya, hujumuisha maoni ya binadamu yeyote ulimwenguni kuhusu yote anayoyafikiria, anayoyasema na anayoyatenda katika shughuli za kiuchumi, kidini, kijamii na vilevile katika kisiasa. Mitazamo hiyo hubadilika kadri mfumo huu unavyobadilika kutokana na mpito wa wakati na hivyo jamii na hizo imani huendelea kubadilika. Kwa mfano, itikadi za kidini ambazo hutumiwa na mifumo

ya ukabaila pamoja na kibepari ili kuwafanya waumini waamini kuwa viongozi huwakilisha Mungu. Vilevile, waumini huamini kuwa kila jambo au tukio limepangwa na Mungu na kila binadamu ana jukumu ambalo Mungu amempangia. Inamaana kuwa yanayotokea ulimwenguni kama vile binadamu kuwa tajiri au mchochole ni mpango wa Mungu. Hivyo, hakuna yeyote ambaye ana uwezo wa kujiondoa katika hali aliyomo kwani yote yamepangwa na Mungu.

Ili kuleta mapinduzi katika jamii, Karl Marx aliorodhesha hatua tatu kuu ambazo zilifuatwa (Karl Marx, 1979). Hatua hizi ni kwanza ishitiraki ambapo binadamu watangamana kwa ushiriki wa pamoja na kuleta manufaa katika jamii kwa ujumla. Hatua ya pili ni biashara ndogo ambazo zilipeleka kukua kwa tabaka la wafanyikazi. Tatu, mfumo wa kibeberu kibwanyenye ambao uliotokana na unayanyasaji na ukandamizaji wa vibarua kwa manufaa ya matajiri pekee. Mfumo huu ulipelekea kuwepo kwa migogoro ya kitabaka na kuleta mapinduzi na kuendeleza mfumo wa kijamaa unaoleta usawa wa binadamu wote. Kwake Karl Marx, itikadi ambazo huangazia mambo ya kidini ni za uongo na hali za kiuchumi katika jamii ndizo zinapaswa kuelekeza fikra, imani na mielekeo yote ya kijamii.

Mihimili itakaotuongoza ni:

Itikadi huwa ungamuzi potoshi. Yaani, imani na fikra huwa uongo. Hii inamaana kuwa imani, fikra na mitazamo hiyo hutumika na tabaka la juu ili kuendelea kuwanyanyasa watu bila wao kujua kuwa wananyanyaswa. Mhimili huu utatusaidia kujua itikadi katika mashairi ya Muyaka kwani mashairi hayo yanajumuisha matumizi ya dini, migao ya kitabaka na nyenzo za kiutawala ambazo zinaendeleza unyanyasaji. Hivyo tunawapata wanajamii kwa kuongozwa na mtunzi, walisimama kidete na kuondoa ile minyororo ya wakandamizaji na utawala wa wakoloni. Hivyo mtunzi anapelekea kuleta mapinduzi katika jamii na kudhihirisha

ule uhuru wake wa kiakili wa kushughulikia masuala ya sokoni, anashughulikia vita na utawala kwa uwazi kando na ule utunzi wa kirasimi.

Historia ya jamii ulimwenguni ni migogoro ya tabaka mbalimbali. Mapinduzi yanapotokea na kufaulu, mifumo ya uzalishaji mali huchukua mkondo mwingine ili kuwa bora zaidi na kuwanufaisha wanajamii. Binadamu kila wakati huwa katika pilka pilka za kuboresha hali yao ya maisha. Mhimili huu utatusaidia kujua mapambano yanayopatikana katika jamii ya Muyaka. Mapambano hayo ndio chanzo cha imani na fikra ambazo zimemfanya Muyaka kuwasilisha kazi yake jinsi ilivyo. Hivyo, utenzi wake kuwasilisha masuala kwa namna tofauti ikilinganishwa na Mwanakupona. Tunampata mtunzi akishughulikia mambo mengi katika jamii kama vita, ukulima, uvuvi, usafiri na hata uongozi wa wakati wake. Kando na namna utunzi wa mashairi wa kipindi cha kirasimi ulivyoegemea tu kwa masuala ya kidini, kiutamaduni na ndoa kama ilivyo katika *Utenzi wa Mwanakupona*.

**Pili, mrengo wa Louis Althusser (1981).** Althusser anakosa kuafikiana na mrengo wa Karl Marx. Louis Althusser ameifafanua dhana hii kama mielekeo, fikra na imani ambazo hutumika na tabaka tawala ambalo husheheni viongozi wa serikali, na amejikita katika vyombo vya kiitikadi na kiudhibiti. Vyombo hivi hutumika ili kuendeleza mahitaji ya watawala ili kujinufaisha wao wenyewe. Kuna vyombo visivyo na matumizi ya nguvu au kulazimisha na pia vile ambavyo hutumia nguvu. Anaendelea kusema kuwa dini kama chombo cha kiitikadi, kilitumika mno kabla ya kipindi cha ubepari kufanikisha imani na matakwa ya tabaka la juu. Vilevile, elimu ni kifaa ambacho hutumiwa na watawala bepari ambapo binadamu yeyote hufunzwa itikadi inayomtayarisha kwa yote atakayoyafanya. Haya ni wakiwemo katika jamii iliyona migawanyiko ya kitabaka kama wanadhulumiwa, wanyanyasaji na wanaoendeleza imani za tabaka la juu ambalo ni tabaka tawala kitaaluma na

kadhalika. Wenye mali huweza kudhibiti wasio na mali kwa nguvu au kwa ukubalifu wao.

Mhimili utakaotuongoza ni:

Kuna vyombo vya kuidhibiti na kiutawala ambavyo vinajumuisha matumizi ya nguvu na visivyo vya matumizi ya nguvu. Vinavyotumia nguvu ni kama jeshi, mahakama, polisi, serikali na magereza na vinginevyo. Vyombo hivi hutumika kwa nguvu pale ambapo watu hawajiamulii vitu kwa hiari yao ili kuendeleza na kuhifadhi matakwa ya tabala tawala. Kwa upande mwingine, kuna vyombo visivyo vya moja kwa moja, yaani, hakuna matumizi ya nguvu. Vyombo hivi ni kama siasa, vyombo vya habari, dini, elimu, utamaduni na sheria. Kupitia mhimili huu, fikra, imani, mielekeo na matamanio hupitishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Binadamu huandaliwa kwa majukumu na kukubali hali yao katika jamii kupitia vyombo vya kiitikadi. Itikadi hii huweza kulinda na kuhifadhi hali ilivyo maishani ili kuendeleza matakwa ya tabaka la juu kwa matumizi ya vyombo vya kiitikadi vya kiutawala na kiudhibiti au kwa kutumia mamlaka na nguvu.

Mhimili huu utatusadia kubaini vyombo vya kiitikadi vinavyopatikana katika mashairi ya Muyaka. Vyombo vilivyojitokeza ni kama dini, elimu, utamaduni, sheria na hata vita na serikali. Vyombo hivi vitatusaidia kuelewa itikadi na pia kuona jinsi itikadi hizo zimepelekea uwasilishaji wa maudhui fulani. Kama vile Muyaka anavyozungumzia utawala wa kipindi chake wa wakoloni na walivyoondoa huo uongozi. Hapa Muyaka anashughulikia mambo ya sokoni ambayo hayakujumuishwa katika uandishi wa mashairi wa kipindi cha urasimi mkongwe.

**Tatu, mrengo wa Antonio Gramsci (1985).** Hapa, itikadi imeelezwa kuwa ni kukubali na kuzoea mambo ila si kwa kutumia nguvu. Katika ufafanuzi wa dhana ya itikadi, mwanakomunisti, mwanaharakati na kiongozi wa kisiasa Antonio Gramsci (1891-1937)

anahusishwa na dhana ya hejemonia. Kama Anderson anavyosema, Gramsci anatumia "hejemonia" kutoa nadharia sio tu hali muhimu ya kupinduliwa kwa mafanikio ya ubepari (kwa mfano, wakulima) (Hoare na Smith, 1971).

Neno "Hejemonia" lilitokana na neno la Kigiriki egemonia, ambalo mzizi wake ni '*egemon*,' linalomaanisha "kiongozi au mtawala " (Williams, 1985). Neno hili linamaanisha hali ya kikundi fulani kukubalika na kutawala kikundi kingine bila kutumia mabavu. Gramsci (1985) anafafanua hejemonia kama aina ya udhibiti ambao hutekelezwa na tabaka tawala; kundi linalodhibiti njia za uzalishaji mali. Kulingana na Gramsci, tabaka tawala lilikuwa la mabepari, wanaofafanuliwa katika Ilani ya Kikomunisti kama "*tabaka la Mabepari wa kisasa, wamiliki wa njia za uzalishaji wa kijamii na waajiri wa wafanyikazi wa ujira.* " Tabaka la chini (makabwela) lilikuwa na uwezo wa kuleta mapinduzi. Kundi hili lilijumuisha vibarua ambao hawakuwa na njia za kuzalisha mali yao ila waliwafanyia kazi waliokatika tabaka la juu (Hoare na Smith, 1971). Lakini hawakuleta mapinduzi kwani walikuwa wamefanywa kuzoea hali yao na walifanywa kukubali na kuwajibikia tabaka tawala.

Mihimili itakayotuongoza ni :

Watu wananyanyaswa kwa ukubali wao wenyewe ila sio kwa matumizi ya nguvu. Mhimili huu utatufaa kuchanganua itikadi katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Mhimili huu unamaana kuwa hakuna matumizi ya nguvu bali ni hiari ya watu ambayo inatumiwa kuwakandamiza bila wao kujua kuwa wanakandamizwa. Huu ni ukubalifu na ukawaida unaoendelezwa na watu katika tabaka la juu. Hivyo, Mwanakupona anapata fikra, mitazamo na mielekeo fulani kutokana na aliyozoea. Yale mazoea tunaona yamezama akilini mwa mtunzi na ni matukio ya kawaida. Tunampata mtunzi akiyazoea matukio

katika mazingira yake na anayapitisha kwa bintiye. Hapa mtunzi anazoeshwa matukio ya kawaida na anayapitisha bila matumizi yoyote ya nguvu k.v jeshi, mahakama na polisi. Tabaka tawala hutumia vigeu vya kiitikadi kama vile dini, utamaduni, serikali, familia, miongoni mwa mengine. Kupitia mhimili huu vigeu hivi hudhaniwa kuwa vitu vya kawaida. Hivyo watu huona ni halali bila kujua kuwa wananyanyaswa kwa kuenda shuleni, kanisani ama hata matumizi ya vyombo vya habari ambavyo huwaelekeza kunyanyaswa bila kulazimishwa na yeyote. Vigeu hivi, hutumiwa na walio kwenye mamlaka ili kuweza kuendeleza mifumo yao ya kumiliki na kuzalisha mali katika jamii bila kupingwa na yeyote, haswa, walio katika tabaka la chini. Mhimili huu utatumika kufanikisha utafiti katika kubaini athari za itikadi za Mwanakupona katika uwasilishaji wa maudhui na mtindo katika mashairi yake. K.m, Mwanakupona anayazoea mambo katika jamii na tunapata akimwambia bintiye atii dini, ndoa na hata utamaduni ili aweze kupata maisha marefu na aende peponi.

### 1.9 Mbinu Za Utafiti

Sehemu hii ilishughulikia muundo wa utafiti, mahali pa kufanyia utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo ya utafiti na maadili yatakayoongoza utafiti.

#### 1.9.1 Muundo Wa Utafiti

Kazi hii ilitumia muundo wa kimaelezo. Kulingana na Kothari (2004), muundo wa utafiti unarejelea mkakati wa jumla ambao mtu anaweza kuchagua kuunganisha vipengele mbalimbali vya utafiti. Haya hufanywa ili kuhakikisha kuwa mtafiti ameshughulikia kikamilifu tatizo la urtafiti. Anaendelea kusema kuwa muundo wa utafiti ni ramani ya ukusanyaji data, kipimo na uchanganuzi wa data yenyewe. Isitoshe, Kombo na Tromp

(2006), wanaeleza kuwa muundo wa kimaelezo hutumika kueleza mielekeo ya watu, maoni na tabia zao na pia huweza kutumika kuelezea maswala ya kielimu, kisiasa na kijamii. Kupitia muundo huu maelezo yalitumiwa kutoa ufafanuzi wa itikadi, beti na mishororo inayoashiria itikadi na jinsi zinavyopelekea uwasilishaji wa maudhui na mitindo.

### 1.9.2 Mahali Pa Kufanyia Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta na ulifanywa kwa kutafiti na kutathmini kazi mbalimbali za wataalamu zinazohusiana na mada yetu na zilizochangia kufanikisha malengo ya utafiti. Maktabani, mtafiti pia alisoma na kuchambua kwa kina mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* ambapo mtafiti alidondoa shairi, beti na hata mishororo inayodhihirisha itikadi.

### 1.9.3 Uteuzi Wa Sampuli

Mugenda na Mugenda (2019) wanasema kuwa sampuli inarejelea sehemu ndogo ya kitu inayochaguliwa katika vitu vingi kwa ajili ya kuwakilisha jumuiya nzima. Vilevile, sampuli ni sehemu ya idadi maalum ya watu ambayo mtafiti atatumia katika ukusanyaji wa data zitakazomsaidia kufikia malengo ya utafiti wake (Mugenda na Mugenda, 2003). Creswell (2007) anadai kuwa sampuli ya kimakusudi ni aina ya sampuli iliyochaguliwa na mtafiti kwa misingi ya sifa anazozichunguzia katika kundi nzima yake. Nakubaliana na kauli ya Creswell (2007) kuhusu pambanua yake ya sampuli ya kimakusudi na kauli yake ilifaa katika utafiti uliotekelezwa.

Mada yetu inachuguza itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Tenzi hizi mbili ziliteuliwa kimaksudi miongoni mwa tenzi za kwanza ambazo zilijumuisha utenzi wa Fumo Liyongo (1913), Al- Inkishafi (1800), vita vya wadachi

kutamalaki Mrima (1895), vita vya majimaji (1910), mashairi ya Muyaka (1800-1840), Utenzi wa Mwanakupona (1858), miongoni mwa tenzi zingine. Tenzi hizi mbili, *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka, ambazo ziliteuliwa miongoni mwa tenzi za kirasmi, zilitupa data ya kutosha ya kuweza kushughulikia mada husika ya itikadi na pia kulingaisha itikadi zilizowaongoza watunzi hawa wawili. Pia, alitumia sampuli hii kuteua mashairi, beti na mishororo inayodhihirisha dhana za kiitikadi katika kazi teule.

Mugenda na Mugenda (1999) wanaeleza kuwa uteuzi wa sampuli ya kimakusudi unafaa katika utafiti wenye muundo wa kimaelezo ambao lengo lake kuu ni kupata habari au data kwa misingi ya malengo ya utafiti husika. Pia, ni kwa msingi huu, mtafiti aliteua mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* ili kufanikisha utafiti huu.

### 1.9.4 Ukusanyaji Wa Data

Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa ulifanywa katika maktaba, mbinu zilizotumika ni usomaji na udondoaji. Vitabu teule, mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* vilitumika. Mtafiti alidondoa beti, mashairi na maneno yaliyothihirisha itikadi. Usomaji wa kina kuhusu nadharia ya itikadi pia ulifanyika kwa kusoma tasnifu, majarida na vitabu mbalimbali ili kupata kufanikisha utafiti.

Mambo yalinakiliwa ili kurahisisha uchanganuzi. Hivyo, tofauti zinazojitokeza katika jinsi watunzi hawa wawili wanavyoongozwa na itikadi tofauti na kuweza kuwasilisha kazi yao kwa namna tofauti ingawa walikuwa watunzi wa kipindi kimoja.

### 1.9.5 Uchanganuzi Wa Data

Data ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo na ufafanuzi kwa kurejelea malengo ya utafiti. Malengo haya ni kubaini itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Pili, kubaini jinsi athari za itikadi zinavyopelekea uwasilishaji wa maudhui kwenye

mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Tatu, kuchunguza athari za itikadi katika uwasilishaji wa mtindo katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Vilevle, data ilichaganuliwa kwa kutumia maelezo katika misingi ya nadharia ya itikadi na pengo lililotarajiwa kuzibiwa.

### 1.9.6 Uwasilishaji Wa Data

Mbinu ya kimaelezo na utoaji mifano mwafaka ya kuthibitisha, ilitunika katika kuwasilisha matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yalithibitisha malengo ya utafiti kwa mujibu wa mada na maswali ya utafiti. Vilevile, kazi hii iliangazia itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*, maudhui na mtindo kupitia uchanganuzi wa nadharia ya itikadi.

### 1.9.7 Maadili Ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maadili kwa kina. Mtafiti alihakikisha kuwa amepewa kibali cha kufanya utafiti na shule ya fani na sayansi ya jamii katika chuo kikuu cha Kenyatta na pia NACOSTI. Aidha, kazi zote zilizotumika kufanikisha utafiti zilinakiliwa katika marejeleo. Pia, utafiti ulikuwa na uyakinifu bila kuwa na mapendeleo ya aina yoyote. Vilevile, mtafiti alihakikisha kuwa utafiti haujafanywa katika Chuo kingine chochote na marejeleo yaliyotumika kunakiliwa.

## 1.10 Hitimisho

Sehemu hii ilijumuisha utangulizi wa utafiti. Tulishughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Vilevile, tulieleza sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti wetu. Katika yaliyoandikwa kuhusu mada tulionyesha kazi zilizofanywa za awali kuhusu itikadi, *Utenzi wa Mwanakupona* na hata mashairi ya Muyaka. Isitoshe, tuliendelea kufafanua nadharia yetu ya itikadi mikabala ya Karl Marx,

Louis Althusser na Antonio Gramsci. Mwisho tulijadili mbinu za utafiti wetu ambazo zilijumuisha muundo wa utafiti, mahali pa kufanyia utafiti na uteuzi wa sampuli, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data na maadili ya utafiti.

Sura iliyofuata tulichanganua na kulinganisha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*.

## SURA YA PILI

## ULINGANISHAJI WA ITIKADI KATIKA *UTENZI WA MWANAKUPONA* NA MASHAIRI YA MUYAKA

### 2.0 Utangulizi

Sura hii imechanganua na kuzilinganisha itikadi katika *Utenzi wa Mwanakupona* na mashairi ya Muyaka. Muyaka Bin Haji (1776 – 1840) na Mwanakupona ni watunzi wa kipindi kimoja cha kirasimi lakini utofauti wa kimaudhui na kimtindo unajitokeza. Haya yamesababishwa na tofauti zinazowaongoza watunzi hawa wawili. Tulichambua mashairi ya Muyaka kwa kufuatia nadharia ya kiitikadi mrengo wa Karl Marx (1977) kwani katika mashairi yake kuna matumizi ya nguvu na vita vya kiserikali kwa kutumia vipengele vya kiitikadi kama ilivyojadiliwa na Althusser (1981). Vilevile mtafiti alichambua itikadi zilizomwongoza Mwanakupona kwa kufuatia mkabala wa Gramsci (1985) kwani mtunzi alisisitiza utii wa hali ya juu wa dini, tamaduni, ndoa na hata sharia kwa hiari yake mwenyewe. Anaendeleza yale aliyoyapata yakiendelezwa katika jamii yake. Hivyo mtunzi anatumia hejemonia ya tamaduni na dini kuendeleza yaliyoko katika jamii na kuyafanya yakae masuala ya kawaida ambayo yanapaswa kufuatwa bila ukinzani wowote. Hapa itikadi inaendelezwa kwa hiari bali si matumizi yoyote ya nguvu.

### 2.1 Itikadi Katika Mashairi Ya Muyaka

Kulingana na Mohammed (1995) itikadi ni imani ambazo huelekeza matendo yote ya binadamu yeyote ulimwenguni na huathiri watunzi katika kazi zao. Muyaka ni mzawa wa mji wa Mvita, ukoo wa Myinyi, Malindi. Alikuwa mfanyabiashara mashuhuri ila hakufanikiwa sana katika shughuli ya biashara. Kutokana na shughuli zake za biashara aliweza kufika sehemu mbalimbali kama Pemba, Bara Hindi, Uarabuni, Ngazija na Unguja.

Tungo zake nyingi zinasimulia maisha ya masuala ya jamii kwa ujumla kwani utunzi huathiriwa na kupewa mwelekeo fulani na mazingira ya mtunzi (Munyole, 2017). Hali hii ilituwezesha kutaka kubaini itikadi zilizomwongoza Muyaka katika mashairi yake.

### 2.1.1 Itikadi Ya Mapinduzi Ya Nguvu

Kwa mujibu wa Marx (1977), itikadi ni zana ya kudhibiti jamii na kudumisha matabaka mawili makuu. Anaorodhesha matabaka haya ifuatavyo; tabaka tawala ambalo ni la wenye vyombo vya uzalishaji mali na tabaka la waliotawaliwa ambalo linasheheni wanaofanya kazi kwa watawala. Kupitia mawazo yake Karl Marx, tunapata kuwa tabaka la watawaliwa hutangamana pamoja ili kubadilisha hali iliyoko katika jamii yao. Mawazo haya ya Marx ya mapambano ya kuleta mabadiliko katika jamii tunayapata katika jamii ya Mvita na yalichangia itikadi hii ya mapinduzi ya nguvu.

Kwa mujibu wa BAKITA (2015) mapinduzi ya nguvu ni mabadiliko muhimu katika jamii ya namna watu wanavyofanya vitu au mambo kwa kutumia nguvu. Itikadi hii ilijitokeza katika mashairi ya Muyaka kwa upana kwani kuna migao wa kitabaka katika mashairi ya yake mtunzi.

Tungo nyingi za mtunzi zilikuwa za wakati wa ukoloni wa Omani na Waarabu mjini Mombasa. Tungo hizo zilijikita sana katika mapinduzi yaliyohusu vita vya upiganiaji uhuru na uzalendo. Katika kipindi hiki, mji wa Mombasa ulikuwa unashuhudia vita vikali. Mtunzi anaonyesha jinsi wenyeji walivyojikaza ili kuleta mapinduzi ya nguvu katika jamii ili kuikata miyororo ya ukoloni na unyanyasaji na pia kupinga juhudi za kutawaliwa. Hili linalipata katika shairi la, "*Vikija Mtaviweza*" (Abdulaziz 1979:133-134).

Muyaka hapa anavitaja vifaa na zana zilizotumika katika vita kama vile: mata, mafumo, ngao, p'anga, p'anga-kule, vitara, msu, ngurumza na fimbo. Pia anatueleza palikuwepo na

michezo na ngoma maalum za kuwafunza vijana vita na pia namna ya kutumia vifaa vile vya vita vizuri. Mfano bora ni pale mtunzi anataja ngoma ya kizungup'ia ambayo ilihusisha mchezo wa vita uliohitaji matumizi ya nguvu na ulichezwa kando ya bahari.

Mashairi mengine pia yalinuia kuwapa nguvu watu wote wa pwani, dhidi ya ushambulizi na unyanyasaji wa Waarabu. Mfano "*Mjenga Nyumba Halali,*"; Muyaka anasema:

> *Risala wa K'ongowea mwenezi kafikilile*
>
> *Kambe na wasosikia maneno yangu wambile,*
>
> *Hawapati kuniraya naliwambia papale,"*
>
> *Mjenga nyumba halele, yulele, ukumbizani.* (Abdulaziz 1979, uk 124)

Katika ubeti huu mtunzi anamwambia mjumbe wake ampelekee watu wa Kongowea ujumbe kuwa hawana haki ya kumlaumu, kwa sababu aliwatahadharisha mapema kuhusu jambo fulani. Anaongeza kwa hekima kuwa "mjenga nyumba halele," akiwa na maana ya mtu anayefanya jambo muhimu au zuri hapumziki wala hakosi changamoto. Hivyo ni bora mtu awe mwangalifu na mwenye bidii ili waweze kupambana na yale mashambulizi.

Kulingana na Abdulaziz (1979), Zahidi bin Mgumi, mtawala wa Lamu, alitaka kujenga ukuta kuzunguka mji wake ili kuzuia mashambulizi ya Mombasa na Pate. Hivyo Muyaka alitunga shairi hilo ili kuwaambia watu wa Lamu kwamba watu wa Mombasa watafaulu kuuteka mji huo licha ya ukuta. Na hili lilipotokea wajenzi wa ukuta (nyumba yenye taa) wangejikuta wamelala nje, uani. Kutokana na hayo ni wazi kuwa mtunzi aliongozwa na itikadi ya mapinduzi ya nguvu kwani anashughulikia vita baina ya mji wa Lamu na Mombasa na Pate wakati wa ukoloni bila kuwaogopa watawala wa wakati huo. Hii ni sababu angedhaniwa kuwa inaibua rabsha baina na watawaliwa ambao wangewatimua watawala.

Isitoshe, itikadi ya mapinduzi ya nguvu pia ilijitokeza pale Muyaka anashughulikia suala la kushindwa kwa mji wa Mombasa. Katika mwaka 1835, Liwali Salim alifariki. Mazrui kwa upande mwingine walibishana kuhusu nani anafaa kumrithi. Hili lilikuwa pigo kubwa kwa umoja wa Mazrui na hivyo basi nguvu ya Mombasa. Mtoto wa Salim, Rashid, aliikamata Ngome hiyo huku wapinzani wake wakiongozwa na ndugu wawili wa Salim wakishikilia mji huo. Mkwamo huo ulidumu zaidi ya mwaka mmoja.

Wakati huo Waswahili wa Mombasa walikuwa wamechoshwa na tabia ya Mazrui kuhusu urithi na hawakuwa tayari tena kuwa na mtu wa familia hii kama gavana wa Mombasa. Kwa hiyo Muallem Shafi, Sheikh wa Kilindini, na viongozi wengine wa Waswahili walikwenda Muscat na kuomba aingilie kati Said. Said alichukua fursa hiyo lakini badala ya kufanya shambulio la moja kwa moja, ambalo lingeweza kuwaunganisha, Mazrui aliungana na Rashid na kumthibitisha kweli kuwa gavana mnamo 1836. Kwa sharti kwamba Rashid aihame Ngome hiyo. Rashid alikubali bila kujua. Said aliimiliki Ngome hiyo na kuweka askari 500. Alimpa Rashid ugavana wa Pemba na Mafia au pensheni kubwa badala yake, kwa sharti kwamba aondoke Mombasa na kuishi Zanzibar, mji mkuu wa baadaye wa Said. Rashid alikataa. Watu wa Said walimkamata Rashid. Utawala wake ulifikia kikomo na vuguvugu la upinzani dhidi ya utawala wa Oman likaporomoka. Said akawa mtawala asiyepingwa wa Mombasa na maeneo mengine ya Pwani.

Itikadi ya mapinduzi ya nguvu pia ilijitokeza katika shairi la '*Ai Mambo*' Muyaka anasema kuwa kuna mambo mengi ambayo yajayo. Anamwambia Bwana Mjombo, kumaanisha mtu muoga, aondoke pamoja na marafiki waliosalia. Jina hilo huenda lilikuwa jina la majazi. Mtunzi anasema:

*Ai mambo ai mambo makuu yayao,*

*Ondoka Bwana mjombo na wenzio waseleo,*

*Wangoma wenele fimbo za t'utu na kiwapio,*

*Napakiwa mke nduyo nae mwondole ndiani. (*Abdulaziz 1979, uk. 217)

Katika ubeti huu Muyaka anazungumzia mambo makuu ambayo anasema kuwa yanakuja. Anawaambia wanaocheza ngoma nao wamejihami na fimbo za t'utu na kiwapio kwa pamoja. Naye mke wa nduguyo kama yupo, pia aondolewe njiani. Hapa huenda shairi hili linarejelea vita walivyokuwa wakivitarajia wakati huo. Kutokana na hayo mtunzi alidhihirisha itikadi ya mapinduzi ya nguvu kwani vita hivyo vilikuwa vya kupigania uhuru na uzalendo wa wanajamii husika dhidi wa mkoloni. Mishororo wa mwisho nao unamaanisha kuwa yule adui anayekuja atafedheheshwa sana hivi kwamba wanawake hawakupaswa kuwa karibu. (Abdulaziz, 1979).

Shairi la "*Mali na Heshima.*":

*"Akitajirika, mja hupata heshima,*

*Maskini anashindwa, hata kauli hajapata."* (Abdulaziz, uk. 36)

Kufuatia natharia ya itikadi mkabala wa Marx (1977), Muyaka hapa anakosoa mfumo wa kiuchumi wa kimatabaka, ambapo heshima na nafasi ya mtu hutegemea mali. Anaonyesha kwamba mamlaka na heshima zinadhibitiwa na tabaka la matajiri, huku maskini wakikosa sauti na ushawishi. Hii ni ishara ya unyonyaji wa kiuchumi ambapo tabaka la juu linanufaika kwa kutumia kazi ya tabaka la chini. Kufuatia kipengele hiki, ilidhihirika kuwa Muyaka aliongozwa na itikadi ya mapinduzi ya nguvu. Muyaka aliichora migao ya kitabaka ambayo ilitumika kupitisha itikadi. Tunapata Marx akisema kuwa imani zinazofikiriwa, zinazosemwa na zinazotendwa na tabaka la juu kwa tabaka la chini, ndizo zinazotumika kuwakandamiza. Tabaka la juu linaonekana kusheheni zana za kiuchumi,

kidini, kijamii na hata kisiasa. Na baadaye mabadiliko huletwa katika jamii kwa walio chini kujiinua wenyewe.

Muyaka hapa alidhihirisha itikadi ya mapinduzi ya nguvu kwa kutunga shairi za kuwashawishi wenyeji kuleta mabadiliko katika jamii. Utunzi wake ulitetea haki za wanajamii na pia kuondoa utawala wa wakandamizaji. Pia alizungumzia utawala uliokuwa katika kipindi kile. Upekee wa utunzi wake ulijitokeza kupitia itikadi hii kwani alishughulikia masuala yanahusu serikali, vita na ata mapambano ya vikundi mbalimbali kando ya utunzi uliokuwa unatawala katika kipindi hiki cha urasimi. Utunzi wa kipindi hicho ulijumuisha utunzi wa masuala ya kidini na kihistoria naye mtunzi aliwahimiza wanajamii katika vita ili kujiondoa katika unyanyasaji na kujinyakulia uhuru.

### 2.1.2 Itikadi Ya Ukandamizaji

Kulingana na BAKITA (2015), ukandamizaji ni hali ya kikundi kimoja kunyima haki watu wengine katika masuala ya kiuchumi, kijinsia na kisiasa. Louis Althusser (1981) anaamini kuwa itikadi inadhibiti jamii kwa kutumia vyombo vya dola na vyombo vya kiitikadi. Kupitia mawazo yake, itikadi ya ukandamizaji inajitokeza katika kazi ya Muyaka kupitia mapenzi na ndoa kama kipengele cha kiitikadi (Althusser, 1981).

#### 2.1.2.1 Mapenzi Na Ndoa

Ndoa na mapenzi ni vyombo vya kiitikadi vinavyokamilishana ili kujenga familia. Familia ni chombo muhimu kwani hakuna jamii bila familia. Kupitia mawazo ya Althusser, itikadi ya ukandamizaji ilijitokeza kupitia kipengele cha mapenzi katika shairi la '*Kuonana na wewe*,' ukurasa 238. Katika shairi hili, mtunzi anamuomba mpenziwe kufanya lolote ili waweze kukutana. Katika jamii hii ya Kiislamu wa wakati wa Muyaka, wanawake walikuwa wamewekewa vikwazo vya kitamaduni na walihitajika kufuata. Kwa mfano,

uhusiano na pia kukutana baina ya wapenzi ilikuwa vigumu sana. Kutokana na hayo, ni dhahiri kuwa hizo imani, fikra na hata mitazamo iliyofuatwa na wanandoa, iliwakandamiza wanajamii bila wao kujua lakini wameyazoea kuwa mambo ya kawaida kulingana na utamaduni na dini ya Kiislamu. Kwa mfano, katika hilo shairi hakuna uhuru wa mtu atakama yu mzima, kufanyia anachotaka. Kama vile vikwazo vinavyomzuia mtu kupatana na mpenziwe. Hizo ni imani potofu kwa mujibu wa Marx (1977) ambazo Muyaka aliamua kuzizungumzia hivyo kuzikiuka na kumwambia mpenziwe afanye chochote ili waweze kupatana. Ujumbe huu pia unaoana na yaliyo katika shairi la ‘*Laiti siwele nyuni*,’ katika ukurasa 328. Shairi hili pia ni usemi wa kutamani na ombi la kuruhusiwa kumtembelea mpenzi wake.

Itikadi hii kupitia mapenzi pia ipo katika shairi la ‘*Ateteyae mtuku,*’ ukurasa 288. Mtunzi anasema:

*Sambwe ilipotekeza ikavundika mk’uku,*

*Usiku wali wa kiza wa huku hawaoni huku,*

*Ndipo twalipo ikweza, tukaichelea mwiku,*

*Ateteyae mtuku ni tangauko la bure.* (Abdulaziz 1979, uk.288)

Katika shairi hili mtunzi anajisuta kwa kupotoka na kujihusisha na mwanamke asiyefaa na aliyemletea shida. Katika mishororo wa tatu, Muyaka anamrejelea kama ‘mtuku.’ Ndio maana anasema kuwa ‘ateteyae mtuku ni tanguko la bure.’ Tanguko ikiwa na maana kuwa ni kama kujisumbua. Kutokana na hayo ni wazi kuwa mtunzi analalamika kwa kujihusisha na mwanamke asiyefaa. Tunapata kuwa anajisuta kwa kujikandamiza yeye mwenyewe kwani anasema yule mwanamke alimletea shida. Hivyo itikadi ya ukandamizaji wa kijinsia ilijitokeza pale kwani yule mwanamke anamfanyia Muyaka mambo yaliyomletea mawazo,

na kumfanya ajisute kwa kujihusisha na yule mwanamke.

Suala hili pia linaoana na yaliyomo katika shairi la '*Ndia mbili zaumiza*,' ukurasa 332. Shairi hili linaeleza hisia za mtunzi za kusalitiwa na mkewe. Muyaka naye hana amani, hasemi, hana furaha wala kicheko. Haya yanapelekea mtunzi kupatwa na huzuni kwani yule mwanamke hamuelewi wala kuwa na tabia bora. Hapa, mwanamke huyu anamkandamiza mtunzi wa kumfanya awaze na kukosa furaha na kicheko. Muyaka anasema kuwa alidhani kuwa yeye ndiye mpenzi wa yule mwanamke peke yake lakini anahuzunishwa na tabia yake ya kumpenda mwanamume mwingine. Hivyo mtunzi anamwambia njia mbili zaumiza. Mtunzi hapa alithihirisha itikadi ya ukandamizaji kwani alisalitiwa na mkewe katika ndoa. Mtunzi amepelekea kusema kuwa yule mwanamke anampa mawazo na kupelekea kiakili. Haya yanamfanya kukosa furaha.

### 2.1.3. Itikadi Ya Uhuru

Karl Marx (1977) alihimiza mapinduzi kutoka kwa jamii ya kiunyonyaji kwenda kwa jamii yenye usawa. Muyaka katika mashairi yake anabadilisha uandishi wake kutoka kwa utunzi unaoegemea dini na kujikita katika masuala ya sokoni ili kuwaelimisha watu yanayoendelea katika jamii na kushughulikia mazingira kwa jumla. Mtunzi hapa aliongozwa na itikadi maalum ya uhuru wa kiakili iliyomfanya asawiri kazi yake kwa namna ya upekee kando na watunzi wengine walioishi katika kipindi cha urasimi. Kulingana na BAKITA (2015), uhuru ni hali ambapo mtu anapata uwezo wa kutenda au kuishi kama apendavyo bila kizuiwa na chochote au yeyote. Vyombo vya kiitikadi vya Althusser (1981) vitatumika hapa. Vyombo hivi vinaonyesha upekee wa utunzi wake ifuatavyo ;

#### 2.1.3.1 Mapenzi Na Ndoa

Kama inavyojadiliwa na Gramsci (1985), mapenzi na ndoa ni kigeu ambacho kimo chini ya kipengele cha ayali. Kwa mujibu wa BAKITA (2015), ayali ni jumla ya watu wanaoishi katika nyumba moja wenye uhusiano wa kindugu na kinasaba. Ili watu wawe na ule uhusiano ni sharti mapenzi na ndoa zikuwemo. Mwanamume na mwanamke, huweza kupendana na kuvutiana kisha wakawa na maridhiano halali ya kuishi pamoja wakiwa mume na me. Kipengele hiki katika mashairi ya Muyaka kilidhihirisha uhuru wa kiakili wa mwandishi wa utunzi wa masuala kwa uwazi. Haya ni kupitia jinsi mtunzi anasawiri dhana ya mapenzi na ndoa.

Kipengele cha mapenzi pia kinapatikana katika ukurasa 238, katika shairi la, '*Kuonana na wewe*.' Katika shairi hili, mtunzi anamuomba mpenziwe kufanyia lolote ili waweze kukutana. Katika jamii hii ya Kiislamu wa wakati wa Muyaka, wanawake walikuwa wameekewa vikwazo vya kitamaduni na walihitajika kufuata. Kwa mfano, uhusiano na pia kukutana baina ya wapenzi ilikuwa vigumu sana. Kutokana na hayo, ni dhahiri kuwa hizo imani, fikra na hata mitazamo iliyofuatwa na wanandoa, iliwakandamiza wanajamii. Kwa mfano, katika hilo shairi hakuna uhuru wa watu atakama yu mzima, kufanyia anachotaka. Matukio haya ya kawaida hupokelewa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine na Muyaka anakiuka kaida hizi.  Muyaka alizizungumzia kwa uwazi na hivyo kuzikiuka pale alimwambia mpenziwe afanye chochote ili waweze kupatana. Haya yalidhihirisha uhuru wa kiakili wa mtunzi.

Ujumbe huu pia ulioana na ujumbe katika shairi la '*Laiti siwele nyuni*,' katika ukurasa 328. Shairi hili pia ni usemi wa kutamani na ombi la kuruhusiwa kumtembelea mpenzi wake lakini mtunzi anasikitika kuwa hana idhini. Hili linathihirisha kuwa kulingana na jamii ya

Muyaka, mapenzi na pia kupatana kwa watu wapendanano kulikataliwa. Haswa, bila idhini wa wazazi. Lakini Muyaka anakiuka haya kulingana na utamaduni pamoja na dini, na kuyashughulikia katika mashairi wake. Kupitia hayo basi ni dhahiri kuwa mtunzi aliongozwa na itikadi ya uhuru wa kiakili sababu anashughulikia masuala kwa namna tofauti na ukawaida ulioko katika jamii.

Uhuru wa mtunzi pia upo katika shairi la '*Musiwate kuonana*,' katika ukurasa 314. Katika shairi hili Muyaka anamtuma mjumbe wa Kongowea kwa mpenzi wake ili amsalimie. Muyaka anamwambia mjumbe aongee naye na amwambie kuwa ametumwa na "Bwana." Mjumbe pia asema kuwa ni lazima wakutane na Muyaka siku hio ili waweze kuonyeshana hisia zao kwa kina ambazo zimo moyoni. Kwa hiyo tunapata kuwa mtunzi alithihirisha uhuru wake wa kiakili wa kuleta mapinduzi ya kaida na tamaduni za Kiislamu na kuzungumzia mambo ya kihisia kwa uwazi kando na mambo ya kidini yalitokuwa yameutawala uwanja wa tungo za kirasimi.

Suala hili la ndoa pia limo katika shairi la '*Harusi ya Bwana Muyaka*,' katika ukurasa 278. Shairi hili linaanza kwa Bwana Muyaka kupewa njia siku ya arusi yake huku vigelegele vikipigwa. Tunapata pia Muyaka anajisifu kwamba mtu yeyote asitilie shaka uume wake. Kulingana na utamaduni wa Waswahili, imekuwa desturi kwa bwana harusi kufunga ndoa na kufanyia tendo la mapenzi ili kudhibitisha uume wake na ubikira wa mkewe. Haya hufanyika ili kutoboa kizinda ili damu itoke na kushuhudiwa na jamaa na marafiki kama ubikira wa msichana upo. Hivyo, katika shairi hili Muyaka anawahakikishia jamaa na marafiki zake kuwa hatawaangusha. Kutokana na hayo uhuru wa kiakili wa mtunzi unathihirika kupitia suala hili la kufanyia mapenzi siku ya harusi ili kudhibitisha uume na ubikira. Masuala haya yalifungamana na tamaduni na vilevile dini ya Waswahili. Yalipewa

uzito na hayangetajwa kiholela. Lakini, tunapata Muyaka anayazungumzia kwa uwazi na kwa kina. Hivyo uhuru wake wa kiakili unajitokeza kutokana na kubadilisha mazoea na kuzungumzia matukio kama hayo kwa uwazi.

Kando na ndoa iliyosimama, mtunzi anashughulikia ukiukaji wa sheria za ndoa. Haya ni matukio ya kilimwengu, ambayo ni ya kawaida katika jamii. Muyaka anayazungumzia katika mashairi yake kwa uwazi, kando na Mwanakupona ambaye anaichora ndoa dhabiti tu. Haya tunayapata katika Shairi la '*Malalamiko ya mke,*' ukurasa 290. Katika shairi hili, mke analalamika sababu ya mume kumkataa bila ya sababu. Anamchukia kwani amezeeka lakini anafurahishwa na waposi wachanga wanaotaka kuposa ambao nao wanamchukia yule mke. Katika mwandamizi anauliza kama kuna yeyote anayeuza ujana ili yule mwanamke aununue. Katika ubeti wa pili anaongeza kuwa ingawa mumewe yu pamoja naye, ana jambo. Anaendelea kuuliza kama kuna haja gani yao kucheka ila ni kujilazimisha. Yule mwanamke anasema kuwa mumewe alijiletea hayo yote yeye mwenyewe. Anamuuliza mtu mwerevu kama yeye anawezaje kufanyia ujinga, 'kukumbika,' kisha kutaka kushauriwa. Mwisho, mtunzi anamshauri yule mwanamke asikumbuke yaliyotendeka ili asijute na asiweke machungu moyoni.

Kutokana na hayo, uhuru wa mtunzi wa kiakili ulidhihirika mtunzi alivyoshughulikia usaliti uliopatikana katika ndoa. Tunapata kuwa yule mke analalamika sababu mumewe anamkataa na anapendezwa na wasichana wachanga. Ujumbe huu pia unaoana na yanayopatika katika shairi la '*Mke wa Risasi*,' katika ukurasa 300. Hapa, Mtunzi anamlaani mja mwingine alimnyemelea na kumtaka mpenzi wake wa marehemi Risasi aliyekuwa katika eda. Kufuatia na imani za Waislamu, mjane akiwa katika eda hakutakikana kuolewa ama kujiingiza katika shughuli za mapenzi. Lakini mtunzi anatuonyesha bwana huyu

akivunja haya na kumtamani kimapenzi mjane wa Risasi. Kupitia hayo, uhuru wa kiakili wa mtunzi ulijitokeza kwa kushughulia masuala yote yaliyotokea katika jamii yake. Yawe masuala yaliyoendana au yawe yalikiuka sheria na kaida za jamii.

#### 2.1.3.2 Mfumo Wa Kiuchumi

Katika mashairi ya Muyaka, mfumo wa kiuchumi unajitokeza kupitia kilimo, biashara, uvuvi, Ufugaji, utengenezaji wa mashua, ufinyaji, uhunzi, mafundi ya Ngozi na ushonaji. Uchumi wa mji wa Mombasa wakati huo wa nusu ya karne ya kumi na tisa ulikuwa umeimarika sana na kupanuka. Muyaka hivo analeta mapinduzi katika uandishi wa ushairi wa kipindi chake kwa kuandika kuhusu mambo ya sokoni. Anaandika kuhusu masuala kando na utii wa dini, ndoa na utamaduni. Haya yamepelekea upekee wa mtunzi ikilinganishwa na Mwanakupona ambaye anafuata kanuni za uandishi wa Kirasimi wa mashairi.  Baadhi ya vitega uchumi alivyovitaja Muyaka katika mashairi yake ni :

Biashara ilikuwa inaendelezwa sana katika jamii hii ya mtunzi. Haya yanajitokeza katika ukurasa 166 katika shairi la '*Hindi ndiko kwenye nguo na Wendao uchi wako*.' Hapa, mji wa Mombasa ulikuwa unajihusisha sana kibiashara na nchi ya India. Wabiashara walibadilishana nafaka na nguo kutoka India na pembe za ndovu na pia watumwa kutoka Afrika Mashariki. Muyaka anaikejeli India katika shairi hili akisema kuwa atakama India ndiko nguo zinakotoka, kuna watu wengi sana wanaotembea uchi. Hivyo, uhuru wa mtunzi wa uandishi unajitokeza kwani tunapata akishughulikia masuala ya biashara ambayo hayakuwa katika kazi za kirasimi. Yaani anashughulikia masuala ya sokoni. Yeye mwenyewe alikuwa mwanabiashara. Misafara ya biashara ilitoka Mombasa kwenda magharibi kupitia Taita, Maasai na kuelekea mbali zaidi hadi kiwango cha kufikia maeneo ya ziwa Baringo.

Vilevile, mfumo wa kibiashara ulijitokeza kupitia uvuvi. Haya yalijitokeza katika ukurasa 172 katika shairi la ‘*Tanzi za nyama*.’

*T’anzi za nyama, t’anzi mkivimiza.*

*Kukanya wakurufunzi sote vyatusangaza*

*Tujile na yetu runzi twatafuta vya kuwaza*

*Mwauza, au ni mittuzi yenu ?* (Abdulaziz 1979)

Katika ubeti huu ni dhahiri Muyaka anazungumzia mvuvi ambaye hangepeana samaki kwa watu waliokuwepo wakitaka samaki. Watu hawa waliwasaidia wavuvi kuegemeza mashua zao walipotoka kuvua kwenye ziwa kuu. Lakini Muyaka anakasirishwa na tabia ya wale wavuvi ya kutowauzia samaki wala kuwabadilishia wale watu samaki na mchele. Hapa uhuru wa Muyaka wa kiakili unajitokeza kwani mtunzi anazungumzia uvuvi ambao uliwapa watu chakula. Anafanya utunzi wake kushughulikia uhalisia ulioko katika jamii kwani fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo wakati wake (King’ei, 2000) Uvuvi pia upo katika shairi la ‘*Kuvua Numbi si kazi*.’ Katika ukurasa 274. Katika huu utungo Muyaka anawakejeli wavuvi ambao hawangewapa chochote wale wasiowezankununua Samaki ila walisaidia kuegemeza mashua zap wakati wa uvuvi. Anasema kuwa wanavua ngwe na k’ozi ila hawawapei wana wa pwani chochote wasio na uwezo wa kununua samaki. Haya ni sababu yanakiuka utamaduni wa waswahili wa kushitiraki. Hii ni hali ya wanadamu kuishi kwa pamoja na kufaidi jamii. Hivyo uhuru wa mtunzi wa kiakili ulijitokeza kwa kushughulikia hayo.

Vilevile, Muyaka ameshughulikia Ufugaji. Haya yanajitokeza katika shairi la ; *Mfuga punda*,’ katika ukurasa 206. Katika jamii ya waswahili, mbuzi, kondoo na ng’ombe ni miongoni mwa wanyama wengi waliofungwa ili watu kupata nyama na maziwa. Waswahili

ila hawakuweza kufikisha kiwango walichokihitaji kwa matumizi yao ya kila siku na walipata zaidi kutoka bara. Pia wanyama kama punda na farasi walifungwa ili watumike katika shughuli za usafiri. Kipengele hiki ambacho kilijitokeza katika mashairi ya Muyaka kilithihirisha uhuru wa mtunzi wa kiakili. Hii ni sababu alishughulikia suala la ufugaji na haya ni kinyume na yale yaliyopatikana katika kazi za kirasimi kama vile *Utenzi wa Mwanakupona.*

Muyaka pia ameandika kuhusu kilimo. Kilimo ni mojawapo wa njia zilizotumika kutega uchumi mjini Mombasa wakati wa Muyaka. Familia zote zilikuwa na mashamba katika sehemu za bara zilizozingira kisiwa cha Mombasa. Watu walilima mpunga, mihogo, mahindi, machungwa, wimbi, ndizi, nazi, maembe na mboga mbalimbali. Katika shairi la '*Panda*,' katika ukurasa 190. Kwa mfano, tunapata Muyaka anataja vyakula walivyopanda wakulima kwa mfano, mnazi, mpunga, wimbi, na zinginezo. Haya ni kama ifuatavyo katika mshororo wa tatu;

*Panda nganu na mpunga afudhali ya viliwa,*
*Panda wimbi na kimanga vipawa vya kupewa,*
*Panda*, *usitunde ch'anga, tauwa mbivu tauwa,*
*Panda ni wako uluwa, panda darajani, panda*. (Abdulaziz 1979)

Kutokana na kipengele hiki cha mifumo ya kiuchumi, masuala yaliyopatikana katika mashairi ya Muyaka ni kilimo, biashara, ufugaji na uvuvi miongoni mwa mengine. Hivyo, uhuru wa kiakili wa mtunzi ulijitokeza kwani alikiuka utunzi wa kirasimi. Utunzi huu ulihusishwa na utunzi wa masuala ya kidini. Kwa mfano *Utenzi wa Mwanakupona*. Kipindi hiki kinahusishwa na wakati ambapo misingi maalum ya kazi za kisanaa. Hivyo, tunapata Muyaka alikiuka utunzi wa kipindi hiki na kuzungumzia mifumo ya kiuchumi.

## 2.2 Itikadi Katika Utenzi Wa Mwanakupona

### 2.2.1 Utangulizi

Mwanakupona binti Mshamu Habhany alizaliwa Pate mwaka wa 1830 (Hichens, 1935). Mwaka 1836 aliolewa na Bwana Muhammadi Is-Haz bin Mbarak. *Utenzi wa Mwanakupona* unaingia katika fungu la tungo za mawaidha na utamaduni. Mwanakupona aliutunga utenzi huu kwa binti yake Hahima Binti Mattaka 1275 H (1858). Tumeelezwa hivyo na mtunzi mwenyewe katika utunzi huo ambaye anamrejelea kama kijana mchinga (ubeti, 92, 94 na 95). Azimio lake lilikuwa kuwazindua pia vijana wengine wa jamii ya Islamu.

Mwanakupona aliutunga utenzi huu akiwa mgonjwa maradhi ya tumbo la uzazi. Alihisi kuwa asingepona, hivyo akaamua kutunga utenzi ili uwe ni wosia wa binti yake ambaye angebaki bila uongozi wa mama (ubeti 2, 90 na 91). Mwanakupona alifariki miaka miwili baada ya kutunga utenzi wake, yaani mwaka 1860. *Utenzi wa Mwanakupona* ndio utenzi wa zamani ambao uliandikwa na mwanamke na ukaacha athari kubwa katika maisha ya ndoa pwani kaskazini. Vilevile, igawa kuna watunzi wengi wa kike kuanzia karna ya 17 hadi leo hawana athari kubwa kama ya Mwanakupona (Kezilahabi, 1983).

Katika sehemu hii tulichanganua na kulinganisha itikadi katika utenzi huu na kazi za Muyaka kwa kufuata mirengo yetu ya kiitikadi kama ifuatavyo;

### 2.2.2 Itikadi Ya Taasubi Ya Kiume

Kulingana na BAKITA (2015), taasubi ya kiume ni hali ya kutathmini zaidi jinsia moja haswa ya kiume kuliko ya kike. Hali hii inajitokeza kutokana na jinsi wataalamu mbalimbali wanavyofaisiri utenzi husika. Kwa mfano M. S Khatib, F. F Senkoro na Joseph Mbele kama wanavyonukuliwa katika kazi ya Njozi (1990). Wataalamu hawa wanabaini

kuwa Mwanamke katika utenzi huu anadhulumiwa na pia kunyanyaswa.

Antonio Gramsci (1985) anaeleza kuwa itikadi haitawali watu kwa nguvu peke yake, bali kwa kuwafanya wakubali mfumo uliopo kwa hiari yao kupitia hegemonia ya kiutamaduni. Haya ndio yamo katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Hejemonia ya kiume inapelekea wanawake kuhimizwa kukubali kwa hiari nafasi zao katika jamii. Imani, fikra na mawazo huzoeshwa na huzama akilini mwa watu na kufanywa kuwa ukawaida.

Kufuatia mkabala wa Gramsci (1985), Mwanakupona anatengeneza hejemonia ya mfumo dume kwa kutumia fasihi kama chombo cha kuwashawishi wanawake wakubali hali yao bila shuruti. Ukubalifu huu ni tofauti na ule ukandamizaji wa moja kwa moja. Mwanakupona kupitia utenzi wake, anahakikisha kuwa wanawake wanaona kuwa utiifu ni sehemu ya maisha yao ya kawaida. Badala ya kulazimisha moja kwa moja. Utawala wa aina hii ni wa mazawo, unaofanya watu wa tabaka la chini kukubali mfumo bila kuhoji wala kupinga. K.m, Mwanakupona anasema kuwa mwanamke anapaswa kuvumilia hata kama mume wake anamfanyia mabaya. Hii inaonyesha kuwa jamii inaweka jukumu lote la mafanikio ya ndoa kwa mwanamke, wakati mume hanahimizwi kubadilika. Kwa mtazamo wa Gramsci (1985), huu ni mfano wa itikadi inayotumia dini na maadili kama njia ya kudhibiti tabaka la wanawake bila matumizi ya nguvu za moja kwa moja.

### 2.2.2.1 Dini Inavyothihirisha Itikadi

Itikadi hii ya taasubi ya kiume ilibainika katika utenzi huu kupitia dini.

*…Mama pulika maneno*

*Kiumbe ni radhi tano*

*Ndipo apate usono*

*Wa akhera na dunia* (Mwanakupona 1858, ubeti 23

*Nda Mngu na mtumewe*

*Baba na mama wayuwe*

*Na ya tano nda mumewe*

*Mno imekaririwa...* (Mwanakupona 1858, ubeti 23)

Mwanakupona katika beti hizi anamwambia bintiye azifuate radhi tano. Hizi Radhi tano mtunzi anasema kuwa ndizo ngazi za mamlaka zinazotambuliwa kidini, kwani 'zimekaririwa' na vitabu vya dini. Radhi ya kwanza ni ya Mwenyezi Mungu, ya pili ni ya Mtume Muhammad, ya tatu ni ya baba, ya nne ni ya mama, na tano ni ya mumewe. Katika ubeti 23, mshororo wa tatu, Mwanakupona anataja kuwa bintiye amheshimu mume. Lakini hakuna mahali ambapo dini inakiri kuwa mume anapaswa kumheshimu mke pia. Mtunzi anaongozwa na itikadi ya taasubi ya kiume maana anateua haya kama mojawapo wa mawaidha ambayo alinuia kumpa bintiye. Mtunzi anakuwa ni mwangwi tu wa mafundisho hayo ya dini yaliyojaa taasubi hii ya kiume.

Baadaye anaacha kuwa mwangwi na kuongeza 'aya' zake mwenyewe anapomwambia binti yake kuwa hata ahera mwanamume ndiye atakayeulizwa kama mkewe aende peponi au motoni. Mume akisema aende pepeoni ataenda mara moja na akisema aende motoni hana budi kuenda. Haya yanapatikana katika ubeti wa 26 na 27.

*... kipenda wende peponi*

*Utakwenda dalhini*

*Kinena wende motoni*

*Huna bundi utatiwa...* (Mwanakupona 1858, ubeti 27)

Mtunzi hapa alisisitiza radhi ya mume kama njia mojawapo ya mke kuongezewa thawabu

na Mungu. Kwa mujibu wa Khatib na Senkoro katika Njozi (1990) wanawake katika jamii ya Waswahili walipuuzwa na kudhalilishwa sana katika utenzi huu. Tunapata hapa kuwa Mwanakupona anamwambia bintiye kuwa mume ndiye atakaye amua hatima ya mke wake. Lakini hatujatajiwa mahali popote mke akiamua hatima ya mume wake. Kutokana na haya ni wazi kuwa mwanamume anapewa hadhi ya juu na dini kwani anapewa mamlaka na hadhi sawa na Mungu. Hii ni kupitia kuamua hatima ya mwanamke.

Isitoshe, itikadi hii inapatikana katika ubeti wa 36. Hapa mtunzi anamshauri pia kuwa ampumbaze mumewe hadi apumbae. Pia atii amri ya mumewe. Iwapo yule mume atamtendea maovu yoyote, basi Mungu ndiye atamlipia. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa mwanamke katika jamii ya Mwanakupona hangeweza kujibizana wala kukataa amri ya mumewe. Na kwani kila wakati anamtendea wema mumewe, iwapo yule mume atamtendea maovu ya aina yoyote, haezi fanya lolote, ila kumwambia Mungu kisha Mungu atamlipia. Hapa Mwanakupona anaonekana kuwa amepumbazwa na dini kiasi cha anamuachia Mungu majukumu yote. Hadi yale anayoweza jifanyia yeye mwenyewe. Hayo yanadhihirisha imani ya kidini aliyonayo Mwanakupona. Ndio maana anamshauri bintiye kuwa yanayohusisana na mumewe Mungu atamlipia. Hivyo, mwanamke hapa anaonewa na kunyanyaswa kwa kupitia imani, fikra na mielekeo bila yeye kujua kuwa anaonewa na kufinyilia.

*...Mpumbaze apumbae*

*Amriye sikatae*

*Maovu kieta yeye*

*Mngu atakulipia...* (Mwanakupona 1858, ubeti 36)

#### 2.2.2.2 Usafi Unavyothihirisha itikadi

Itikadi ya taasubi ya kiume pia ilijitokeza kupitia mafunzo ya usafi. Kulingana na Mulokozi (1999), jambo la uzazi ni jambo jingine la mafunzo ya Kiafrika ambalo hutiliwa mkazo katika unyago. Haya yanathihirika kupitia mafunzo kuhusu usafi na kujipamba ili kumpokea mume katika hali safi itakayomvutia.

*...Mwanangu siwe mkoo*
*Tenda kama uonao*
*Kupea na kosha choo*
*Sidharau mara moya...* (Mwanakupona 1858, ubeti 37)

Mwanakupona anamshauri Binti Mattaka awe msafi na asipuuze usafi. Anaendelea katika ubeti 38 kumwambia aweze kuoga na kujisugua. Nywele zake azifunge pia. Aweze kutia firashani kwenye matandiko pia.

*... Nawe ipambe libasi*
*Ukae kama arusi*
*Maguu tia kugesi*
*Na mikononi makoa...* (Mwanakupona 1858, ubeti 39)

Katika ubeti huu anaongeza kuwa bintiye apambe libasi yake. Yaani, avae na pia kujipamba vizuri kila siku. Ili aweze kukaa kama ni siku ya arusi yake kila wakati. Katika mshororo wa tatu anamwambia atie kugesi mguuni na aeke makoa mikononi. Haya ni mapambo ambayo anamwmabia ayavae ili amvutie mume wake. Anasema katika ubeti 40 kuwa pia avae kidani na kibano katika shingo na apake marashi na daiia. Hii ni aina ya poda yenye harufu nzuri.

*... Na kidani na kifungo*

*Sitoe katika shingo*

*Muili siwate mwingo*

*Kwa marashi na daiia...* (Mwanakupona 1858, ubeti 40)

Katika ubeti wa 41 anaongeza kuwa bintiye asikose kuvaa pete vidoleni, kupaka hina kwenye kucha za mikoni na uwa na wanda machoni na nyusi za macho. Beti hizi zimetupa taswira ya mwanamke Muislamu jinsi anavyokaa. Hivyo, Mwanakupona alimshauri bintiye jinsi alivyopaswa kuvaa na kujiremba ili awe mwanamke mswahili kamili na pia aweze kumvutia mume wake. Haya yalionyesha jinsi Mwanakupona alivyoamini na kutilia mafunzo ya usafi maanani na ndiposa anapitisha hayo yote kwa bintite. Kwa kufuatia mafunzo ya Gramsci (1985), mtunzi hapa anapitisha yale mafunzo sababu aliyapata yakiendelea, akayaamini na kuona kuwa ni matukio ya kawaida ambayo kila mwanamke anapaswa kutii. Haya yanaafikina na yanayozungumziwa na Joseph Mbele (Njozi, 1990). Mbele anasema kuwa Mwanakupona anatoa ushauri wa aina hii kwa binti yake si kwa sababu ndiyo njia sahihi ya mwanamke kuishi, bali kama njia ya kuepuka matatizo na kudumisha ndoa yake katika jamii ya Waswahili iliyojaa ubabedume. Hivyo, jinsia ya kike inapewa majukumu mengi yanayotokana na utamaduni ili kudumisha ndoa. Haya yanapelekea jinsia hii ya kike kulimbikiziwa majukumu chungu kizima kwa hiari yao wenyewe sababu ni mambo yanayokubalika na ya kawaida katika jamii.

#### 2.2.2.3 Ndoa Inavyothihirisha Itikadi

Itikadi ya taasubi ya kiume ipo pale Mwanakupona anamshauri bintiye asimnyime mume wake chochote anachohitaji, na vilevile kumhudumia kitandani. Anamwambia hapa kuwa akae na mume wake kwa amani. Analotaka mume amtimizie ila hatujatajiwa popote mume pia amtimizie mke anachotaka. Vilevile, Mwanamke amechorwa kama ambaye hapaswi

kubishane na mume kamwe kwani akishindana naye ataumia. Kutokana na hayo, Mwanakupona anamfunza Binti Mattaka namna ya kudumisha amani katika ndoa.

*... Enda naye kwa imani*

*Atakalo simkhini*

*We naye sikindaneni*

*Ukindani huumia...* (Mwanakupona 1858, ubeti 29)

Anaongeza katika ubeti 47 kuwa anapoondoka nyumbani, binti arudi kwa upesi ili akae na mume wake. Amtengenezee matandiko mumewe ili wapate mahali pa kulalia. Vilevile, anaongeza kuwa wakilala asijitenge na mumewe. Bali, amkaribie. Pia, ampapase na kumpepea usiku na anapoanza kusinzia asimuondoe.

*.... Kilala sikukuse,*

*Mwegeme umpapase,*

*Na upepo asikose,*

*Mtu wa kumpepea....* (Mwanakupona 1858, ubeti 31)

Mafunzo ya aina hii yanaelekezwa kwenye jambo la uzazi, ambalo katika mila za Waafrika wengi, huwa mafunzo ya unyago na jado (Mulokozi, 1999). Kutokana na hayo, tunapata kuwa Mwanakupona alitaka kumfunza bintiye yake mafunzo haya ili aweze kutunza suala la uzazi na pia kudumisha ndoa yake. Kulingana na Senkoro akinukuliwa na Njozi (1990), mwanamke katika jamii hii ya Waswahili anaonekana kama chombo cha mwanamume cha kujifurahisha. Senkoro na Njozi wanaongeza kuwa kwa kumfananisha mwanaume na mtoto mdogo ambaye alipaswa kupapaswa na kutunzwa kama mtoto, haya yanamchora mwanamma kama kiumbe dhaifu. Kutokana na hayo ilibainika kuwa jamii hii iliongozwa na tamaduni ambazo kila mwanamke anapaswa kuzifuata bila kupinga. Hivyo,

Mwanakupona alionekana aliadhirika kwa kiasi kikubwa na itikadi hii ya taasubi ya kiume kwani anafunza bintiye majukumu na mafunzo duni yaliyomnyanyasa yeye kama mwanamke, ilhali yeye mwenyewe haoni kuwa zinamkandamiza.

Jambo jingine la mila na desturi zinazolandana na mila za Kiafrika ni namna ya kuishi bila ugomvi ndani ya nyumba. Kulingana na Njozi (1990), Mulokozi (1999), utenzi huu unamfunza mwanamke mbinu za kujinusuru katika ndoa na kuepuka ugomvi ndani ya ndoa. Kupitia haya mwanamke pekee anapewa jukumu la kusimamisha ndoa yake. Ila mwanamume hajapewa jukumu lolote. Mwanakupona anamwambia bintiye amtii mume wake.

*...Keti naye kwa adabu,*
*Usimtie ghadhabu,*
*Akinena simjibu,*
*Itahidi kunyamaa... (*Mwanakupona 1858, ubeti 28)

Anaongeza katika ubeti wa 29 kuwa bintiye akae na mume wake kwa imani. Binti ampe mume analotaka. Anaendelea kumshauri binti asibishane naye pia kwani binti ataumia yeye mwenyewe. Aliarifiwa kutojibizana au kushindana na mume. Ni sawa na kusema kuwa maisha ya ndoa katika jamii ya Mwanakupona hayataki ushindani baina wanandoa husika, ili kuthibitisha taadhima yake kwa fahari kubwa kama ilivyodaiwa na Gibbe (1993).

Vilevile, akitoka mume wake, aagane naye vizuri. Akiingia pia ampokee kwa furaha (ubeti 30). Kulingana na Njozi (1990), wataalamu kama Senkoro, Khatib na Joseph Mbele wanasema kuwa hizi ni mbinu za kumdhalilisha mwanamke. Hivyo mwanamke ananyanyaswa bila yeye kujua kuwa ananyanyaswa kwa kupewa majukumu mengi, mume kuwa kama mlinzi wa mwanamke pale anaposhauriwa kuomba mumewe ruhusa anapotoka

na pia asishindane na mume. Hizi ni imani zilizochorwa kama za kawaida ambazo ni za kibebedume ambazo zilimuongoza Mwanakupona katika utunzi wake kumpa bintiye mawaidha yaliyomdhalilisha kama mwanamke.

Mtunzi katika utenzi huu aliendeleza imani za kikawaida ambazo ziliendelea kumnyanyasa mwanamke na kumchora mwanamke kama kiumbe kilicho chini ya ulinzi wa mwanamume. Hii iliendeleza ubaguzi wa kijinsia kwa kuhalalaisha utawala wa wanaume katika ndoa na jamii. Haya yameendelezwa na mtunzi kwa hiari yake mwenyewe kwani ameyachukulia kama matukio ya kawaida na anayapitisha kwa bintiye ili ayatii kama ilivyojadiliwa na Gramsci (1985)

### 2.2.3 Itikadi Ya Utiifu.

#### 2.2.3.1 Dini Kama Njia Ya Udhibiti Wa Itikadi

Gramsci (1985) anasema kuwa itikadi, utamaduni na dini hutumika kudhibiti fikra za watu. Si kwa nguvu za kijeshi au mahakama, bali kwa ushawishi wa kiakili na kimaadili. Gramsci anataja dini kama kigeu kinachoendeleza itikadi na haya tunayapata katika huu utenzi. Dini kwa mujibu wa Gramsci hutumika kudumisha utawala wa tabaka tawala. Kufuatia haya dini huhalalisha mamlaka na kufunza uvumilivu, kwa matumaini ya thawabu za mbinguni. Kulingana na Finnegan (1970) tenzi nyingi huwa na maudhui ya ushujaa, dini, vita na matukio yoyote ya kihistoria. Katika kipindi hiki cha kirasimi, kanuni za utunzi wa sanaa, haswa mashairi na tenzi, ziliorodheshwa. Kwa mfano, tenzi nyingi zinahusiana na maudhui ya kidini na kihistoria. Masinde (2003) anaafikiana na haya kwa kusema kuwa tenzi nyingi waandishi walianza kwa kutaja majina yao na ukoo wao au mahali walipozaliwa. Katika mwili watunzi walieleza ujumbe wao ambao maudhui makuu yalikuwa dini au matukio ya kihistoria. Mwishowe, tenzi humalizika kwa kumshukuru Mungu na kuomba msamaha

kama mtunzi alifanya makosa katika utenzi au utunzi huo.

Suala la dini ndilo kuu linalojitokeza katika kazi nyingi za urasimi. Kulingana na Wafula na Njogu (2007), wanatoa mfano wa utenzi wa Al-Inkishafi ambao uliandikwa na S. Abdalla Ali bin Nasir. Wanasema ni utungo wa kidini ambao mwandishi anauonya moyo wake usifuate raha za kilimwengu bali aandamane na mambo yanayohusu Mungu. Vilevile, wanasema kuwa *Utenzi wa Mwanakupona*, ni utungo unaosheheni masuala ya kidini pia, pamoja na jinsi ya kutangamana na watu, na jinsi ya kutunza ndoa. Hivyo, Mwanakupona aliongozwa na itikadi ya utiifu kwa kufuata sharia zinazolenga utathmini wa mashairi na sheria hizi zilitumika kuwekea kipimo tungo za Kiswahili.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1985) kufika kwa waarabu na uislamu maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki, kulikuwa na athari sana kwa jamii ya Waswahili. Hivyo, itikadi za jamii hizi ziliathiriwa pakubwa na dini ya Kiislamu. Ndio maana Mwanakupona anasisitiza haja ya kuzingatia mafunzo ya dini ya Kiislamu; kumtii Mungu na mtume wake; kupenda kutenda haki kama ilivyo kidini; kumtii mumuwe na kuishi kama dini inavyoagiza. Mwanakupona anadhihirisha haya kwa kushughulikia yaliyokuwa yakitawala uwanja wa fasihi katika jamii ya Waswahili wakati ule.

Tulipata itikadi hii katika ubeti wa 4. Hapa, Mwanakupona anamwambia bintiye akishaakuja karibu, kwa jina la Mungu yeye anaandika. Anamshauri amsalie Mungu, mtumewe na wafuasi wake pamoja.

> *...Ukisa kutaqarabu,*
>
> *Bismillahi kutubu,*
>
> *Umsalie Habibu,*
>
> *Na sahabaze pamoya...* (Mwanakupona 1858, ubeti 4)

Anaongeza katika ubeti wa tano kuwa aklitangaza jina la Mwenyezi Mungu, anastahili kuomba kwa wingi ili Mola awajalie. Katika ubeti huu Mwanakupona aliamini dini na ndio maana anatanguliza utenzi wake kwa kumwambia bintiye amuamini Mungu pamoja na mitume wake. Pia, aliamini kuwa waumini wanapoomba Mola, yeye huweza kuwajalia.

Mtunzi anaendelea kumshauri bintiye ashike dini. Anamwambia asikatae kutimiza wajibu huo wa kufuata dini. Mwanakupona anahimiza utii kwa mume, kwa wazazi na kwa Mungu kwa kutumia mtindo wa mawaidha unaoendeleza itikadi ya dini. Kwa mujibu wa Gramsci (1985), dini ni kigeu cha kiitikadi ambacho hutumika kuendeleza itikadi ya tabaka tawala. Hivyo, Mwanakupona anatenda kazi kama mdomo wa mfumo wa kidini ambao unasisitiza utii wa mwanamke kwa mume kama njia ya kudhibiti jamii. Vilevile, anaongeza kuwa tendo la hiari kidini ikiwezekana ni wajibu wake kufuata. Katika Kurani takatifu na Sunnah ndivyo vitu vya msingi katika maisha ya Mwislamu. (Karisa na Mwinyifaki, 2022).

Athari ya mafundisho kutoka Kurani na Sunnah yanajitokeza sana katika utenzi huu hasa pale tunampata akisema katika ubeti wa 12 kuwa ;

*...La kwanda kamata dini*
*Faradhi usiikhini*
*Na sunna ikimkini*
*Ni wajibu kuita...* (Mwanakupona 1858, ubeti 12)

Katika Kurani tukufu Luqman alimpa mwanamwe nasaha juu ya jinsi alivyotakiwa kuwaheshimu wazazi, kuishi na wengine na kuomba Mwenyezi Mungu kama inavyooneshwa katika Surat Luqman aya 13-19. Binti Mshamu, ambaye anatarajiwa kuolewa, anahitaji mno wosia wa jinsi ya kuishi na mumewe kwa msingi wa dini ya Kiislamu. Kwa mujibu wa mafundisho ya Luqman, mtunzi alijiona ana wajibu wa

kumuusia bintiye na akachagua kutumia utunzi wa utenzi.

Vilevile, itikadi ya utiifu kufuatia kipengele hiki cha dini ipo katika ubeti wa 22, na 23. Hapa Mwanakupona anamwambia azifuate Radhi tano. Hizo radhi tano ndizo ngazi za mamlaka zinazotambuliwa kidini, kwani 'zimekaririwa' na vitabu vya dini. Mwanakupona hapa anasisitiza kuwa mke anapaswa kumtii mumewe kwani kulingana na jamii yake tendo hilo lilikuwa njia mojawapo ya kumtii Mwenyezi Mungu na mtume wake Muhammad. Haya ni sababu Mwenyezi Mungu ndiye ambaye amemfadhilisha mume zaidi ya mke.

*…Mama pulika maneno*

*Kiume ni radhi tano*

*Ndipo apate usono*

*Wa akhera na dunia...* (Mwanakupona 1858, ubeti 12)

Mwanakupona hapa anasisitiza radhi ya mume, akijua kwamba ni njia mojawapo ya mke kuongezewa thawabu na Mwenyezi Mungu. Hivyo, Mwanakupona aliongozwa na itikadi hii ya utiifu kwa kuzungumzia dini kwa undani haswa pale aliposhughulikia radhi tano na hata uamuzi wa mume wa kama mke aende peponi ama motoni. Anatumia funzo hili la dini kumthabiti mwanamke ili aendelee kumtii mume. Hapa kwa mujibu wa Gramsci (1985) dini ilitumika kama kifaa cha kiitikadi kinachoweza mfumo iliopo katika jamii.

Hivyo ni wazi kuwa itikadi hii ilimtawala mtunzi kwa hiari yake mwenyewe kama ilivyojadiliwa na Gramsci (1985). Tunapata kuwa Mwanakupona anaendeleza imani kuwa bintiye atii amri ya mumewe. Iwapo yule mume atamtendea maovu yoyote, basi Mungu ndiye atamlipia. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa mwanamke katika ile jamii hangeweza kujibizana wala kukataa amri ya mumewe katika ubeti 34. Na kwani kila wakati anamtendea wema mumewe, iwapo yule mume atamtendea maovu ya aina yoyote, haezi

fanya lolote, ila kumwambia Mungu kisha Mungu atamlipia.

.... *Mnyoe mpatilize*

*Sharafa umtengeze*

*Na udi umfukize*

*Bukuata wa ashia*... (Mwanakupona 1858, ubeti 34)

Katika ubeti 36 Mwanakupona anaonekana kuwa amepumbazwa na dini kiasi cha anamuachia Mungu majukumu yote. Hadi yale anayoweza jifanyia yeye mwenyewe. Hayo yanadhihirisha imani, fikra na mtazamo huu wa kidini alionao Mwanakupona. Na itikadi hii, ameipokea kwa hiari yake mwenyewe bila kulazimishwa na yeyote. Hivyo, itikadi hii ilimuongoza mtunzi kwa ukubalifu na ukawaida na anaitumia dini kuendeleza ule mfumo wa utii.

...*Mpumbaze apumbae*

*Amriye sikatae*

*Maovu kieta yeye*

*Mngu atakupia*... (Mwanakupona 1858, ubeti 36)

Kulingana na Karisa na Mwinyifaki (2017), mawaidha ya Mwanakupona kwa bintiye kuhusu maisha ya ndoa wanasema kuwa yanatokana na mafundisho ya Kurani Tukufu na Sunnah. Mafunzo ya mtunzi yanatoka kwa Kurani Tukufu na Sunnah ambavyo ni vitabu takatifu vya Waislamu. Wanaendeleza kuwa katika Kurani Tukufu bibi zake Mtume Muhammad wanachukuliwa kama mfano wa kuigwa na wanawake hasa kuhusu jinsi wanavyotakikana kuwa watiifu kwa waume zao. Katika Surat Al Ahzab aya 30-31, wananukuu maandishi ya Kurani:

"*Enyi wake wa mtume, yeyote atakayefanya kosa la aibu, adhabu yake itakuwa mara mbili*,

*na hili ni jambo rahisi kwa Mwenyezi Mungu, lakini (mke) atakayekuwa mtiifu kwa Mungu na Mtume, zawadi yake itakuwa mara mbili*."

Isitoshe, Karisa na Mwinyifaki (2017) wanaendelea kusema kuwa Kurani inatoa mifano ya wanawake ambao hakuwa watiifu kwa waume wao na adhabu waliyopata. Wanasema kuwa Surat Al-Tahrim aya ya 10 Kurani inasema: "*Mwenyezi Mungu anatoa mfano wa bibi wa Nuhu na bibi wa Luti kwa wale wasioamini. Wanasema kuwa wanawake hawa waliolewa na watu wawili wacha Mungu, lakini hawakuwa watiifu kwa wanaume wao na wakaambiwa 'Nendeni jehanam*"

Katika Kurani Tukufu na Sunnah vilevile wanaonyesha jinsi Mwenyezi Mungu anatoa mifano ya wanawake waliowatii waume wao. Katika Surat Al-Tahrim aya ya 11 wanasema kuwa Kurani Tukufu inasema kuwa bibi wa Pharao alifanya mema na akaenda peponi. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa Mwanakupona aliongozwa na maandishi ya kidini kutoka katika vitabu vitukufu katika utunzi wake. Mtunzi hivyo aliongozwa na itikadi ya utiifu kwani alifuata mafunzo ya kidini na aliyatumia yale mafunzo kuendeleza mfumo wa utii wa wanaume katika ndoa.

Vilevile, itikadi hii ya utiifu imo katika ubeti wa 66, 67 na 68. Kutokana na beti hizo, Mwanakupona anasema kuwa amefikisha maneno yake tamati. Anamwambia bintiye kwa pamoja wamuombe Mungu ili aweze kupokea dua la mamake (Mwanakupona), anaongeza kuwa yote ambayo amenena, mwanadamu ni kiumbe dhaifu. Mola ndiye pekee awezaye kutenda makuu. Vilevile, anamwambia bintiye amfuate Mungu katika ubeti wa 68. Ili ampe msaada wa aina yoyote. Hivyo, Mwanakupona anampa bintiye wosia huu kutokana na ukawaida ulioko katika jamii. Yaani, yale mambo ambayo aliyazoea katika jamii kuwa ya kawaida. Hivyo, tunapata alitawaliwa na itikadi ya utiifu kwani kazi nyingi za urasimi

zilisheheni masuala ya dini.

Katika ubeti wa 69 Mwanakuponaanaomba Mungu Mola aweze kuhifadhi aliyonena yote na yaliyosalia. Mwisho anaomba Mungu awe naye. Katika yale maombi, anaongeza kuwa Mungu aweke wana wake, na Ndugu yake mdogo (mnuna). Yakue yao majina. Ikiwa na maana ya kuwa waweze kuishi kwa miaka mirefu na familia yao kuwa pana. Anaongeza katika ubeti wa 71 kuwa Mungu awaweke wana wa ndugu zake. Katika ubeti wa 72 pia anaiombea jamii ya Islamu. Anasema Mola awarehemu waislamu wote. Pia awape matakwa yao ili nyoyo zao ziweze kufurahia.

Katika ubeti wa 73 Mwanakupona anaendelea kuwaombea wana wake. Anasema wawe na amani, Mungu awatunze na asiwacha kuwaangalia. Katika ubeti wa 74 anaongeza kuwa Mungu aweze kuwatenda mema na awatunze na kuwahifadhi. Katika ubeti wa 75 anaongeza kuwa Mungu awaangalie watoto wake kwa huruma. Pia awaongoze ili waweze kutenda mema. Vilevile, Mungu awaepushie tamaa na akhera na dunia. Mwisho Mwanakupona anajiombea yeye mwenyewe katika ubeti wa 76 hadi ubeti wa 89. Katika ubeti 76, Mwanakupona anasema kuwa hakomi kumuomba Mungu wala hatafumba ulimi. Yaani, hatanyamaza. Anasema katika mshororo wa tatu kuwa mwenye kufaraji na kuhami, ikiwa na maana ya Mungu, amkomeshee ushia. Anaongeza katika ubeti wa 77 kuwa anamtaraji Mungu amfariji haraka kutokana na ule ugonjwa aliokuwa akiugua. Anasema apewe faraji ya wokovu na afya njema. Hapa Mwanakupona anamuomba Mungu amuondolee ugonjwa mbovu. Pia, anaongeza Mungu amsamehe dhambi zake zote na maovu. Katika ubeti wa 79 tunapata akisema kuwa kwetu wanadamu ni mazito ila kwake ni mepesi. Kumeweza kutokea mchemko wa moto na anaomba uweze kuepuka mara moja. Katika ubeti wa 80 mtunzi anaongeza kuwa anaomba kwake Latifa. Ikiwa na maana ya

Mungu mpaji.  Anasema Mungu amuondolee Makhafa, yaani hofu, kwa sherehe ya Arafa na udi wa udhia. Haya yanaamisha na siku ya sadaka. Hizi ni sherehe zilizofanyika Maka wakati wa Hija. Anaongeza katika ubeti wa 81 kuwa Mungu amuokolee. Anasema kuwa, 'Naifu Rabbi naifu.' Katika ubeti wa 82 vilevile anaendelea kuorodhesha majina yaliyotumika kumrejelea Mungu. Anasema; "Ya Ailahu ya Ailahu, Ya Rabbahu ya Rabbahu, Ya GJayata Raghbatahu, Niyika hukwamkuwa." Hapa anamaana ya 'Ewe Bwana, Ewe Bwana, aombwaye na kutimiza.' Katika ubeti wa 83 anaendelea kumuomba Rabbana, ikiwa na maana ya mungu, kwa majina yake mazuri, kusikia maombi yake.

Katika ubeti wa 84 anaongeza kuwa jamii ya Islamu inapoomba, Mungu aweze kuwasikiliza. Anasema kuwa wakinena Mungu ayafahamu na wakiomba Mungu ayajibu. Kutokana na hayo, yanayodhihirika ni sifa za Mungu na majina yaliyotumika na Wasilamu kumrejelea Mungu. Haya ni majina kama Rabbahu, Ailahu, Mola, Rabbana na Rabbi. Vilevile, anataja sifa za Mungu kama Mungu mpaji, aombaye na kutimiza, kuwapa watu matakwa yao, kuwaanagalia watu wake na kuwapa watu afya njema, miongoni mwa mengine.

Katika ubeti wa 85, mtunzi anaendeleza maombi yake kwa Mungu. Anasema kuwa yeye ni mtumwa wake mdhaifu, mwenye matatizo au taabu nyingi. Anaomba Mungu ampunguzie shida na aweze kupona. Anaendeleza katika ubeti wa 86 kuwa anaomba Mungu haraka mambo asiyoweza kuyafikiria au kuyahesabu, Mungu amletee kila la kheri. Haya ni kuwa Mungu amuepulie shida au matatizo.

Vilevile, katika ubeti wa 87, anasema Mungu amtimizie mambo asiyoweza na anayonena moyoni aweze kuyasikia na ayatimize. Pia, Mungu amfurahie, mambo mema ampe, amuondolee maovu na asikumbwe na maovu kamwe (ubeti wa 88). Katika ubeti wa 89

anasema Mungu amweke duniani kwa muda mrefu na afapo aende peponi. Anaomba ahifadhiwe katika makao yaliyo mema.

Kutokana na haya, ni wazi kuwa itikadi ya utiifu ilimtawala Mwanakupona kupitia imani na fikra zilizojitokeza katika maombi yake. Katika beti zilizo hapo juu, Mwanakupona anaiombea jamaa yake, waislamu na hata yeye mwenyewe. Maombi hayo yanajitokeza katika sehemu kubwa ya utenzi wake (ubeti wa 66 hadi 89). Hivyo, kupitia chombo hiki cha kiitikadi kama ilivyojadiliwa na Gramsci (1985), ni wazi kuwa mtunzi alitawaliwa na itikadi ya utiifu.

Mwisho, kipengele cha dini kinajitokeza katika ubeti wa 101 na 102. Katika beti hizo, Mwanakupona amehitimisha utenzi wake kwa kutaja jina la Mungu. Anaomba baraka zake. Katika ubeti 101 anamuomba Mungu arahisishe mambo ili wapate baraka za nabii na wafuasi wa mtume Muhamadi. Anataja katika mshororo wanne kuwa hiyo ndiyo dini ambayo Mungu aliwateulia kama Waislamu. Katika ubeti 102 anaongeza kuwa anamtukuza Mungu.

Kipindi 1810 hadi 1960 ambacho Mwanakupona aliutunga utenzi wake, mtunzi husika alilazimika kuzungumzia na kufuata mafundisho ya dini ya kiislamu kwa kuzingatia masuala ya maisha ya wakati wake (Mulokozi, 1999). Hivyo, utenzi huu kando ya mashairi ya Muyaka, unatokana na utamaduni wa zama hizo na utungo wenyewe unawakilisha mawaidha yaliyosheheni masuala ya ndoa na dini. Kutokana na hayo, kipengele cha dini kilidhihirika kwa uwazi kuwa ndicho kimesheni sehemu kubwa ya utenzi wa Mwanakupona kama kigeu muhimu ambacho mtunzi ametumia kupitisha mafunzo muhimi katika jamii.  Hivyo, itikadi ya utiifu ilijitokeza hapa kufuata mpangilio wa kazi yake. Tunapata kuwa utenzi wake unasehemu ya hatima ambayo mtunzi anataja jina la Mungu

na kuomba Mungu arahisishe mambo ili wapate baraka. Isitoshe, alimtukuza Mungu. Vilevile, utiifu ulijitokeza kwa kushughulikia hejemonia ya dini kwa uwazi kama ilivyozungumziwa na Gramsci (1985). Pia mtunzi ameshughulikia masimulizi marefu yenye mgao wa mwanzo, katikati na hatima ambapo Mwanakupona alimshukuru Mungu na kuomba baraka zake.

#### 2.2.3.2 Utamaduni Unavyothihirisha itikadi

Kila jamii huwa na tamaduni zake. Wanajamii husika huzoea mambo fulani kwa kuamini ukweli ule na hujipata wanafuata masuala fulani kwa hiari yao wenyewe bila kujua kuwa wanakandamizwa. Utamaduni ni kipengele ambacho hupitishwa kwa watu wa kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo, ni vigumu kujitenga na ukweli na mila na desturi za jamii. Watu hukumbatia yale mazoea kwani yamechorwa kama ukawaida katika jamii na huwa vigumu kuachana na yale wanayoamini (Gramsci, 1985).

Waswahili walikuwa na mila na desturi zao za jadi kuhusu mahusiano ya watu katika ndoa na maisha kwa jumla, ambazo waliwafunza watoto wao. Mafunzo hayo kwa watoto wa kike haswa yalifanyika katika unyago, ngao na masimulizi mengine. Pia, yaliendelezwa katika matendo ya kimila ya kila siku au kwa mashairi na nyimbo zilizoimbwa katika sherehe au wakati maalum. Vilevile, tunapata Mwanakupona akiutunga utenzi huu kwa madhumuni ya kumpa bintiye mawaidha yanayohusiana na utamaduni aliozoea kama ukawaida katika jamii ya Waswahili. Kupitia utenzi huu ni wazi kuwa mtunzi aliongozwa na itikadi ya utiifu kwa kushughulikia kipengele cha utamaduni kwani kulingana na yeye, hayo yalikuwa mazoea ambayo aliyataka pia bintiye ayafahamu. Hivyo itikadi mrengo wa Gramsci ulitumika kubaini itikadi katika utenzi huu kwani kinachojitokeza kwa uwazi kupitia kipengele cha utamaduni ni itikadi ya utiifu. Mwanakupona anayazoea mambo

kuwa kawaida na kuyakubali bila kujua kuwa yanatumika na ule utamaduni kumnyanyasa yeye kama mwanamke. Haya yanakubaliwa pia na M. S Khatib katika makala ya Njozi (1990). Njozi anasema kuwa *Utenzi wa Mwawanakupona* ni shairi "sumu" ambalo linatafuta kuweka kitaifa na kurudisha watumwa wa wanawake.

Mwanakupona anampa bintiye ushauri wa jinsi ya kutangamana na watu. Haya ni mawaidha ambayo yalijikita katika jinsi Binti Mattaka atakavyofanya yeye mwenyewe ili kuwa mtu wa kupendeka na kutangamana na watu bila ugomvi. Katika ubeti wa 13 anamwambia awe na adabu. Akinena anene yanayofaa. Anaongeza kuwa bintiye awe mtu wa kupendeka. Anahitimisha katika mishororo wa nne kuwa akule anapopewa na anapokaribishwa.

*...Pili uwe na adabu*
*Na ulimi wa thawabu*
*Uwe mtu mahabubu*
*Kula utakapoingia...* (Mwanakupona 1858, ubeti 13)

Katika ubeti wa 14, pia tunapata akimshauri bintiye awe mtu wa kuaminika. Analoambiwa alikamilishe. Vilevile, ajitenge na watu waovu wasioshika haki na asiandamane na wajinga njiani.

*…La tatu uwe sadiqi*
*Wambiwalo ulithiqi*
*Mtu asoshika haqi*
*Sandamane naye ndia...* (Mwanakupona 1858)

Katika ubeti wa 15 anaongeza kuwa awe mtu wa kunyenyejea mbele ya matajiri.

*…Tena mwanangu idhili*

*Mbee za maqabaili*

*Uwaonapo mahali*

*Angusa kuwenukia...* (Mwanakupona 1858)

Kutokana na hilo, katika jamii ya Waswahili, watu katika tabaka la juu walipewa heshima. Ndiposa Mwanakupona anamwambia bintiye kuwa anapotangamana na matajiri, anapaswa kuwanyenyekea. Hivyo, kulingana na mila na desturi za Waswahili, matajiri waliheshimika.

Njozi (1990) anasema kuwa Mwanakupona anamshauri bintiye kuwaheshimu matajiri na pia kutojiunga na watumwa. Kutokana na hili Senkoro akinukuliwa na Njozi (1990) anasema kuwa ata Mwanakupona mwenyewe alikanganywa na ile migao ya kitabaka ilikuwa katika utamaduni wao. Anaongeza kuwa hii ni mielekeo potoshi ilioko katika ile jamii ili kuwakandamiza watu wa tabaka la chini. Mwanakupona katika ubeti wa 16 anaongeza kuwa bintiye awaonapo matajiri awainukie na moyo uliofurahia. Kisha awaonyeshe njia wanapokwenda.

*.... Wangiapo wenukie*

*Na moyo ufurahie*

*Kisa uwapeke mbee*

*Watakapokwenda ndia...* (Mwanakupona 1858)

Vilevile, anamshauri katika ubeti wa 17 kuwa awe mtu mwadilifu. Anamwambia ajifanye mcheshi na anene kwa maneno yasioudhi au kudanganya. Pia asifanye ubishi ili watu wasije wakamchukia.

*.... Ifanye mteshiteshi*

*Kwa maneno yasoghashi*

*Wala sifanye ubishi*

*Watu wakakutukia...* (Mwanakupona 1858)

Kando na hayo, katika ubeti 18 kuwa bintiye anene na watu kwa mzaha. Anene nao yanayowaletea furaha ili asilete chuki. Anamshauri heri kujinyamazia. Anaendelea kusema bintiye asiamini mambo asiyoona na asisengenyane.

*...Nena nao kwa mzaha*

*Yaweteao furaha*

*Iwapi ya ikraha*

*Khera kuinyamalia...* (Mwanakupona 1858)

Itikadi hii ya utiifu ilijitokeza katika ubeti wa 20.

*...Sitangamane na watumwa*

*Ilia mwida wa khuduma*

*Watakuvutia tama*

*La buda nimekwambia...* (Mwanakupona 1858)

Kipengele cha utamaduni kinaendelezwa pale Mwanakupona anamfunza bintiye mazoea yaliyoko ya migao iliyoko katika jamii. Haya ni kupitia pale anamwambia bintiye asiandamane na watumwa. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa jamii husika ilikuwa na tabaka la juu lililosheheni nyenzo za uzalishaji mali na tabaka la chini ambalo lilisheni wafanyikazi ambao ni watumwa. Hii ni imani potofu ambayo Mwanakupona aliiendeleza kwa bintiye. Hivyo, tunapata Mwanakupona akimwambia kuwa aandamane nao tu wakati wa kazi. Akiandmana nao watampotosha.

Pia, katika ubeti wa 21 anaongeza asiandamane na wajinga wasiojua kujichunga. Tunapata mtunzi akiwasawiri kama viumbe wasio haya katika mishororo wa tatu. Anahitiisha

sehemu hiyo kwa kumwambia katika ubeti wa 22 kuwa afuate hayo aliyomwambia ilia aepuke ya ahera na dunia. Hivyo, atapata utulivu. Mawaidha haya yanadhihirisha kuwa ile migao ya kijamii ilikuwemo wakati wa Mwanakupona. Ndio maana anampa wosia bintiye kuhusu haya ili aweze kuyafahamu pia yeye. Kutokana na hayo ni wazi kuwa utamaduni wa Mwanakupona ulikubali ile mitazamo na fikra kuhusiana na migao ya kijamii. Hio mitazamo ilichorwa kupitia utamaduni na tunapata itikadi ya utiifu wa mtunzi ikibainika kwa jinsi alivyofuata ule utamaduni bila kujali kama unamkandamiza bintiye au la.

Kando na hayo, itikadi hii ya utiifu pia ilijitokeza kupitia utamaduni pale Mwanakupona anamfunza bintiye masuala ya kazi. Anamwambia apende kazi. Hivyo, kazi ilikuwa muhimu katika utamaduni wa Waswahili kwani mtu hakupaswa kuzembea. Katika utenzi huu, hili halijajitokeza sana labda kwa kuwa Mwana Hashima ni mtoto wa tabaka tawala mwenye watumwa na watumishi wa kumhudumia. Hivyo halazimiki kufanyia kazi ngumu (Mulokozi, 1999). Lakini katika utenzi huu kipengele cha kazi kinajitokeza nyumbani katika asasi ya ndoa. Haya yanajitokeza katika ubeti 37. Hapa mtunzi anamshauri bintiye afanye kazi haswa katika ndoa yake. Anamwambia asiwe mvivu kwa kutenda anayoyaona. Yaani, kutenda yale aliyoona mama yake akiyatenda ili kutunza ndoa yake. Pia, kutenda ambayo anayoyaona yanafaa ili kudumisha ndoa yake. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa hata Mwanakupona mwenyewe alifanya kazi. Hivyo, utamaduni wa Waswahili haukumruhusu mtu kuwa mvivu (Mulokozi,1999). Ndiposa anamshauri bintiye kufanya kazi bila kudhania kuwa sio jukumu lake kwani kulingana na Njozi (1990) Mwanakupona alikuwa ameolewa na mfalme. Hivyo, haya yanaonyesha kuwa anayomshauri bintiye ni maadili ambayo anayopaswa kuzingatia.

Itikadi ya utiifu kupitia kipengele cha utamaduni pia ilipatikana kupitia mafunzo ya usafi.

Kulingana na Mulokozi (1999), jambo la uzazi ni muhimu katika mafunzo ya Kiafrika ambalo hutiliwa mkazo unyagoni. Maadili ya dini ya Kiislamu tunapata hayaelezwi wazi katika utenzi huu, lakini tunapata Mwanakupona akiyashughulikia. Haya yanathihirika kupitia mafunzo kuhusu usafi na kujipamba ili kumpokea mume katika hali safi itakayomvutia. Katika ubeti 37, Mwanakupona anamshauri Binti Mattaka awe msafi na asipuuze usafi. Anaendelea katika ubeti 38 kumwambia aweze kuoga na kujisugua. Nywele zake azifunge pia. Aweze kutia firashani kwenye matandiko pia.

...*na Kowa na kuisinga*

*Na nyee zako kufunga*

*Na smini kutunga*

*Na farashani kutia*... (Mwanakupona 1858)

Vilevile, katika ubeti 39, anaongeza kuwa bintiye apambe libasi yake. Yaani, avae na pia kujipamba vizuri kila siku. Ili aweze kukaa kama ni siku ya arusi yake kila wakati. Katika mshororo wa tatu anamwambia atie kugesi mguuni na aeke makoa mikononi. Haya ni mapambo ambayo anamwmabia ayavae ili amvutie mume wake.

...*Nawe ipambe libasi*

*Ukae kama arusi*

*Maguu tia kugesi*

*Na mikononi makoa*... (Mwanakupona 1858)

Anasema katika ubeti 40 kuwa pia avae kidani na kibano katika shingo na apake marashi na daiia. Hii ni aina ya poda yenye harufu nzuri. Katika ubeti wa 41 anaongeza kuwa bintiye asikose kuvaa pete vidoleni, kupaka hina kwenye kucha za mikoni na uwa na wanda machoni na nyusi za macho.  Haya yote, yametupa taswira ya mwanamke Muislamu jinsi

alivyo tarajiwa kuwa. Hivyo, Mwanakupona anamshauri bintiye jinsi anavyopaswa kuvaa na kujiremba ili awe mwanamke Mswahili kamili na pia aweze kumvutia mume wake kama inavyoelekezwa na utamaduni.

Mwanakupona anaendelea kumshauri bintiye asimnyime mume wake anachohitaji na kumpa huduma za kitandani katika ubeti wa 29.

.... *Enda naye kwa imani*

*Atakalo simkhini*

*We naye sikindaneni*

*Ukindani huumia...* (Mwanakupona 1858)

Anamwambia akae na mume wake kwa amani. Analotaka mume amtimizie. Asibishane naye kamwe kwani akishindana naye ataumia. Kutokana na hayo, mwanakupona anamfunza Binti Mattaka namna ya kudumisha amani katika ndoa. Anaongeza katika ubeti 47 kuwa anapoondoka nyumbani, binti arudi kwa upesi ili akae na mume wake. Amtengenezee matandiko mumewe ili wapate mahali pa kulalia. Vilevile, anaongeza kuwa wakilala asijitenge na mumewe. Bali, amkaribie. Pia, ampapase na kumpepea usiku na anapoanza kusinzia asimuondoe. Haya yanapatikana katika ubeti 31.

...*Kilala siikukuse*

*Mwegeme umpapase*

*Na upepo asikose*

*Mtu wa kumpepea...* (Mwanakupona 1858)

Mtunzi hapa alithihirisha utiifu kwa kumshauri bintiye jinsi ya kunusuru ndoa yake kama inavyosisitizwa na utamaduni na pia dini.

Anaongeza katika ubeti wa 29 kuwa bintiye akae na mume wake kwa imani. Analotaka

mumewe Binti Mattaka asimkataze. Asibishane naye pia kwani akishindana na mume wake ataumia yeye mwenyewe. Binti hapa anaarifiwa kutojibizana au kushindana na mume. Vilevile, akitoka mume wake, aagane naye vizuri. Akiingia pia ampokee kwa furaha (ubeti 30).

Jambo jingine ni jinsi ya kudumisha amani na wanajamii. Jambo hili lilijitokeza pale ambapo Mwanakupona anampa mawaidha kuhusu jinsi ya kutangamana na wanajamii ili kuepuka mikwaruzano na ugomvi. Haya yanajitokeza katika ubeti 57 hadi 64. Katika ubeti 57 mtunzi anasema;

*...Mausio ya mvuli,*

*Allah Allah Yaamili,*

*Na nduguzo na ahali,*

*Wapende na kuusia....* (Mwanakupona 1858)

Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa anamshauri bintiye ashirikiane na wanaohusiana naye kinasaba. Tunapata katika ubeti 58 akiongeza akuwa Binti Mattaka awaonapo marafiki, wanaohusiana nao kinasaba aharakishe kuwakaribisha.

Ilibainika kuwa mtunzi aliadhiriwa sana na utamaduni kwani masuala mengi aliyoyashughulikia aliyatoa katika dini na utamaduni wa Waswahili. Kwa mfano, jinsi ya kuishi na wanajamii kwa amani, jinsi ya kusimamisha ndoa yake na kumheshimu mume miongoni mwa mengine. Hivyo, Mwanakupona aliongozwa na itikadi ya utiifu kwa kutoa wosia kwa hejemonia ya utamaduni ambayo inasawiri matukio kama yaliyokubaliwa na yanapaswa kufuatwa bila pingamizi yoyote. Hivyo wanawake katikaa jamii ya mtunzi wanatarajiwa kufuata yale mafunzo ili kujinusuru na kusimamisha ndoa na kuendeleza uhusiano bora.

#### 2.2.3.3 Fasihi inavyothihirisha itikadi

Katika *Utenzi wa Mwanakupona,* fasihi imetumika kama chombo kisichotumia nguvu kulingana na mtazamo wa Gramsci (1985) ili kuhakikisha kuwa wanawake wanakubali mfumo wa kijamii. Mfano*:*

> ... *Mnyoe mpatilize*
>
> *Sharafa umtengeneze*
>
> *Na udi umfukize*
>
> *Bukuata wa ashia*.... (Mwanakupona 1858, ubeti 34)

Mwanakupona katika ubeti huu anamshauri bintiye anyoe nywele za mume wake. Amtengeneze sharafa na kumfukiza udi asubuhi na jioni. Huu ni mfano wa itikadi inayotumiwa katika familia na fasihi ili kuwafanya wanawake waone kuwa wao ndio wanapaswa kubeba mzigo wa ndoa. Anapatiwa jukumu la kumnyoa mume nywele lakini mume haambiwi anyoe nywele zake na ni mtu mzima. Fasihi hii yote ya Mwanakupona inasababisha wanawake kujidhibiti wenyewe kwa hiari, wakikubali nafasi yao katika jamii bila kulazimishwa moja kwa moja.

Utenzi huu umesheheni ushauri wa mama kwa binti yake kuhusu ndoa. Mwanakupona binti Msham anaeleza jinsi mwanamke anavyopaswa kuwa mnyenyekevu, mtiifu, na mwenye heshima kwa mume wake. Mtunzi alisisitiza maadili mema, uvumilivu, na utii kama nguzo kuu za ndoa yenye mafanikio. Kupitia utenzi huu, Mwanakupona anatumia maneno ya upole na ushauri katika utenzi wake badala ya amri au shinikizo. Hivyo, kuifanya itikadi iwe ya kudumu zaidi kwa sababu ilikubaliwa bila upinzani kupitia fasihi yake.

### 2.2.4 Itikadi Ya Ukawaida

#### 2.2.4.1 Utamaduni

Kwa mujibu wa Gramsci (1985), hejemonia ya utamaduni inatumika kuendeleza ukawaida potofu. Kwa mafano, Mwanakupona anamfunza bintiye mazoea yaliyoko ya migao iliyoko katika jamii. Haya ni kupitia pale anamwambia bintiye asiandamane na watumwa. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa jamii husika ilikuwa na tabaka la juu lililosheheni nyenzo za uzalishaji mali na tabaka la chini ambalo lilisheni wafanyikazi ambao katika huu utenzi ni watumwa. Hii ni imani potofu ambayo Mwanakupona anaiendeleza kwa bintiye. Hivyo, tunapata Mwanakupona akimwambia kuwa aandamane nao tu wakati wa kazi. Akiandmana nao watampotosha. Pia, katika ubeti wa 21 anaongeza asiandamane na wajinga wasiojua kujichunga. Kutokana na hayo ni wazi kuwa utamaduni wa Mwanakupona unakubali ile mitazamo na fikra kuhusiana na migao ya kijamii. Hio mitazamo inachorwa kupitia utamaduni na tunapata itikadi ya ukawaida ya mtunzi imebainika kwa jinsi alivyofuata ule utamaduni bila kujali kama unamkandamiza bintiye au la.

*...Sandamane na watumwa*
*Ilia mwida wa khuduma*
*Watakuvutia tama*
*La buda nimekwambia...* (Mwanakupona 1858)

Hejemonia ya utamaduni pia ilijitokeza kupitia mafunzo ya usafi. Katika ubeti 37, Mwanakupona anamshauri Binti Mattaka awe msafi na asipuuze usafi. Anaendelea katika ubeti 38 kumwambia aweze kuoga na kujisugua. Nywele zake azifunge pia. Aweze kutia firashani kwenye matandiko pia. Katika ubeti 39, anaongeza kuwa bintiye avae na pia

kujipamba vizuri kila siku. Ili aweze kukaa kama ni siku ya arusi yake kila wakati. Katika mshororo wa tatu anamwambia atie kugesi mguuni na aeke makoa mikononi. Haya ni mapambo ambayo anamwambia ayavae ili amvutie mume wake. Anasema katika ubeti 40 kuwa pia avae kidani na kibano katika shingo na apake marashi na daiia. Hii ni aina ya poda yenye harufu nzuri. Katika ubeti wa 41 anaongeza kuwa bintiye asikose kuvaa pete vidoleni, kupaka hina kwenye kucha za mikoni na uwa na wanda machoni na nyusi za macho. Haya yote, yanatupa taswira ya mwanamke Muislamu jinsi anavyokaa. Hivyo, Mwanakupona anamshauri bintiye jinsi anavyopaswa kuvaa na kujiremba ili awe mwanamke Mswahili kamili na pia aweze kumvutia mume wake.

Pia, mawazo ya Gramsci (1985) yalijitokeza pale Mwanakupona anamshauri bintiye kutomnyima mume chochote anachokitaka katika ubeti 29, na kumhudumia kitandani pia. Anamwambia katika ubeti huu kuwa akae na mume wake kwa amani. Analotaka mume amtimizie. Asibishane naye kamwe kwani akishindana naye ataumia. Kutokana na hayo, Mwanakupona anamfunza bintiye namna ya kudumisha amani katika ndoa. Anaongeza katika ubeti 47 kuwa anapoondoka nyumbani, binti arudi kwa upesi ili akae na mume wake. Amtengenezee matandiko mumewe ili wapate mahali pa kulalia. Vilevile, anaongeza kuwa wakilala asijitenge na mumewe bali, amkaribie. Pia, ampapase na kumpepea usiku na anapoanza kusinzia asiache kumpapasa, ubeti 31. Mtunzi anasema;

*...Kilala sikukuse,*
*Mwegeme umpapase,*
*Na upepo asikose,*
*Mtu wa kumpepea...* (Mwanakupona 1858)

Mafunzo ya aina hii yanaendeleza hejemonia ya utamaduni. Kutokana na hayo, tunapata

kuwa mtunzi alipitisha yale mafunzo ili bintiye aweze kutunza suala la uzazi na pia kudumisha ndoa yake.

Suala lingine linaloendeleza hejemonia ya utamaduni katika jamii husika ni namna ya kuishi bila ugomvi ndani ya nyumba. Katika ubeti wa 22 na 23 Mwanakupona anasema kuwa kumheshimu mume ni miongoni mwa radhi tano za jamii hiii. Hivyo, kumheshimu mume lilikuwa jambo muhimu katika utamaduni wa Waswahili. Mwanakupona tumepata akimwambia bintiye amtii mume wake. Anasema katika ubeti wa 28 kuwa;

*...Keti naye kwa adabu,*

*Usimtie ghadhabu,*

*Akinena simjibu,*

*Itahidi kunyamaa...* (Mwanakupona 1858)

Anaongeza katika ubeti wa 29 kuwa bintiye akae na mume wake kwa imani. Analotaka mumewe Binti Mattaka asimkataze. Asibishane naye pia kwani akishindana na mume wake ataumia yeye mwenyewe. Hapa anaarifiwa kutojibizana au kushindana na mume. Vilevile, akitoka mume wake, aagane naye vizuri. Akiingia pia ampokee kwa furaha (ubeti 30). Hizi ni mbinu za kumdhalilisha mwanamke ambazo zinachorwa kama mambo ya kawaida na ambayo yalikubalika katika jamii lakini hatupati mwanamme akitajiwa lolote la kudumisha ndoa na uhusiano bora.

Kutokana na hejemonia ya utamaduni ni dhahiri kuwa mila na desturi ziliweza kujitokeza kwa uwazi katika utenzi huu. Ilibainika kuwa mtunzi aliadhiriwa sana na mawazo ya Gramsci katika kazi yake kwani masuala mengi aliyoyashughulikia yalihusiana na hejemonia ya mfumo wa kijamii na hejemonia ya utamaduni wa Waswahili. Hivyo kupitisha zile fikra zake kwa bintiye kwani ndio ukubalifu katika jamii. Ndio maana haoni

imani zingine kama za kuikandamiza jinsia ya kike. Naye bintiye alilazimike kufuata zile imani kwani ni mazoea katika jamii yake na yalifanywa kuzama akilini mwa kila mwanamke mswahili.

### 2.2.5 Ulinganishaji

Uchanganuzi kuhusu itikadi za watunzi ni muhimu katika fasihi kwani itikadi ndizo ambazo huwaelekeza watunzi katika kazi zao (Rossiland, 1990). Sura hii ilidhihirisha kwamba itikadi tofauti ziliweza kuwaongoza Muyaka na Mwanakupona katika uchanganuzi wa yaliyo faafu katika jamii husika. Hii ni sababu ya wanavyowasilisha matukio katika jamii. Muyaka kufuatia mawazo ya Marx (1977) na Althusser (1981) imebainika kuwa aliongozwa na itikadi ya uhuru wa kiakili kwa kushughulikia masuala mbalimbali ya sokoni. Muyaka pia alithihirisha itikadi ya ukandamizaji kwa kushughulikia jinsi kikundi kimoja kulinyimwa haki na wengine kama ilivyoonyeshwa na Karl Marx kuwa kikundi kimoja huendelea kudhibiti kikundi.  Mwisho, Muyaka alithihirisha itikadi ya mapinduzi ya nguvu pale alishughulikia mivutano ya kisiasa na mivutano baina ya miji na jinsi za kujinasua kwa mikono ya mkoloni kama Karl Marx alivyosema kuwa historia yote ya jamii ni historia ya mapambano ya kitabaka. Muyaka ameonyesha kuwa siasa na mamlaka ni uwanja wa mapambano kati ya tabaka husika na tabaka la watawaliwa jinsi lilivyopambana kuondoa ile mifumo ya unyanyasaji wa wakoloni.

Katika upande mwingine tuliweza kubaini kuwa Mwanakupona aliongozwa na itikadi ya utiifu kupitia dini, utamaduni, ndoa na familia na jinsi alivyoichora fasihi yake. Mtunzi amesawiri vigeu hivi kama masuala ya kawaida kama anavyoakisi Gramsci (1985) na Althusser (1981) na hivyo kuendeleza ule utii kwa kizazi kingine.  Isitoshe, itikadi ya taasubi za kiume na ukawaida ziliweza kubainika. Kutokana na hayo, ilithihirika kuwa

Mwanakupona na Muyaka waliongozwa na itikadi tofauti. *Utenzi wa Mwanakupona* uliendeleza mfumo dume kwa kutumia fasihi na hejemonia ya utamaduni na dini kama vigeu vinavyoendeleza itikadi. Katika mtazamo wa Gramsci Mwanakupona aliunga mkono tabaka la wanaume kwa kuhakikisha wanawake wanatii. Muyaka naye anafuata mawazo ya Karl Marx na kukosoa unyonyaji wa kiuchumi, migogoro ya kitabaka na udhalimu wa watawala. Katika mtazamo wa Gramsci, Mwanakupona alitumia fasihi kueneza hejemonia ya mfumo wa ndoa na dini kuhakikisha wanawake wanatii bila shuruti. Ilhali Muyaka kwa mawazo ya Karl Marx, alipinga hejemonia ya wageni, alihimiza kujitawala na alileta mabadiliko na uhuru wa kiakili. Kutokana na hayo ni wazi kuwa Mwanakupona alisisistiza sana utii kwa kufuatia utunzi wa kirasimi kwa kuandika kuhusu dini, ndoa na utamaduni. Muyaka naye amebadilisha utunzi wake kuwa wa sokoni na kushughulikia mambo mengi ya sokoni kama vita, utawala, jinsi wapenzi walivyoendeana kinyume na hata biashara.

### 2.2.6 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kuchanganua na kulinganisha itikadi zinazojitokeza katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Imebainika kuwa Muyaka alitawaliwa na itikadi ya uhuru, mapinduzi ya nguvu na ukandamizaji kwa kuonyesha jinsi wanajamii walikandamizwa na watawala na hata jinsi wapenzi walivyoendeana kinyume katika ndoa. Mwanakupona naye ilibainika aliongozwa na itikadi ya utiifu, taasubi ya kiume na ukawaida, kwa kutumia hejemonia ya utamaduni, dini na ndoa kuendelezwa mifumo ya kiudhibiti.

Sura iliyofuata ilishughulikia jinsi itikadi za watunzi zilipelekea uwasilishaji wa maudhui katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona.*

# SURA YA TATU

# ATHARI YA ITIKADI KATIKA USAWIRI WA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA MWANAKUPONA* NA MASHAIRI YA MUYAKA

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti ulishughulikia jinsi itikadi katika jamii zilivyowaathiri katika usawiri wa maudhui yao. Maudhui katika fasihi yoyote hutokana na jinsi jamii ilivyo wakati wa utunzi maalum (King'ei, 2000). Kwa hivyo, masuala katika ulimwengu wa mtunzi huathiri pakubwa uandishi wa mtunzi. Kwa hivyo, data ya utafiti huu imeainishwa kwa mihimili mikuu wa nadharia ya itikadi ambao ni itikadi huwa ung'amuzi potoshi na kuwepo kwa migao ya kitabaka katika mashairi ya Muyaka, na itikadi huendelezwa kwa hiari katika *Utenzi wa Mwanakupona*.

## 3.1 Itikadi Zinavyoathiri Uwasilishaji wa Maudhui katika Mashairi Ya Muyaka

### 3.1.1 Maudhui Yaliyopelekewa na Itikadi Ya Ukandamizaji

#### 3.1.1.1 Maudhui ya Tamaa

Muyaka alishughulikia masuala mengi yaliyojitokeza katika jamii kama vile ndoa na familia, mifumo ya kiuchumi, vita na hata umasikini. Uhuru wake wa kuandika fasihi ya aina hii ulipelekea mada hii ya tamaa. Mada hii ya tamaa ilichangiwa pakubwa na itikadi ya ukandamizaji. Katika tungo zake, Muyaka alionyesha jinsi watu wanawakandamiza wengi na kuwaathiri kimaisha. Kwa mujibu wa BAKITA (2015), tamaa ni hamu kubwa ya kufanya jambo au hali ya kujawa na matarajio ya kupata kitu.

Maudhui haya yalijitokeza katika shairi la '*Ulimwengu usiungie*,' ukurasa 259. Muyaka anamkejeli mwanamke ambaye anatarajia Muyaka kumpa chake. Lakini kwa upande mwingine, yule mwanamke hampi Muyaka chochote. Muyaka anasema kuwa yule

mwanamke asiufanyie ulimwengu pupa. Vilevile, Mtunzi katika ubeti wa pili anaongeza kuwa angependa kumuondoa au kumuacha yule mwanamke lakini amemuandama kama kupe. Yule mwanamke hataki kujiepua wala kulegeza ile tabia ila anasema kuwa yuko papo hapo.

Kutokana na hayo, ni dhahiri kuwa mwanamke katika hili shairi anatamani mali ya mtunzi, anamganda kama kupe ila chake hampi mtunzi. Itikadi ya ukandamizaji katika ndoa ilijitokeza hapa. Hii ni sababu yule mwanamke anatamani mali ya mtunzi, anamganda kama ganda, ilhali hayo ni tofauti na inavyopaswa kuwa baina ya wapenzi.

Tamaa pia ilijitokeza katika shairi la '*Pawala Malambi*,' ukurasa 326. Mtunzi hapa anasema kuwa siku hizi watu (masikini) wanakula chakula kibaya na vinyama vichafu vilivyokonda (mbofuwafu). Hii ni tabia ya walio kwenye tabaka la chini. Wamekandamizwa kabisa bila kutamka neno lolote na walioko kwenye tabaka la juu ambalo limesheheni mabwanyenye. Masikini hapa wamefungwa midomo yao kama mitego. Muyaka anahitimisha kwa kusema kuwa kushika au kupanda ngazi ni ipi rahisi? Hapa, tamaa ya mabwanyenye inajitokeza. Matajiri wamejilimbikizia mali kiasi cha kuwa masikini wanakula chakula kibaya na nyama chafu zilizokonda. Hawasemi lolote wala hawana uwezo wa kutetea nafsi zao. Hivyo, Muyaka anauliza, 'kupanda au kushika ngazi ni ipi rahisi?' Hii ni sababu masikini huwa wamezoea hali yao na wakizinduka na kujitetea, kuna urahisi wao kupanda ngazi, lakini ni haraka tajiri kushika ngazi sababu ya tamaa nyingi ambayo hufanya mtu kukosa yote.

Maudhui ya tamaa vilevile yalipatikana katika shairi la '*Cha mtu utakulaji*,' ukurasa 328. Hapa mtunzi anauliza utawezaje kula cha mtu lakini kwa upande mwingine hamkubali yule mtu. Muyaka anamuuliza anayerejelewa mbona alimtuma mjumbe ampe ujumbe lakini

aliyepelekewa ule ujumbe hakuenda kama alivyoarifiwa. Mtunzi alitaka angalau amuulize anaendelea vipi. Lakini anastaajabika kutokana na ile tabia ya anayerejelewa. Yule mtu anapuuza mambo na ndio maana mtunzi anamuuliza mbona akubali vitu au mali ya wengine wakati hamkubali anayempa zile vitu. Hii inaonyesha hali ya juu ya ukandamizaji. Hii ni sababu anatamani mali lakini hamtaki mwenye kumpa mali.

**3.1.1.2 Maudhui ya Utabaka.**

Kulingana na Abdulaziz (1982) kipindi alichoishi Muyaka, Waarabu walikuwa na ufanisi mkubwa sana mjini Mombasa lakini ufanisi wao pamoja na utawala wa Wamazrui haukudumu kwa muda mrefu. Matajiri waliporomoka na mwishowe kuyaonja maisha ya umasikini. Lakini ingawaje kwa kawaida baada ya mporomoko wandani huwatoroka na kuwakana rafiki zao walioporomoka, Mwandishi hakufanya hivyo. Aliwafariji watu wa Mombasa na alikuwa nao hadi wakati walipoporomoka kama walivyokuwa pamoja kutoka mwanzoni walipokuwa matajiri.

Muyaka anakosoa mfumo huo wa kijamii ambapo heshima na uhusiano unategemea tabaka la juu na la chini. Marx (1977) anasema kuwa mashairi yake yanaonyesha migao ya kitabaka na unyonyaji wa kiuchumi. Hii inaonyesha kuwa fasihi ya Muyaka inatumika kueleza mapambano ya kiuchumi, matabaka na kutilia shaka mfumo wa kiuchumi wa wakati ule. Hapa mtunzi aliathiriwa pakubwa na itikadi ya ukandamizaji wa kiuchumi kwani anatuonyesha jinsi kulikuwa na migao ya kitabaka katika jamii yake na vilevile kuleta mabadiliko ili kuwafanya watu wawe sawa na wamoja. Haya yanachangia mtunzi kushughulikia umasikini ifuatavyo;

Mporomoko wa ufanisi wa Mombasa katika shairi lake la “*Ulimwengu*” (uk.153). Mwandishi alieleza namna watu katika jamii hujigawa katika matabaka tofauti lakini

anaendelea kusema ni kawaida kumuona tajiri ameshushwa hadhi hadi akawa masikini waliokuwa katika tabaka la chini. Mtunzi hapa anasema kuwa jamii huwa na mabadiliko ya kitabaka kila wakati na matajiri hushuka ngazi na masikini hupanda ngazi.

**3.1.1.3 Maudhui ya Umasikini**

Katika shairi la "*Ukiwa Wako*" (ukurasa.209), Mwandishi anatueleza kuhusu kijana mmoja alitumia fedha zake kiholela na akageuka kuwa maskini hohehahe. Mrejelewa alielekea kurudi kwa mama yake na kumtishia ampe pesa au kujidunga kwa kisu na kujitoa uhai. Ila yule mama anakataa kumpa pesa, anamkashifu kwa tendo lake na kutumia pesa vibaya na anamfukuza yule kijana.

Umasikini pia upo;

*Kwa heri mwana kwa heri, nenda zangu Ngezi-maji,*

*Nimeazimu safari kwa p'epo za maleleji,*

*Kwa malenge na shuwari natawakali Mpaji,*

*Baada ya dhiki faraja, hakuna lislilokuwa*. (Abdulaziz 1979, uk 109)

Anaongeza kuwa;

*Natamani kulivuta tao la nyanje maua;*

*Kulla ambapo napita haoneka na sitawa;*

*Si hofu tupa ukuta, tangu chambwa na kuambiwa;*

*Nna ukunyunyu wa t'awa na kujikuna nguoni*. (Abdulaziz 1979, 109)

Maoni ya jumla yanayopatikana katika aya hii ni kuwa Muyaka hakuwa na hali nzuri ya kimaisha. Yaani umaskini. Kwa mfano hapo juu tunapata mtunzi akihurumia hali yake duni. Analaumu mavazi yake machafu na pia anazungumzia jinsi watu walivyomtupia maneno ya kumkejeli kuhusu ile hali yake. Anasema kuwa anatamani kulivuta tao la nyanje

maua ili anapopita mahali, watu waone kuwa anangaa. Anaongeza kuwa hana hofu kufukuza ule umaskini kwani amekuwa katika hali ile kwa muda mrefu. Ameongewa na pia kusutwa na watu. Anamalizia kwa kusema kuwa mavazi yake yamejaa chawa na anajikuna mwilini sana.

Katika aya nyingine katika ukurasa 109, Muyaka ansema;

> *Ai nilivute tao nende mwendo wa utambo;*
>
> *Muone mipendezao, shani yangu na urembo;*
>
> *Kikuu hukua kwao, mwema hupendeza umbo,*
>
> *Shuhudiani kabombo kinawashinda wenziwe.* (Abdulaziz 1979)

Hapa, mtunzi anaamua kuvaa vizuri na kutembea kwa mwendo wa utambo ili watu waone jinsi anavyopendeza. Watu waone shani na urembo wake. Anaongeza kuwa mtu hupata wema na sifa kutoka kwa jamaa yake. Hivyo, anasema watu washuhudiwa kabombo siku hiyo kwani kunawashinda wenziwe. Ikiwa na maana kuwa yeye ni bora kuliko wenzake.

Isitoshe, katika aya nyingine, tunapata mtunzi akikashifu mavazi yake;

> *Maninga yangu ch'iyavua ch'iona wenye mavao,*
>
> *Kwamba ni majaaliwa ndio wajaaliweo,*
>
> *Name niwapo kupewa nalingana na wao,*
>
> *Hindi ndiko kwenye nguo, na wendao tupu wako.* (Abdulaziz 1979)

Hapa, anasema kuwa anapofungua macho yake na kuona watu wakiwa na mavazi mazuri, yeye hujiambia kuwa ni majaliwa ndio wajaliwao. Naye fursa yake inapofika, ata yeye atavaa bora kama wao. Hivyo, anamaliza kwa kusema kuwa 'Hindi ndiko kwenye nguo, na kunao wanaoenda tupu.' Maudhui haya yamepelekewa na itikadi ya ukandamizaji kwani tumepata kuwa mtunzi amekandamika sana kimaisha. Kiasi cha anatamani sana siku yake

ya kuwa tajiri ifike ili ata yeye avae bora kama wao. Hivyo migao iliyoko katika zile tabaka za Marx (1979) tunapata mtunzi akizipokea na anaandika kuhusu matabaka, matajiri na masikini.

Maudhui ya umaskini pia yamo katika shairi la '*Ufukara enda zako.*'. Muyaka anaufukuza ufukara kwani waliagana. Mtunzi hataki kukandamizwa tena na ule ufukara. Anauambia uende ukawafuate wengine. Ili uwatie wasiwasi kiasi cha nyonyo zao zisikitike. Anaongeza kuwa ule ufukara umemkumba mtunzi naye mtunzi amekabiliana nao. Hivyo, wanaagana kwa heri. Katika ubeti huu, inasemekana Muyaka aliutunga alipoambiwa kuwa anakwenda kumrithi jamaa aliyefariki huko Pemba (Abdulaziz, 1979).

Mwisho, maudhui haya yalipatikana katika shairi la '*Kupata haya si haba.*' Mtunzi anamshukuru Mungu na anasema kuwa hali aliyokuwa katika, ndio hali ya maisha. Hii ni hali ya wanadamu kupata mema na mabaya yakamuondokea. Mwanadamu huongozwa na rehema ya Mungu milele. Naye mtunzi anakiri kua yamemkumba yaliyomema na mabaya na alichonacho anasema si kibaya. Hivyo hakuna ambalo asilolifahamu. Mashaka yaliyompata, mazito na magumu, Mungu alimuondolea. Mwishowe, mtunzi anatabasamu. Anamalizia kwa kusema kuwa anamshukuru Mungu kwa kupata aliyonayo na hio ni baraka kutoka kwa Mungu. Kutokana na hayo, inathihirika kuwa Muyaka alikuwa amekandamika sana kiuchumi. Alikuwa anawategemea walinzi, jamaa na marafiki wake (Abdulaziz, 1979). Ndiposa hapa tunapata akimshukuru Mungu kwa kumuondolea mashaka na mazito. Anasisitiza mazuri ambayo Mungu aliomfanyia na ndio maana anasema kupata aliyonayo ni baraka na haezi lalamika.

#### 3.1.1.3 Maudhui ya Magonjwa na Kifo

Mashairi ya Muyaka bin Haji tulipata yanagusia kwa kina magonjwa na kifo, hasa

muktadha wa maadili ya jamii, hatima ya binadamu na mtazamo wa kisiasa. Itikadi ya ukandamizaji wa kimwili ilichangia uteuzi wa maudhui ya magonjwa na kifo. Haya ni kupitia mitazamo ifuatayo; kijamii (kifo na magonjwa kama fundisho la maadili), kidini (imani ya Kiislamu kuhusu maisha na kifo), kisiasa (kifo kama matokeo ya uongozi mbaya na vita) na kiuchumi (magonjwa yanayoathiri masikini zaidi kuliko matajiri).

Kupitia mtazamo wa kisiasa, Muyaka anaonyesha jinsi K'ongowea ilivyougua katika shairi la '*Kongowea yaugua*.' Muyaka hapa anaanza kwa kusema kuwa K'ongowea yaugua kwa vilio vya maumivu. Hii ni sababu ya mambo kubadilika. Mtunzi ndiposa anamwambia Mungu aipe Kongowea afueni kwani hakuna lolote linalomshinda. Anamalizia ule ubeti kwa kusema wamaizi mjini ule wakutane ili watafute njia mwafaka ya kufanyia.

*...Kongowea yaugua, kwa kite na uuguzi,*

*Kwa mambo kuyageua, kugeua mageuzi,*

*Rabi, Ngwaipa afua ! Na kuiafu si kazi,*

*Kutanani wamaizi shauri jema mtende. ...* (Abdulaziz 1979, uk 202)

Ubeti huu pili, Muyaka anasema wamaizi wakutane kwani ni wana wa Kongowea. Wainue mikono juu huku wakiombea ile mji wao. Haya ni ili watu wa Kongowea wasibadilishe nyoyo zao bali waendelee kufanyia linalostahili. Kwa mujibu wa Abdulaziz (1982) shairi hili limepewa tafsiri mbili. Kwanza, linarejelea wakati ambapo kulikuwa na janga la ndui humo Mombasa. Pili, kuwa Mombasa ilikuwa hoi kama mgonjwa kwa sababu ya ugomvi wa ndani. Ndiposa, mtunzi anasema K'ongowea yaugua na anawaomba wamaizi waombee ule mji ili watu humo wasibadilishe nyoyo zao bali waendelee kufanyia linalostahili. Hapa, itikadi ya ukandamizaji ilipelekea mtunzi kushughulikia utungo huu pale anapotuchorea kuwa ugomvi wa ndani unasababisha magonjwa mjini na pia kuwaambia watu

watangamane na kuombea Kongowea ili kuleta mabadiliko mjini humo.

Muyaka pia anazungumzia kifo katika shairi la ‘*Kifo kikimbizwa funza*.’ Anauliza ni wapi maiti inaweza ekwa ili kuikinga dhidi ya wadudu ili isiendelee kuumia. Anasema kuwa ipewe mabaniani kwani wanajua mahali pakuiweka. Watateka kuni na kuitengenezea ile maiti moto wa kuichoma hadi kuwa jivu. Hivyo, anauliza inapochomeka, ile maiti iliyogeuka kuwa jivu itawezaje umizwa na wadudu. Kutokana na lile shairi, tunapata kuwa Muyaka anashughulikia masuala ya maiti kukandamizwa na wadudu ndiposa anauliza ni wapi wataekwa ili wasiendelee kuumia. Muyaka anahimiza uvumilivu na unyofu kwa jamii, akionyesha kuwa hakuna anayeepuka kifo. Anaonyesha kuwa tabaka lolote linaweza kufariki, hivyo watu wanapaswa kuishi kwa maadili mema. Hivyo itikadi ya ukandamizaji ilipelekea maudhui haya ya kifo kwani mtunzi anaonyesha jinsi maiti anavyokandamizwa na wadudu.

Haya pia yamo katika ukurasa 232, shairi la ‘*Aliyekimbia Ole*.’ Hapa, Muyaka anasema kuwa hakuna aliyekimbia kifo kwa mwendo wa miaka sitini. Mtu anapofika pale mitilizini, hupata anaambiwa, ‘njoo tukale, mwandani wangu mwandani !’ mtu anapouliza ni nani yule anayemkaribisha, hujibiwa, ‘simi waleo.’ Kutokana na hayo, inadhihirika kuwa mtunzi alimaanisha kuwa kifo humkumba kila mtu kwa wakati fulani.

Muyaka pia anawahimiza watu wakubali magonjwa na kifo kama sehemu ya maisha ya kijamii. Hii ni itikadi ya kidini inayodhihirisha ukandamizaji wa binadamu, inayohimiza uvumilivu na kuacha malalamiko. Hapa, Muyaka anaadhirika pakubwa na itikadi ya uhuru wa kiakili na ukandamizaji unaosababishwa na magonjwa. Haya tunayapata ukurasa 188 katika shairi la ‘*Aha*.’ Shairi hili limetungwa na Muyaka wakati alipokuwa mgonjwa. Mtunzi anasema kuwa ugonjwa unamuumiza. Hana afya mwilini mwake mzima. Hapati

raha na ndio maana anasema aha ! Katika kibwagizo anasema kuwa hasemi kwa wema ila ni kwa ule ugonjwa anaougua. Vilevile, anaongeza hajaugua kwa kujitakia. Anaugua homa na kichwa. Na wazazi hawaoni kwa furaha ila anawaona wakifuta machozi.

Muyaka pia anaendelea kuonyesha kuwa magonjwa yanavyoathiri na kuwakandamiza masikini zaidi kuliko matajiri, hasa wafanyabiashara na wakulima. Kupitia uhuru wake wa kiakili tunaona jinsi ugonjwa unamkandamiza masikini. Mfano wa shairi ; *"Dunia ya mateso."* "*Masikini akiumwa, hana wa kumwangalia, matajiri akikohoa, daktari hupo tayari."*

Muyaka kufuatia itikadi ya ukandamizaji wa kiuchumi, anakosoa mfumo wa kiuchumi ambapo matajiri wanapata huduma bora za afya. Huku masikini wakiachwa kuteseka. Kwa Mujibu wa Marx (1977), mfumo huu unaonyesha unyonyaji wa kiuchumi, ambapo tabaka la juu linadhibiti rasilimali za afya. Hii ni hoja ya ukosefu wa usawa wa kijamii. Mtunzi anasema kwa uwazi kuwa masikini wanakufa zaidi kwa sababu hawana uwezo wa kupata matibabu.

Vilevile, Muyaka anaonyesha kifo kama sehemu ya mapambano ya kijamii ya Kiswahili dhidi ya wageni na watawala dhalimu. Mfano wa shairi ; "*waliokufa kwa Nchi*." Hapa Muyaka anaonyesha kuwa kifo cha kishujaa ni sehemu ya kujitolea kwa taifa. Kwa mtazamo wa Gramsci (1985), hii ni itikadi inayopinga hegemonia, ambapo jamii inajitambua na kupinga ukandamizaji. Hii inaonyesha kuwa maudhui haya sio tu mwisho wa maisha, bali ni sehemu ya harakati za kijamii na kisiasa. Hivyo, itikadi ya ukandamizaji na mapinduzi ya nguvu yaliathiri mtunzi pakubwa hapa. Anashughulikia suala la ukandamizaji wa wageni na pia mapinduzi ya nguvu ambayo yanapelekea kuwepo kwa vifo. Anaonyesha kifo kama sehemu ya mapambano ya jamii ya kisiasa.

### 3.1.2 Maudhui yaliyopelekewa na Itikadi Ya Mapinduzi Ya Nguvu

#### 3.1.2.1 Maudhui ya Uzalendo na vita

Mashairi ya Muyaka Bin Haji yanaonyesha mwelekeo wa kisasa na wa kimapinduzi kinyume na utunzi wa kidini uliokuwa umetawala kipindi cha urasimi mkongwe. Muyaka alijikita katika maisha ya kijamii, siasa, uchumi na mapambano ya tabaka la chini, hali ambayo inaakisi msukumo wa kiitikadi wa kupinga dhuluma na kuhimiza ujasiri wa kijamii. Uteuzi wake wa maudhui na mtindo wa kuelezea mambo mengi na yote yaliyoko katika jamii ni ushahidi wa wazi wa msukumo wa mapinduzi ya kiitikadi.

Kwa mujibu wa Marx (1977 na 1979), historia ya jamii ni historia ya migogoro ya kitabaka. Katika kazi zake, Marx anaeleza kuwa tabaka la watawala hutumia fikra, dini, sheria na taasisi nyingine ili kuendeleza maslahi yao. Maoni yangu ni kuwa Muyaka kupitia mashairi yake ya kijamii, anapinga hali hii kwa kutumia mashairi kama chombo cha mapambano ya kijamii, jambo ambalo linaendana na dhana ya Marx ya "ung'amuzi potoshi"

Tunapata kuwa tungo nyingi zake aliziandika wakati wa ukoloni wa Waarabu wa Omani mjini Mombasa. Tungo hizo zilizungumzia uzalendo na mapambano ya kivita, haswa kutokana na uhalisia wa kipindi cha mtunzi. Mazingira ya kipindi chake yalichangia pakubwa katika tungo zilizoegemea mapinduzi yaliyosheheni nguvu. Katika karne ya kumi na tisa kulikuwa na vita vikali mjini Mombasa. Mwandishi katika tungo nyingi anaonyesha namna wenyeji walipambana kivita ili kukata miyororo ya ukoloni na unyanyasaji, na pia kupinga juhudi za kutawaliwa.

Katika shairi la, "*Vikija Mtaviweza*" la Muyaka ambalo limenukuliwa katika Abdulaziz 1979 :133-134), mwandishi ametaja vifaa na zana zilizotumika katika vita. Abdulaziz avitaja vifaa k.v mata, mafumo, ngao, p'anga, p'anga-kule, vitara, msu, ngurumza na

fimbo. Pia anatueleza kuwa kulikuwa na ngoma na michezo maalum iliyotumika na wenyeji ili kufanikisha mafunzo kwa vijana ya jinsi ya kutumia zana za vita vizuri na suala la vita kwa ujumla. Muyaka pia anataja ngoma ya kizungup'ia, ambayo ilikuwa ni mchezo wa vita uliohitaji matumizi ya nguvu iliochezewa kando ya bahari.

Maudhui ya vita pia yamo katika shairi la '*Kafa Li Man Hadhara'* ukurasa 133. Muyaka akinukuliwa na Abdulaziz anasema :

> *Dunia liwazingia ikawa kama duwara,*
>
> *Wasipate pa kuingia, mfano kama majura,*
>
> *Vijana vya K'ongowea wakijaribu vitara,*
>
> *Kafa li man hadhara! Watambi mumesikia.* (Abdulaziz 1979*)*

Katika ubeti huu mtunzi anasema kuwa dunia imewazungukia kama duara, kiasi cha kuwa hawapati pa kuingia mfano wa wapumbavu. Anaongeza kuwa vijana wa Kongowea wamejaribu vitara. Vitara ni aina silaha ya vita zilizotumika. Mwishowe mtunzi anasema kuwa wale vijana wana nguvu sawa na wale watambi wa Omani. Muyaka hapa ametumia maneno ya kiarabu kuwalenga wale watambi wa Omani wa Said. Kutokana na hili mtunzi anawapa ari wenyeji wa Mombasa kwa kuwalinganisha na watambi wa Omani. Muyaka anasema kuwa wamejiandaa na wenyeji wananguvu sawa na wale watambi hivyo wataweza kupambambana nao dhidi ya ukandamizaji wa Waarabu. Hivyo kujiondoa kutoka kwa minyororo ya Waarabu. Hapa itikadi ya mapinduzi ya nguvu inachangia shairi hili sababu mtunzi anaongelea kuhusu vita vya kuwaondoa Waarabu utawalani na wanajamii waweze kujitawala. Pia mtunzi anataja kifaa cha vita 'kitara.' Hivyo anashughulikia yaliyoko katika mazingira yake na kutaka ule mbadiliko kama Marx (1977) anavyoakisi kuwa tabaka la chini hung'ang'ana kusababisha migogoro ambayo hupelekea

mapinduzi ya uongozi mbaya.

Isitoshe, haya yamo katika shairi la '*Mwatupa Shauri Gani*?' ukurasa 136. Hapa Muyaka anaeleza hisia iliyohisiwa wakati wa vita baina ya watu wa Mombasa na Seyyid Said. Itikadi ya mapinduzi ya nguvu inapelekea awaambie watu wa Mombasa watafute suluhisho na pia waombe na watafute la kutenda. Hii ni sababu wakati vita vitakapoanza vitanuka vibaya. Yaani vita kuwa vikali vitakapoanza.

Isitoshe, Muyaka pia anashughulikia mapambano mapya na watu wa Omani kutokana na itikadi ya mapinduzi ya nguvu. Mfano, '*Mwina wa Chiza*,' ukurasa 143. Kushindwa huku katika vita kulikuwa pigo kubwa kwa utawala wa Said. Kabla ya mwisho wa 1829 alituma msafara mwingine mkubwa hadi Mombasa, na kushambulia Kisiwa kutoka njia zote mbili za mashariki na magharibi. Mashambulizi haya yalishindwa kwa urahisi na Wakenya. Tabia ya diplomasia ya Said juu ya kushindwa, alimpa Salim kurejesha mkataba. Salim alikubali lakini kwa sharti kwamba hakuna askari wa Oman waliowekwa kwenye Ngome wakati huu. Imam aliuidhinisha mkataba huo na akarudi nyumbani Muscat.

Katika shairi la '*Kimya*' ukurasa 194, tunapata Muyaka anawaambia watu wasifurahie kimya bali wajue kuwa kimya kina mambo mbele na wakitahadhari. Hicho kimya husababisha moshi kuzuka ghafla. Yaani, huzua vita na watu kupoteza mali yao.

*Kimya kina mshindo mkuu, ndivyo wambavyo wavyele,*
*Kimya chataka k'umbuu viunoni mtatile,*
*Kimya msikidharau, nami sikidharawile,*
*Kimya kina mambo mbele, tahadharini na kimya!* (Abdulaziz 1979)

Mwishowe anawaambia watu wakuwe tayari kila wakati. Hii ni sababu, kimya huleta ukulele au vita. Kimya chatunda p'umzi na vita bado vinaendelea. Hivyo, watu wawe

tayari. Haya yanajitokeza kama ifuatavyo ;

*Kimya vuani maozi, vuani mato muole !*

*Kimya kitaangusha mwanzi mwendako msijikule,*

*Kimya chatunda p'umzi kiumbizi kiumbile,*

*Kimya kina mabo mbele, tahadharini na kimya.* (Abdulaziz 1979)

Shairi hilo linarejelea utulivu uliovuma katika vita na Sayyid Said. Muyaka anawaonya wananchi kutochukulia amani kama jambo la kawaida. Bali, wakae tayari kwanza badala ya kufurahia ule utulivu na kimya, endapo shambulio la kushtukiza lingetokea. Muyaka anamkosoa mfuasi wa mifumo ya kidini au kijamii bila kufikiri, jambo ambalo linamaanisha kuwa anahamasisha watu kufikiri nje ya mfumo, hali inayolingana na dhana ya kupambana na itikadi tawala kwa kutumia fikra huru, kama inavyodokezwa na Marx (1977)

Tunapata vita pia katika shairi la '*Ai Mambo*' ukurasa 217. Mtunzi anasema kuwa kuna mambo mengi ambayo yajayo. Anamwambia Bwana Mjombo, kumaanisha mtu muoga, aondoke pamoja na marafiki waliosalia. Jina hilo huenda lilikuwa jina la majazi.

*Ai mambo ai mambo makuu yayao,*

*Ondoka Bwana mjombo na wenzio waseleo,*

*Wangoma wenele fimbo za t'utu na kiwapio,*

*Napakiwa mke nduyo nae mwondole ndiani.* (Abdulaziz 1979)

Vilevile, wanaocheza ngoma nao wamejihami na fimbo za t'utu na kiwapio kwa pamoja. Naye mke wa nduguyo kama yupo, pia aondolewe njiani. Hapa huenda shairi hili linarejelea vita walivyokuwa wakivitarajia wakati huo wa Muyaka. Mishororo wa mwisho nao unamaanisha kuwa yule adui anayekuja atafedheheshwa sana hivi kwamba wanawake

hawakupaswa kuwa karibu. (Abdulaziz, 1979).

Gramsci (1985) anazungumzia uwezo wa tabaka tawala kudhibiti mitazamo ya watu kupitia hejemonia, yaani ukubalifu wa hali ya mambo kama kawaida bila upinzani wa moja kwa moja. Muyaka, kwa kutumia mashairi yenye mwelekeo wa kuhamasisha, anakusudia kuvunja ukawaida na imani hizi potofu, kwa kuonyesha kuwa si lazima jamii ifuate mkondo wa utii na kunyamaza mbele ya udhalimu. Alifungua milango ya fikra na kuwapa watu wa kawaida jukwaa la kufikiri upya nafasi zao katika jamii. Haya yanaashiria kuwa mtunzi aliongozwa na itikadi ya ukandamizaji na mapinduzi ya nguvu kwa kushughulikia mapambano ya kuondoa utawala unaowakandamiza.

### 3.1.3 Maudhui Yaliyopelekewa na Itikadi Ya Uhuru Wa Mtunzi

#### 3.1.3.1 Maudhui ya Utamaduni

Mwandishi katika utunzi wake alishughulikia kipengele cha utamaduni na mila. Kutokana na mazingira yake, mtunzi anatawaliwa na itikadi ya uhuru wa kiakili kwa upana. Alisifu sana mila na desturi za watu wa pwani haswa mila muhimu katika utamaduni husika. Alisisitiza suala la wanajamii kujikita katika utamaduni na mila na kuepuka kupotoka kutokana na mtagusano baina yao na watu wa jamii zingine.

##### 3.1.3.1.1 Chakula

Chakula kilicholiwa sana katika jamii ya Muyaka wakati huo, kilikuwa ni mseto wa mchele na mtama uliopikwa na nazi, kwa kitoweo cha samaki, nyama au mboga. Inaonekana pia jamii ya mtunzi, ilitumia ngano, matunda na samli kama chakula. Abdulaziz (1982) anasema kuwa katika tungo nyingi za Muyaka, ametaja kuwa ngano ilitumika kama “chakula mbadala” hasa na matajiri. K.v;

*Ai ngano na samli, viliwa vyema khiyari,*

*Vitu viawavyo mabali, Renu na Baunagari,*

*Apo mwende akali, Mola humjaza kheri,*

*Ai ziwa na sukari! Itakapokukutana.*

Katika utungo wa "*Panda*" ukurasa 190 (Abdulaziz, 1982), Muyaka anasema;

*Panda nganu na mpunga afudhali ya viliwa*

*Panda wimbi na kimanga vipawa vya kupewa*

*Panda usitunde ch'anga, tauwa mbivu tauwa*

*Panda ni wakouluwa, panda darajani, panda !* ` (Abdulaziz 1979, ubeti 3)

Wakati huo wa Muyaka familia zilijihusisha na kilimo ili kuweza kujikimu kimaisha na hata kutega uchumi. Familia zote zilizoweza kupata mapato na kujikimu kimaisha kwa kumiliki mashamba katika sehemu za bara zilizozingira kisiwa cha Mombasa. Watu walilima mpunga, mahindi, miboga, machungwa, wimbi, ndizi, maembena mboga za aina tofauti. Katika shairi hapo juu, tunapata uhuru wa mtunzi pale anataja vyakula walivyopanda wakulima. Na vyakula hii vinadhihirisha utamaduni wa jamii husika.

Vilevile, katika shairi la '*Tanzi za nyama*,' maudhui haya yanajitokeza.

*T'anzi za nyama, t'anzi mkivumiza,*

*Kukanya wakurufunzi sote vyatusangaza,*

*Tujile na yetu runzi twatafuta vya kuwaza,*

*Mwauza, au ni mituzi yenu ?* (Abdulaziz 1979, uk 172)

Katika shairi hili, Muyaka anazungumzia jinsi mvuvi mmoja alivua samaki lakini hangewapa watu waliomsaidia kuegemeza mashua samaki. Watu hawa waliwasaidia walipotoka kuvua kwenye ziwa kuu. Lakini Muyaka anakashifu tabia ya wale wavuvi ya kutowauzia watu wale samamki wala kuwabadilishia wale Samaki na mchele.

Uvuvi wa samaki pia unajitokeza katika ukurasa 274 katika shairi la '*Kuvua numbi si kazi*,' nukuu la Abdulaziz (1982)

> *Enywi wavuvi wa leo kuvua hamkuwezi,*
> *Ni neno mzoeleo, kuliwata ni majonzi*
> *Mwapata na kialio cha wali na mtunzi,*
> *kuvua numbi si kazi, kuu ni magawioni* (Abdulaziz 1979, ubeti 1)

Hapa Muyaka anakejeli wavuvi ambao hawangewapa watu chochote. Hawa watu waliwasaidia kuegeza mashua baada ya kutoka kuvua katika ziwa kuu. Wale watu wanaozungumziwa hapa hawakuwa na uwezo wa kununua wale samaki. Mtunzi anasema katika lile shairi kuwa wavuvi wale walivua ngwe na kozi ila hawawapei wana wa pwani chochote, wasio na uwezo wa kununua samaki. Kutokana na hayo, inadhihirika kuwa watu wa jamii ya Muyaka walizoea kula samaki na hata mchele. Kutokana na uhuru wa kiakili wa Muyaka tunapata mtunzi akivitaja vitu hivi viwiali na maneno yale yanatokana na utamaduni wa Waswahili wakati wake mtunzi. Mtunzi alitoka kwa uandishi wa kidini na utamaduni na kushughulikia chakula kwa kufuata mkondo wa uvuvi na ukulima. Kando na Mwanakupona, Muyaka alituonyesha vyakula vilivyopatikana katika ulimwengu wake kwa kuvitaja katika tungo zake.

### 3.1.3.1.2 Mavazi

Katika baadhi ya mashairi yake, mtunzi anataja mavazi ya wanaume Waswahili kama Kanzu ambalo ni vazi lililovaliwa sana. Hili ni vazi lenye mikono mirefu na linalofika miguuni lililotengenezwa na malighafi tofauti tofauti lakini jeupe. Anataja pia kitambi ama kikoi ambayo ilivaliwa chini ya kanzu. Vilevile Muyaka anataja Kizibao. Hili ni vazi liliibuka ambalo haikuwa lazima liwe na mikono mirefu na lilikuwa angavu. Pia mtunzi

unatutajia kitambaa kilichofungwa kiunoni ambacho kilitumika sana ili kuzuia kanzu kumsumbua mtu aliyeivaa anapokuwa akifanya kazi na pia kilitumika kushikia silaha za kivita kama kisu, upanga, majambia na pembe za unga wa bunduki. Mtunzi anasema "jifungetoni masombo" ikiwa na maana ya kuwaomba watu wakaze vikoi vyao. Upande wa wanawake Waswahili, mtunzi anasema kuwa walihitajika kuvalia visutu au leso zilivyotengenezwa kwa pamba. Wanaweka wa tabaka la chini nao walivalia kaniki na leso zilizotengenzwa kwa pamba hafufu iliyokuwa ya bei rahisi. Pia walivalia mikufu, shanga na vipuli mbali mbali. Mfano unajitokeza katika utungo wake wa "*Si Wanawake wa Huja*";

*Ukiwaona kwa mbali, kwa vikuku na viganja*

*Wamba ni wake wa kweli ukienda wakidhi haja*

*Kanan ni batili swiswi na wao mamoja,*

*Si wanawake wa huja yalla ni yale mavao.* (Abdulaziz 1979, uk 172)

Uhuru wa kiakili wa mtunzi ulipelekea kipengele hiki cha mavazi kwani mtunzi anaeleza mavazi yaliyopatikana katika jamii yake kwa kina. Isitoshe alitueleka jinsi pia watu wa tabaka tofauti walikuwa na mavazi tofauti. Uhuru wake wa kiakili unamfanya kuvuka mipaka na kuonyesha jinsi ile migao ya kitabaka ilipelekea watu kutofautishwa hadi na mavazi. Haya ni tofauti na yaliyo katika *Utenzi wa Mwanakupona*.

**3.1.3.1.3 Maudhui ya Usafiri**

Katika kipindi hiki cha mtunzi shughuli ya usafiri ilikuwa barabarani na ni wanyama kama punda na farasi waliotumika. Mfano umo katika shairi la "*Mfuga Punda.*" Kulingana na Abdulaziz (1982) vilevile kulikwa na usafiri wa baharini uliotumia mashua na mitumbi hasa usafiri uliomlazimu mtu kutoka kisiwa kimoja kilichokuwa karibu na kingine. Pia, wanabiashara waliotoka mbali kama Uarabuni na India, walitumia meli katika usafiri wao.

Mfano uliohapa chini, mtunzi anatueleza jinsi watu walitumia mashua :

*Simba ndume na wambuji, sikizanitatongoa,*

*Naketele vitongoji, na safari za mashua,*

*Leo nakumbuka mbiji, ya kutweka na kutua,*

*Ai, pato na pewa, litako kukutana. (Abdulaziz 1979, uk 206)*

Usafiri kwa kutumia mashua pia unajitokeza katika shairi la '*Kuvua numbi si kazi*,'katika ukurasa 274. Muyaka katika shairi hili anawakejeli wavuvi ambao hawangewapa watu chochote. Hawa watu waliwasaidia kuegeza mashua baada ya kutoka kuvua katika ziwa kuu. Wale watu wanaozungumziwa hapa hawakuwa na uwezo wa kununua wale samaki. Kutokana na hayo, inadhihirika kuwa usafiri pale katika ziwa kuu ulihusisha mashua. Haya ni kutokana na pale mtunzi anasema kuwa wale wavuvi walikuwa wanatoka katika ziwa kuu na walihitajika kuegeza mashua zao. Hivyo, walisaidiwa na wale watu wanaorejelewa kama wana wa pwani ili kuegeza mashua zao. Itikadi ya uhuru wa mtunzi wa kiakili ulipelekea mtunzi ashughulikie dhana hii ya usafiri ambayo ilipatikana katika ulimwengu wa mtunzi. Kando na uandishi wa kitambo ambao uliegemezwa kwa dini na utamaduni, mtunzi anavuka mpaka na kutuonyesha jinsi usafiri uliendelezwa katika jamii yake na kudihirisha mapinduzi yaliyotajwa na Marx (1977). Muyaka hapa anashughulikia suala la mengi ambayo ni tofauti ikilinganishwa na Mwanakupona ambaye anashughulikia tu ndoa, dini na utamaduni katika utenzi wake kwa mujibu wa kanuni za uandishi wa urasimi mkongwe.

**3.1.3.2 Maudhui ya Dini**

Kwa Mujibu wa Karisa na Mwinyifaki (2017), Uislamu ulipoletwa na Mtume Muhammad ulikuta ushairi upo. Nyakati hizo kulikuwa wa washairi mashuhuri katika kabila la Kiarabu

kama vile Immil Qais, Zuheer bin Khaab, Hassan bin Thabit na Farazdak. Kwa umahiri wao katika utunzi, Mtume Muhammad aliwatumia washairi hawa kuwahamasisha wanajeshi wake wakati wakienda katika vita vya jihad. Hivyo Uislamu uliingizwa katika Kasida. Kutokana na hayo ni wazi kuwa ushairi ulianza kutumika kitambo kama chombo cha dini ya Kiislamu, hususan katika kuwahamasisha Waislamu kuhusu Uislamu. Haya yalipelekea kuwepo kwa istilahi na mawazo ya Uislamu na pia maelezo ya hisia za kidini katika tungo zilizotungwa hasa katika kipindi cha uongozi wa Umayyad (Shahid, 1980). Ushairi wa Kasida ulipoletwa katika jamii ya Waswahili ulikuwa tayari una majukumu ya kuhamasisha watu juu ya Uislamu. Hii ndiyo sababu iliyowafanya watunzi wa tenzi za Kiswahili kutumia tenzi zao kuhubiria mafunzo ya Uislamu kwa mfumo wa 'iktibasi' (Karisa na Mwinyifaki, 2017)

Muyaka anahimiza watu kuaminia dini, jambo ambalo lilipatikana katika tungo za kirasimi. Uhuru wake wa kiakili ulimfanya ashughulikie masuala mengi yanayohusiana na dini ifuatavyo ;

Katika shairi la '*Mwanadamu kup'ani*,' ukurasa (216), Muyaka anauliza ni kipi ambacho mwanadamu atakupa ambacho kitamtosha mwenziwe ? Kumaanisha kuwa mwanadamu hawezi mtosheleza mwenziwe. Katika mishororo wa tatu tunapata mtunzi akisema kuwa Mungu pekee ndiye ana uwezo wa kumpa mwanadamu kitu kiasi cha kumtosheleza, kwani hatawahi acha kumpa mwanadamu anachotaka. Hii ni sababu sisi ni waumini wake ambao hutajia rehema yake kila wakati. Hapa ni dhahiri kuwa kuna utegemezi wa binadamu haswa, waumini kwa Mungu. Hapa, Mungu anaonekana kama kiumbe kikuu ambacho kina uwezo wa kuwatosheleza binadamu kila wakati. Ila si binadamu mwenye hii nguvu.

Maudhui haya pia yamo katika shairi la '*Kongowea yaugua*,' ukurasa 202. Muyaka hapa

anaanza kwa kusema kuwa K'ongowea yaugua kwa vilio vya maumivu. Hii ni sababu ya mambo yanabadilika. Mtunzi ndiposa anamwambia Mungu aipe Kongowea afueni kwani hakuna lolote linalomshinda. Anamalizia ule ubeti kwa kusema wamaizi mjini ule wakutane ili watafute njia mwafaka ya kufanyia. Katika ubeti wa pili, anasema wamaizi wakutane kwani ni wana wa Kongowea. Wainue mikono juu huku wakiombea ile mji wao. Haya ni ili watu wa Kongowea wasibadilishe nyoyo zao bali waendelee kufanyia linalostahili.

Maudhui ya dini pia inajitokeza katika ukurasa 236 katika shairi la '*Mwivi Alokwiba Changu*.' Hapa, Muyaka anamlaani mwizi aliyeiba kitu kutoka kwake. Muyaka anasema kuwa yule mwizi ameondoa utukufu wake. Aliiba twangu, kombe na hata kijaluba chake. Ndiposa, mtunzi anamwambia Mungu ampe yule mwizi maovu (ngwampa fumo) na ukuba, yaani, amuadhibu kwa kumpeleka jehanamu. Muyaka pia anaongeza kuwa toba yake Mungu asiikubali na vilevile afe katika hali ya hazaya. Hapa, tunapata kuwa kuna masuala ambayo humu duniani, binadamu huyaweka mikononi mwa Mungu. Masuala yanayojitokeza hapa ni kama binadamu kuomba toba, adhabu zinazohusihwa na watu kuenda jehenami na pia adhabu ambazo binadamu hawezifanya. Ndiposa, Muyaka anaacha haya yote mikononi mwa Mungu. Hii ni sababu hangeweza kumuadhibu yule mwizi ila anaacha haya mikononi mwa Mungu. Vilevile, tunapata mwandishi anaamini kuwa kuna maisha ya baadaye, baada ya kifo. Haya yanapatikana pale anasema Mungu ampe ukuba.

Maudhui haya pia yanajitokeza katika shairi la '*Hakuna Lisilokuwa*,' ukurasa (264). Shairi hili lilirejelea wakati ambapo Muyaka, alikuwa akisubiri kurithi mali kutoka kwa jamaa wake aliyefariki huko Pemba. Wakati huo Muyaka alikuwa fukara. Mtunzi anasema kuwa anasafiri kuenda Ngezi-maji, katika vitongoji vya Twaka. Tunampata akiongeza kuwa

Mungu hamuachi mja wake na hakuna ambalo linalomshinda Mungu. Hivyo, watu waombe Mungu. Vilevile, Mungu huondoa watu kutoka maangamio.

Haya yanaoana na yalioko katika shairi la '*Kupata haya si haba*,' katika ukurasa 309. Kutokana na hilo shairi tunapata mtunzi anamshukuru Mungu na anasema kuwa hali aliyokuwa katika, ndio hali ya maisha. Hii ni hali ya wanadamu kupata mema na mabaya yakamuondokea. Mwanadamu huongozwa na rehema ya Mungu milele. Naye mtunzi anakiri kuwa yamemkumba yaliyo mema na mabaya na alichonacho anasema si kibaya. Hivyo hakuna ambalo asilolifahamu. Mashaka yaliyompata, mazito na magumu, Mungu alimuondolea. Mwishowe, mtunzi anatabasamu. Anamalizia kwa kusema kuwa anamshukuru Mungu kwa kupata aliyonayo na hio ni baraka kutoka kwa Mungu. Kutokana na hayo, inadhihirika kuwa uhuru wa mtunzi wa kiakili ulimfanya ashughulikie dini. Muyaka alimuamini Mungu ndiposa hapa tunapata akimshukuru Mungu kwa kumuondolea mashaka na mazito. Anasisitiza mazuri ambayo Mungu aliomfanyia na ndio maana anasema kupata aliyonayo ni baraka na haezi lalamika.

Dini pia imo katika shairi la '*Simuwati Muwatiwa*,' ukurasa 296. Hapa, haijabainika kwa uwazi kama mtunzi anamaanisha mtoto au mtu mzima aliyeachwa katika uangalizi wa mtunzi. Anasema kuwa watu wasikilize kwa makini na vilevile walio na macho wajionee wenywe. Kuwa mtunzi haezi muacha wake aliyekuwa katika uangalizi wake. Anayerejelewa huenda anampa mtunzi machungu lakini mtunzi ataendelea kumtunza. Haya ni sababu Mungu, muumba wa jua na mwezi, ni yeye anasababisha yote. Kupitia haya, ni dhahiri kuwa mtunzi anaiamini dini. Tunampata akikiri kuwa Mungu ndiye husababisha yayaowatendekea wanadamu. Hivyo, mtunzi hana shaka kupatwa na hofu ama kumuacha anayerejelewa katika shairi.

Dini pia imo katika shairi la '*Tima na Ima*,' ukurasa 244. Hapa, mtunzi anayataja majina ya wanawake wa Mombasa ambao ni Tima, Ima, Mwaniya na Mwanakombo. Wanawake anawataja sababu ya tabia ya ulevi na usherati. Walikuwa waraibu wa pombe kiasi cha kuwa walikiuka tamaduni na dini wa Islamu. Waislamu waliamini maisha ya baadaye na wanawake hawa walikiuka haya. Walifanya dhambi kwa uwazi bila kujali yeyote. Kutokana na hayo, tunapata kuwa mtunzi anaonyesha uhuru wake wa kiakili pale anapoonyesha kuwa wale wanawake walikiuka masuala ya kidini na tamaduni zao. Mtunzi anasema;

*Katika Tima, na Ima, Mwaniya na Mwanakombo,*

*Wakeel kama wagema kwa kufurahia tembo,*

*Tukiwambia, si vyema na kuzimu kuna mambo,*

*Walisema, havijambo, hata twendapo n'lini?* (Abdulaziz 1979)

Kutokana na kipengele cha dini, inabainiska kuwa mtunzi aliathirika pakubwa na itikadi ya uhuru wa kiakili kwa anashughulikia masuala mengi ya dini. Mtunzi anashughulikia masuala ya kuamini Mungu, kuamini kuwa ni yeye anayelipiza maovu, anaamini maisha ya baadaye na pia anaamini kuwa Mungu ndiye anayemtosheleza binadamu anachohitaji peke yake. Muyaka anashughulikia mengi kuhusiana na dini na hapa anaonyesha utii na uhuru wake wa kiakii kuhusiana na utunzi wa kirasimi.

#### 3.1.3.3 Maudhui ya Ndoa na Mapenzi

Suala la mapenzi hayakushughulikiwa kwa tungo za Waislamu kwa uwazi. Ila kupitia itikadi ya uhuru wa kiakili, Muyaka anakosoa ukandamizaji huu kwa uwazi na anapigania haki za wapenzi. Mfano wa mashairi yake ambapo Muyaka anashughulikia mahaba ni '*Sipati usingizi*,' ukurasa 200. Katika shairi hili, Muyaka anasema kuwa anamtuma njiwa

mwenye macho mazuri ili aupeleke ujumbe kwa mpenzi wake. Huyo njiwa ni mwerevu, hodari na anayefahamu mambo yote. Anamtuma kwanza ampe mpenziwe salamu. Akimkaribia yule mpenzi wa Muyaka, Muyaka anamwambia amnyenyekee na amweleze yaliyo moyoni mwa mtunzi. Amwambie kuwa anapomfikiria yule mpenzi, mtunzi hapati usingizi. Pia, macho yake mtunzi hayaoni kwa kukosa usingizi.

Haya pia yanaoana na yale yanapatikana katika shairi la, '*Enda kaseme Naye*,' ukurasa 222. Hapa, mtunzi pia anamtuma mtu aende akaseme na mpenziwe. Mtunzi anamuelekeza asiseme na yeyeote njiani, asikae na ashike njia iliyowazi. Haya ni ili asije akapotea wala kupoteza muda. Mtunzi anatumana mpenziwe aambiwe kuwa akubali kipendo cha moyo wake. Vilevile, nafasi yake ina machungu na huyo mpenzi ndiye atakayeondoa hayo machungu. Hapa mtunzi anazungumzia hisia kwa uwazi na haya yanaonyesha kuwa mtunzi aliongozwa sana na itikadi ya uhuru wa kiakili.

Mapenzi pia yanajitokeza katika ukurasa 238, katika shairi la, '*Kuonana na wewe*.' Katika shairi hili, mtunzi anamuomba mpenziwe kufanyia lolote ili waweze kukutana. Katika jamii hii ya Kiislamu wa wakati wa Muyaka, wanawake walikuwa wameekewa vikwazo vya kitamaduni na walihitajika kufuata. Kwa mfano, uhusisano na pia kukutana baina ya wapenzi ilikuwa vigumu sana. Kutokana na hayo, ni dhahiri kuwa hizo imani, fikra na hata mitazamo iliyofuatwa na wanandoa, iliwakandamiza wanajamii. Kwa mfano, katika hilo shairi hakuna uhuru wa mtu atakama yu mzima, kufanyia anachotaka. Kama vile vikwazo vinavyomzuia mtu kupatana na mpenziwe. Hivyo, hizo ni imani potofu ambazo tunapata kuwa Muyaka anaamua kuzizungumzia hivyo kuzikiuka kwa kumueleza mpenziwe afanye chochote ili waweze kupatana. Anakosoa huo ukandamizaji na kupitia uhuru wake wa kiakili anayazungumizia katika fasihi yake kwa uwazi.

Ujumbe huu pia unaoana na yanapotikana katika shairi la '*Laiti siwele nyuni*,' ukurasa 328. Shairi hili pia ni usemi wa kutamani na ombi la kuruhusiwa kumtembelea mpenzi wake. Muyaka anasema laiti angekuwa nyuni ambaye angeruka hadi mahai ambapo mpenzi wake yupo. Wangepata nafasi ya kuwa pamoja na ampe lisani yake naye mpenziwe ampe yake. Lakini katika mishororo wa mwisho ubeti wa kwanza, anasema kuwa anatamani sana kuenda kwa mpenzi wake lakini hana idhini. Vilevile, anaongeza katika ubeti wa pili kuwa anamtamani mpenzi wake sana. Yupo akilini mwa mtunzi na ndio maana Muyaka anahuzunika kwana anatamani kuenda kumuona. Lakini anasikitika kuwa hana idhini. Hili linadhihirisha kuwa kulingana na jamii ya Muyaka, mapenzi na pia kupatana kwa watu wapendanano kulikataliwa. Haswa, bila idhini wa wazazi. Lakini tunapata Muyaka akikiuka haya kulingana na utamaduni pamoja na dini, na kuyashughulikia. Kutokana na hayo, kuna itikadi ya uhuru ambayo inamuongoza mtunzi huyu katika kazi zake.

Vilevile, maudhui haya yamo katika shairi la '*Ulimwengu Usiungile*,' ukurasa 258. Muyaka hapa anamkejeli mwanamke ambaye anatarajia kupata anachotaka lakini chake hataki kumpa mtunzi. Anamwambia kuwa hilo tendo limemfanya mtunzi atake kumuacha yule mwanamke lakini anamuandama Muyaka kama kupe.

Shairi lingine linaloonyesha haya ni '*Ateteyae mtuku*,' katika ukurasa 288. Hapa, mtunzi anajisuta kwa kupotoka na kujihusisha na mwanamke asiyefaa aliyemletea shida. Katika mishororo wa tatu, Muyaka anamrejelea kama 'mtuku.' Ndio maana anasema kuwa 'Ateteyae mtuku ni tanguko la bure.' Tanguko ikiwa na maana kuwa ni kama kujisumbua.

Uhuru wa mtunzi wa kiakili pia unapatikana katika shairi la '*Musiwate kuonana*,' katika ukurasa 314. Hapa, Muyaka anamtuma mjumbe wa Kongowea kwa mpenzi wake ili amsalimie. Muyaka anamwambia mjumbe aongee naye na amwambie kuwa ametumwa na

"Bwana." Mjumbe pia asema kuwa ni lazima wakutane na Muyaka siku hio ili waweze kuonyeshana hisia zao kwa kina ambazo zimo moyoni. Hapa, tunapata kuwa mtunzi alidhihirisha mapinduzi kwa kushughulikia masuala ambayo yalikiuka kaida na tamaduni za jamii ya Waswahili. Tunapata hapa anazungumzia mambo ya kihisia kwa uwazi na haya yalikuwa kinyume na tamaduni za jamii husika. Haya pia yaoana na ujumbe unaopatikana katika shairi la '*Kwamba hutaki Nambia*,' ukurasa 322, ambapo Muyaka anamsihi mpenzi wake kudhihirisha mapenzi yake kwa uwazi ili Muyaka ajue mahali walipo na yule mwanamke.

Suala hili pia linaoaana na yaliyomo katika shairi la '*Ndia mbili zaumiza*,' katika ukurasa 332. Hapa, mtunzi anamkumbusha mpenzi wake kuwa alikuwa amemwambia afanye uamuzi (kumteuza) kuhusu nani aliyemtaka. Hii ni sababu njia mbili zaumiza na angewapoteza wanaume wote wawili Muyaka akiwemo. Lakini hakumsikiza Muyaka. Ndio maana anamwambia katika ubeti wa tatu kuwa angemsikiliza kwani mambo hayangekuwa jinsi yalivyo. Hivyo, yule mwanamke hangekuwa amejawa na chuki jinsi alivyo. Lakini hakuweza kufanyia uamuzi wa kumuacha mmoja wao. Hapa mtunzi kupitia uhuru wake wa kiakili, ameitumia fasihi yake kueleza haya kwa uwazi, ambayo yalikuwa kando na mila na desturi za jamii husika. Haya tunayapata pia katika shairi la '*Madanganyo ni maovu*,' katika ukurasa 304.

Shairi hili ni ombi kwa mwanamke kutimiza ahadi zake kwake mtunzi. Anamuuliza katika ubeti wa pili kwa nini hakutimiza ahadi walizoahidi. Je, ni kwa sababu hakupendezwa sana na mtunzi au yule mpenzi alikuwa na Mawazo ya pili. Ama hakuvutiwa na wazo la wao kuwa wapenzi. Muyakla anasema kuwa hawezi kusubiri tena kwani siku nyingi zimepita.

Pia uhuru wa kiakili wa mtunzi unapelekea kipengele cha ndoa katika fasihi ya mhusika.

Katika shairi la '*Harusi ya Bwana Muyaka*,' ukurasa 278, tunapata shairi likianza Bwana Muyaka kupewa njia siku ya arusi yake huku vigelegele vikipigwa. Tunapata pia Muyaka anajisifu kwamba mtu yeyote asitilie shaka uume wake. Kulingana na utamaduni wa Waswahili, imekuwa desturi kwa bwana harusi kufunga ndoa na kufanyia tendo la mapenzi ili kudhibitisha uume wake na ubikira wa mkewe. Haya hufanyika ili kutoboa kizinda ili damu itoke na kushuhudiwa na jamaa na marafiki kama ubikira wa msichana upo. Hivyo, katika shairi hili Muyaka anawahakikishia jamaa na marafiki zake kuwa hatawaangusha. Kutokana na hayo uhuru wa mtunzi ulidhihirika pale ambapo mtunzi anazungumzia kwa uwazi suala hili la kufanyia mapenzi siku ya harusi ili kudhibitisha uume na ubikira. Masuala haya yalifungamana na tamaduni na vilevile dini ya Waswahili. Hivyo, yalipewa uzito na hayangetajwa kiholela. Lakini, tunapata Muyaka anayazungumzia kwa uwazi na kwa kina. Hiyo, alizungumzia masuala ambayo yalifaa kuwa fiche na takatifu kwa uwazi. Hivyo, kulazimisha suala hilo kuwa wazi katika jamii na kujulikana na kila mtu si mtoto si mtu mzima.  Hivyo uhuru wake wa kiakili kudhihirika kwa uwazi.

Ujumbe huu pia unaoana na yanayopatika katika shairi la '*Mke wa Risasi*,' ukurasa 300. Hapa, Muyaka anamlaani mtu mwingine alimnyemelea na kumtaka kimapenzi mkewe marehemu Risasi. Mwanamke huyu alikuwa katika eda. Kulingana na mitazamo ya Waislamu, mjane akiwa katika eda hakutakikana kuolewa wala kujiingiza katika shughuli za mapenzi. Lakini bwana huyu, alikiuka mtazamo huo na kumtaka kimapenzi mke wa marehemu Risasi. Kupitia hizo shairi, uhuru wa kiakili wa mtunzi unajitokeza kwa kushughulia masuala yote yaliyotokea katika jamii yake. Yawe masuala yaliyoendana au yawe yalikiuka sheria na kaida za jamii.

### 3.2 Itikadi za Mwanakupona zilivyopelekea uwasilishaji wa Maudhui

#### 3.2.1 Jinsi itikadi ya Itikadi Ya Utiifu ilivyopelekea maudhui

##### 3.2.1.1 Maudhui ya Dini

Utenzi wa Mwanakupona ni mojawapo wa kazi mashuhuri katika fasihi ya Kiswahili, ukiakisi itikadi za utiifu, taasubi ya kiume na ukubalifu na ukawaida. Katika muktadha wa kidini, Mwanakupona anaeleza maudhui yanayoathiriwa na utiifu wa maadili, dini, kanuni za Kiislamu, nafasi ya mwanamke katika dini na hatima ya maisha.

Maudhui ya dini ndiyo yamesisitizwa sana katika utenzi huu (Karisa na Mwinyifaki, 2017). Mwanakupona anasisitiza haja ya kuzingatia mafunzo ya dini ya Kiislamu (Wandera, 1996); kumtii Mungu na mtume wake; kupenda kutenda haki kama ilivyo kidini ambayo ilisisitiza utii wa mume na kuishi naye kama dini inavyoagiza kama ifuatavyo;

Maudhui haya yanapatikana katika ubeti wa 4. Hapa, Mwanakupona anamwamnbia bintiye akishaakuja karibu, kwa jina la Mungu yeye anaandika. Anamshauri amsalie Mungu, mtumewe na wafuasi wake pamoja. Haya yanadhihirika ifuatavyo; "*Ukisa kutaqarabu, Bismillahi kutubu, Umsalie Habibu, Na sahabaze pamoya.*" Vilevile, anaongeza katika ubeti wa 5 kuwa akisa kulitangaza jina la Mola muweza, basi anastahili kuomba kwa wingi ili Mola awajalie. Haya yanadhihirisha kuwa Mwanakupona aliamini dini na ndio maana anamwambia bintiye amuamini Mungu pamoja na mitume wake. Pia, anaamini kuwa waumini wanapoomba Mola, yeye huweza kuwajalia. Haya yanadhihirisha itikadi ya utiifu kwani anafuata kanuni za uandishi wa Kirasimi. Ambapo watunzi walilazimika kuanza tungo kwa kulitaja jina la Mungu na tungo zilizosheheni maudhui ya kidini.

Vilevile, katika ubeti wa 12, mtunzi anamshauri bintiye ashike dini. Anamwambia asikatae kutimiza wajibu huo wa kufuata dini. Vilevile, anaongeza kuwa tendo la hiari kidini

ikiwezekana ni wajibu wake kufuata. Kutokana na hayo, ni kuwa Mwanakupona anamshauri akamate dini. Katika Kurani takatifu na Sunnah ndivyo vitu vya msingi katika maisha ya Mwislamu. (Karisa na Mwinyifaki, 2022).

Pia, dini inajitokeza katika ubeti wa 22, na 23. Hapa Mwanakupona anamwambia azifuate Radhi tano. Hizi Radhi tano ndizo ngazi za mamlaka zinazotambuliwa kidini, kwani 'zimekaririwa' na vitabu vya dini. Anaendeleza kuwa mume ndiye atakayeulizwa kama mkewe aende peponi au motoni. Akisema aende pepeoni ataenda mara moja na akisema aende motoni hana budi kuenda. Haya yanapatikana katika ubeti wa 26 na 27.

Mwanakupona vilevile anasisitiza kuwa mke anapaswa kumtii mumewe kwani kulingana na jamii yake tendo hilo lilikuwa njia mojawapo ya kumtii Mwenyezi Mungu na mtume wake Muhammad. Haya ni sababu Mwenyezi Mungu ndiye ambaye amemfadhilisha mume zaidi ya mke. Mwanakupona alisisitiza radhi ya mume, akijua kwamba ni njia mojawapo ya mke kuongezewa thawabu na Mwenyezi Mungu.

Kwa mujibu wa Gramsci (1985), dini ni miongoni mwa vyombo vya kiitikadi visivyo vya moja kwa moja vinavyotumiwa na tabaka tawala kuendeleza mfumo wa kijamii uliopo. Katika utenzi huu, Mwanakupona anatumia dini kama mwavuli wa kuhalalisha nafasi ya mwanamke kuwa mnyenyekevu na mtiifu. Hapa Mwanakupona anaonyesha kuwa dini ni msingi wa maisha ya Mwanadamu, hasa kwa Mwanamke, na ni lazima aishi kulingana na mafundisho ya Kiislamu. Anasisistiza kuwa dini inapaswa kuwa kipaumbele maishani. Hii inaonyesha itikadi ya utiifu wa uandishi wa Kirasimi na pia kanuni za Kiislamu wakati ule. Ambapo tabia, maamuzi na majukumu ya mtu yanaongozwa na mafundisho ya dini.

Isitoshe, maudhui haya yanapatikana katika ubeti wa 36. Hapa mtunzi anamshauri pia kuwa ampumbaze mumewe hadi apumbae. Pia atii amri ya mumewe. Iwapo yule mume

atamtendea maovu yoyote, basi Mungu ndiye atamlipia. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa mwanamke katika ile jamii hangeweza kujibizana wala kukataa amri ya mumewe. Na kwani kila wakati anamtendea wema mumewe, iwapo yule mume atamtendea maovu ya aina yoyote, haezi fanya lolote, ila kumwambia Mungu kisha Mungu atamlipia. Hapa Mwanakupona anaonekana kuwa amepumbazwa na dini kiasi cha anamuachia Mungu majukumu yote. Hadi yale anayoweza jifanyia yeye mwenyewe. Hayo hivyo yanadhihirisha imani ya kidini aliyonayo Mwanakupona. Ndio maana anamshauri bintiye kuwa yanayohusisana na mumewe Mungu atamlipia. Haya yanaashiria kwamba mke anatakiwa akubali hali aliyopewa na jamii na asihoji mamlaka ya mume, jambo ambalo linaonyesha wazi kazi ya dini kama chombo cha kudhibiti fikra

Mwanakupona hapa anahimiza utumishi wa mke kwa mume wake kama sehemu ya mafundisho ya dini. Anamfunza bintiye kuwa mtiifu kwa mumewe na kufuata maadili ya Kiislamu. Kwa mtazamo wa Gramsci (1985), hizi ni fikra za uongo zinazopandikizwa na tabaka tawala ili kudumisha hali ya mambo ilivyo. Utenzi huu unaonyesha kuwa Mwanakupona amepokea na kusambaza imani hizi, ambazo zinahakikisha mwanamke anaendelea kuwa chini ya mamlaka ya mwanaume kwa kuamini kuwa hiyo ndiyo nafasi yake ya asili, jambo ambalo si kweli kiasili bali ni zao la mfumo wa kiitikadi wa wakati huo. Kwa hivyo, utii wa Mwanakupona hauwasilishwi kama chaguo la hiari tu, bali kama wajibu wa lazima wa kijamii na kidini, jambo linalodhihirisha kuwa mtunzi ameathiriwa kwa kiwango kikubwa na dini.

Mwanakupona anaendelea kumtolea bintiye mfano wa jinsi walivyoishi kwa amani na mume wake. Hii inaweza kutafsiriwa kwamba mama katika nyumba ana jukumu kubwa la kufunza maadili kwa wanafamilia (Mwinyi, 2020). Mtunzi anamtolea mfano wa vile ndoa

yao ilijaa furaha bila ugomvi wowote katika ubeti wa 51 na 55. Kulingana na Karisa na Mwinyifaki (2017), mawaidha ya Mwanakupona kwa bintiye kuhusu maisha ya ndoa wanasema kuwa yanatokana na mafundisho ya Kurani Tukufu na Sunnah. Wanaendelea kuwa katika Kurani Tukufu bibi zake Mtume Muhammad wanachukuliwa kama mfano wa kuigwa na wanawake hasa kuhusu jinsi wanavyotakikana kuwa watiifu kwa waume zao.

Maudhui haya pia yanadhihirika katika ubeti wa 66, 67 na 68. Katika ubeti 66 Mwanakupona anasema kuwa amefikisha maneno yake tamati. Anamwambia bintiye kwa pamoja wamuombe Mungu ili aweze kupokea dua la mamake (Mwanakupona), anaongeza kuwa yote ambayo amenena, mwanadamu ni kiumbe dhaifu. Mola ndiye awezaye kutenda makuu katika ubeti 67. Vilevile, anamwambia bintiye amfuate Mungu katika ubeti wa 68. Ili ampe msaada wa aina yoyote. Katika ubeti wa 69 anaongeza kuwa;

*...Yote nimezoyanena,*
*Rabbi taqabali minna,*
*Na yasalieo tena,*
*Rabbi Mola nitendea...* (Mwanakupona 1858)

Hapa anaomba Mungu Mola aweze kuhifadhi aliyonena yote na yaliyosalia. Mwisho anaomba Mungu awe naye. Katika yale maombi, anaongeza kuwa Mungu aweke wana wake, na Ndugu yake mdogo (mnuna). Yakue yao majina. Ikiwa na maana ya kuwa waweze kuishi kwa miaka mirefu na familia yao kuwa pana. Anaongeza katika ubeti wa 71 kuwa Mungu awaweke wana wa ndugu zake. Katika ubeti wa 72 pia anaiombea jamii ya Islamu. Anasema Mola awarehemu waislamu wote. Pia awape matakwa yao ili nyoyo zao ziweze kufurahia. Maombi haya yanaendelea hadi ukurasa 100.

Mwanakupona anahitimisha utenzi wake kwa kutaja jina la Mungu na kuomba baraka zake.

Katika ubeti 101 anamuomba Mungu arahisishe mambo ili wapate baraka za nabii na wafuasi wa mtume Muhamadi. Anataja katika mshororo wa nne kuwa hiyo ndiyo dini ambayo Mungu aliwateulia kama Waislamu. Katika ubeti 102 anaongeza kuwa anamtukuza Mungu. Hivyo, ni wazi kuwa utii wa Mwanakupona wa kufuata maudhui makuu yaliyotawala utunzi wa urasimi mkongwe ya dini, na kuzungumzia haya kwa upana ualimwathiri sana. Sababu Mwanakupona anamwambia bintiye ashike dini sana na atii mafunzo yake ili awe na maisha mema. Hivyo itikadi ya utiifu imechangia sana maudhui ya dini katika huu utenzi.

#### 3.2.1.2 Maudhui ya Utamaduni

Utamaduni umeelezwa na wataalam mbalimbali kama vile ; Mbaabu (1985), Adler (1997), Wamitila (2003), na Oatey (2008). Mbaabu (1985) anaakisi kuwa, utamaduni unahusu mila, asili, jadi na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia na maisha ya jamii kwa jumla. Adler (1997) naye anaifasiri dhana hii kama maarifa, imani, sanaa, maadili, sheria, desturi na mazoea ya kundi fulani la watu. Vilevile, Wamitila (2003) anasema kuwa utamaduni ni kama ukawaida wa kimaisha wa watu fulani. Neno hili huleta pamoja masuala ya kijamii ambayo huiwezesha jamii kujieleza na kujitambulisha pamoja na kufanya shughuli zao za kila siku.

Kwa mujibu wa Oatey (2008), utamaduni ni seti ya makisio na maadili, maelekezo ya maisha, desturi, sera na kanuni zinazotumika na kundi fulani la watu. Kanuni na desturi hizi huathiri tabia na mienendo ya wanajamii na kuwatofautisha na jamii zingine. Hivyo, utamaduni ni mfumo wa kimaisha wa watu fulani, wanavyoishi na wanavyoendeleza maisha yao. Huo mfumo unajumlisha imani, sanaa, maadili, mila, sheria na desturi.

Waswahili walikuwa na mila na desturi zao za jadi kuhusu mahusiano ya watu katika ndoa

na maisha kwa jumla, ambazo waliwafunza watoto wao. Mafunzo hayo kwa watoto wa kike haswa yalifanyika katika unyago, ngao na masimulizi mengine. Pia, yaliendelezwa katika matendo ya kimila ya kila siku. Vilevile, tunapata Mwanakupona akiutunga utenzi huu kwa madhumuni ya kumpa bintiye mawaidha. Haya ni kama ifuatavo;

Utamaduni unajitokeza pale Mwanakupona anampa bintiye ushauri wa jinsi ya kuwa kutangamana na watu. Haya ni mawaidha ambayo yalijikita katika jinsi Binti Mattaka atakavyofanya yeye mwenyewe ili kuwa mtu wa kupendeka na kutangamana na watu bila ugomvi. Katika ubeti 13 anamwambia awe na adabu. Akinena anene yanayofaa. Anaongeza kuwa bintiye awe mtu wa kupendeka. Anahitimisha katika mishororo wa nne kuwa akule anapopewa na anapokaribishwa. Katika ubeti 14, pia Mwanakupona anamshauri bintiye awe mtu wa kuaminika. Analoambiwa alikamilishe. Vilevile, ajitenge na watu waovu wasioshika haki na asiandamane na wajinga njiani. Katika ubeti 15 anaongeza kuwa awe mtu wa kunyenyekea mbele ya matajiri. Katika jamii hii, watu wa tabaka la juu walipewa heshima. Ndiposa Mwanakupona anamwambia bintiye kuwa anapotangamana na matajiri, anapaswa kuwanyenyekea. Mwanakupona katika ubeti 16 anaendelea kumshauri bintiye kuwa awaonapo matajiri awainukie na moyo uliofurahia. Kisha awaonyeshe njia wanapokwenda. Katika ubeti 17 Mwanakupona anaendelea kumshauri bintiye kuwa awe mtu mwadilifu. Anamwambia ajifanye mcheshi na anene kwa maneno yasioudhi au kudanganya. Pia asifanye ubishi ili watu wasije wakamchukia. Kando na hayo, anaongeza katika ubeti 18 kuwa Mattaka anene na watu kwa mzaha. Anamwambia heri kujinyamazia na asiamini mambo asiyoona na asisengenyane.

Maudhui haya pia yanajitokeza katika ubeti 20. Hapa Mwanakupona anamfunza mazoea yaliyoko ya migao iliyoko katika jamii. Haya ni kupitia pale anamwambia bintiye

asiandamane na watumwa. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa jamii husika ilikuwa na tabaka la juu lililosheheni nyenzo za uzalishaji mali na tabaka la chini ambalo lilisheni wafanyikazi ambao ni watumwa. Binti Mattaka inadhihirika kuwa alikuwa katika tabaka la juu. Mwanakupona anamfunza bintiye kutoandamana na watumwa ili aelewe mazoea yaliyokuwa katika jamii yake ili naye bintiye ayafahamu. Hivyo, tunapata Mwanakupona akimwambia kuwa aandamane nao tu wakati wa kazi. Akiandamana nao watampotosha. Hapa Mtunzi aliathirika anayapitisha mambo anayaona kuwa ya kawaida katika jamii ambayo hata yeye alipata yakiendelezwa. Hivyo anadhihirisha utii wa utamaduni ambao unapelea maudhui ya utamaduni.

Pia, katika ubeti wa 21 anaongeza asiandamane na wajinga wasiojua kujichunga. Tunapata mtunzi akiwasawiri kama viumbe wasio haya katika mishororo wa tatu.

*...Sandamane na wainga*
*Wasyua kuitunga*
*Ziumbe wasio tanga*
*Wala kuwaqurubia...* (Mwanakupona 1858)

Anahitiisha sehemu hiyo kwa kumwambia katika ubeti wa 22 kuwa afuate hayo aliyomwambia ili aepuke ya ahera na dunia. Hivyo, atapata utulivu. Mawaidha haya yanadhihirisha kuwa ile migao ya kijamii ilikuwemo wakati wa Mwanakuona. Ndio maana anampa wosia bintiye kuhusu haya ili aweze kuyafahamu pia yeye. Mawaidha haya yalielekea kuwa mazoea yaliyopitishwa kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine ndiposa mtunzi anayapokea na kuyapitisha kwa bintiye kwa hiari tu kulazimishwa na yeyote. Hivyo itikadi ya utiifu inapelekea Mwanakupona kutii ule utamaduni na kuupitisha ili bintiye aujue ndiposa awe na maisha mema.

Kando na hayo, utiifu wa utamaduni unajitokeza pale Mwanakupona anamfunza bintiye masuala ya kazi. Anamwambia apende kazi. Hivyo, kazi ilikuwa muhimu katika utamaduni wa Waswahili kwani mtu hakupaswa kuzembea. Katika utenzi huu, hili halijajitokeza sana labda kwa kuwa Mwana Hashima ni mtoto wa tabaka tawala mwenye watumwa na watumishi wa kumhudumia. Hivyo halazimiki kufanyia kazi ngumu (Mulokozi, 1999). Lakini katika utenzi huu kipengele cha kazi kinajitokeza nyumbani katika asasi ya ndoa. Haya yanajitokeza katika ubeti 37 ufuatavyo;

...*Mwanangu siwe mkoo,*

*Tenda kama uonao,*

*Kupea na kosha choo,*

*Sidharau mara moya*... (Mwanakupona 1858)

Hapa mtunzi anamshauri bintiye afanye kazi haswa katika ndoa yake. Anamwambia asiwe mvivu kwa kutenda anayoyaona. Yaani, kutenda yale aliyoona mama yake akiyatenda ili kutunza ndoa yake. Pia, kutenda ambayo anayoyaona yanafaa ili kudumisha ndoa yake. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa hata Mwanakupona mwenyewe alifanya kazi. Hivyo, utamaduni wa Waswahili haukumruhusu mtu kuwa mvivu (Mulokozi,1999). Mwanakupona hapa aliathiriwa na utii kwa kushughulikia utamaduni wa kufanya kai katika ndoa ili kuitunza. Mtunzi anapokea ile imani ya kazi na anaipitisha kwa bintiye bila kulaziishwa na yeyote.

Utamaduni pia unapatikana kupitia mafunzo ya usafi. Kulingana na Mulokozi (1999), jambo la uzazi ni jambo jingine la mafunzo ya Kiafrika ambalo hutiliwa mkazo katika unyago. Maadili ya dini ya Kiislamu tunapata hayaelezwi waziwazi katika utenzi huu, lakini tunapata Mwanakupona akiyashughulikia. Haya yanadhihirika kupitia mafunzo

kuhusu usafi na kujipamba ili kumpokea mume katika hali safi itakayomvutia. Kwa mujibu wa Khamis (2016), mwanamke wa Pwani ana utamaduni wake wa kujipodoa na kujipamba kwa kutumia vitu mbalimbali kama vile mapambo ya fedha na dhahabu kwa sura ya vidani, pete, hereni, bangili na vikuku. Inaweza kusemwa kuwa, usafi na umaridadi ni kipengele muhimu katika maisha ya mwanamke wa Pwani. Katika ubeti 37, Mwanakupona anamshauri Binti Mattaka awe msafi na asipuuze usafi. Anaendelea katika ubeti 38 kumwambia aweze kuoga na kujisugua. Nywele zake azifunge pia. Aweze kutia firashani kwenye matandiko pia.

Vilevile, katika ubeti 39, anaongeza kuwa bintiye apambe libasi yake. Yaani, avae na pia kujipamba vizuri kila siku. Ili aweze kukaa kama ni siku ya arusi yake kila wakati. Katika mshororo wa tatu anamwambia atie kugesi mguuni na aeke makoa mikononi. Haya ni mapambo ambayo anamwmabia ayavae ili amvutie mume wake. Anasema katika ubeti 40 kuwa pia avae kidani na kibano katika shingo na apake marashi na daiia. Hii ni aina ya poda yenye harufu nzuri. Katika ubeti wa 41 anaongeza kuwa bintiye asikose kuvaa pete vidoleni, kupaka hina kwenye kucha za mikoni na uwa na wanda machoni na nyusi za macho. Haya yote, yanatupa taswira ya mwanamke Muislamu jinsi anavyokaa (Khamis, 2016). Hivyo, Mwanakupona anamshauri bintiye jinsi anavyopaswa kuvaa na kujiremba ili awe mwanamke Mswahili kamili na pia aweze kumvutia mume wake. Haya yanaonyesha utiifu wa Mwanakupona wa utamaduni unaomhitaji mwanamke kuwa msafi. Isitoshe, jambo la uzazi linajitokeza pia pale Mwanakupona anamshauri bintiye kumhudumia mume wake kitandani na kutomtosheleza chochote atakachohitaji katika ubeti 29. Anamwambia katika ubeti huu kuwa akae na mume wake kwa amani. Analotaka mume amtimizie. Asibishane naye kamwe kwani akishindana naye ataumia. Kutokana na

hayo, mwanakupona anamfunza Binti Mattaka namna ya kudumisha amani katika ndoa. Anaongeza katika ubeti 47 kuwa anapoondoka nyumbani, binti arudi kwa upesi ili akae na mume wake. Amtengenezee matandiko mumewe ili wapate mahali pa kulalia. Vilevile, anaongeza kuwa wakilala asijitenge na mumewe. Bali, amkaribie. Pia, ampapase na kumpepea usiku na anapoanza kusinzia asimuondoe. Haya yanapatikana katika ubeti 31. Mtunzi anasema;

.... *Kilala sikukuse,*

*Mwegeme umpapase,*

*Na upepo asikose,*

*Mtu wa kumpepea*... (Mwanakupona 1858)

Mafunzo ya aina hii yanaelekezwa kwenye jambo la uzazi, ambalo katika mila za Waafrika wengi, ndio lengo lao la mafunzo ya ungago na jado (Mulokozi, 1999). Kutokana na hayo, tulipata kuwa Mwanakupona alitaka kumfunza bintiye yale mafunzo ili aweze kutunza suala la uzazi na pia kudumisha ndoa yake kwa hiari yake. Na hakumwambia yale akikusudia kumnyanyasa mwanamke bali ni mazoea ambayo ni ya kawaida katika jamii ambayo yanapaswa kufuatwa. Hivyo itikadi ya utiifu ilipatikana kumwongoza mtunzi hapa. Jambo jingine la mila na desturi zinazolandana na mila za Kiafrika ni namna ya kuishi bila ugomvi ndani ya nyumba. Kulingana na Mulokozi (1999), utenzi huu unamfunza mwanamke mbinu za kujinusuru katika ndoa na kuepuka ugomvi ndani ya ndoa. Kupitia haya mwanamke anapewa jukumu la kusimamisha ndoa yake. Tunapata katika ubeti wa 22 na 23 Mwanakupona akisema kuwa kumheshimu mume ni miongoni mwa radhi tano za jamii hiii. Hivyo, kumheshimu mume lilikuwa jambo muhimu katika utamaduni wa Waswahili. Mwanakupona tunapata akimwambia bintiye amtii mume wake. Anasema

katika ubeti wa 28 kuwa;

*...Keti naye kwa adabu*

*Usimtie ghadhabu*

*Akinena simjibu,*

*Itahidi kunyamaa...* (Mwanakupona 1858)

Anaongeza katika ubeti wa 29 kuwa bintiye akae na mume wake kwa amani. Analotaka mumewe bintiye asimkataze. Asibishane naye pia kwani akishindana na mume wake ataumia yeye mwenyewe. Hapa anaarifiwa kutojibizana au kushindana na mume. Pia, akitoka mume wake, aagane naye vizuri. Akiingia pia ampokee kwa furaha (ubeti 30). Kulingana na Mulokozi (1999), watetezi wa haki za wanawake wanasema kuwa hizi ni mbinu za kumdhalilisha mwanamke. Lakini Mwanakupona haoni yale majukumu kama yanayomkandamiza mwanamke bali ni tamaduni zinazostahili kufuatwa. Utiifu wake unamfanya kuona hayo kama ukawaida na anapitisha ule utamaduni kwa hiari yake.

**3.2.1.3 Maudhui ya Uhusiano wa Wanajamii**

Jambo jingine ni jinsi ya kudumisha amani na wanajamii. Maudhui yalijitokeza pale ambapo Mwanakupona anampa mawaidha kuhusu jinsi ya kutangamana na wanajamii ili kuepuka mikwaruzano na ugomvi. Haya yamo kutoka ubeti 57 hadi 64. Katika ubeti 57 mtunzi anasema;

*...Mausio ya mvuli*

*Allah Allah Yaamili*

*Na nduguzo na ahali*

*Wapende na kuusia...* (Mwanakupona 1858)

Ni dhahiri katika ubeti huu kuwa Mwanakupona anamshauri bintiye ashirikiane na

wanaohusiana naye kinasaba. Hizi ni mila za jamii husika na Mwanakupona anadhihirisha utii kwa kuzizungumzia katia wosia wake na kuzipitisha kwa kizazi cha bintiye.

Binti Mataka pia anaambiwa na mamake kuwa ashirikiane na wandani wake. Mwanakupona anasema kuwa hao wandani wakimwalika asikatae wito. Pia, wakimwandalia andaa chakula, akile bila maringo wala madharau ya aina yoyote. Hapa Mwanakupona anamfunza bintiye jinsi ya kuendeleza mahusiano bora na marafiki katika jamii. Jamii husika ilipaswa kuwa yenye amani na Mwanakupona tunapata akidhihirisha utii wa kanuni hizo. Mawaidha haya yanapatikana kutoka ubeti 58 hadi 60.

Mwanakupona anaendelea kumshauri bintiye amsaidie mtu anayetarajia msaada wake. Haya yanajitokeza kutoka beti za 61 hadi 64. Katika beti hizo, Mwanakupona anamtahadharisha bintiye asije akawabagua na kuwadharau yeyote kwani huenda atahitaji msaada wao pia siku moja siku moja. Ingawa binti huyu anashauriwa kuwapenda watu wote kwa usawa, anaonywa kuwa na uhusiano wa kindani na yeyote ambaye anaweza kumpotosha. Awe mwanamke au mwanaume, maskini au tajiri, mtumwa au kabaili.

Mwanakupona anamwambia bintiye katika ubeti 14 kuwa awe mtu wa kuaminika, asiwe mtu muovu asioishi kwa haki na asiandamane na mtu wa aina hio njiani. Ubeti 21 anaendelea kusema kuwa asiandamane na wajinga wasiojua kujichunga na asiandamane na viumbe wasio haya. Bintiye hapa anashauriwa kuwaepuka watu wasiojua yanayoendelea katika jamii yao. Anawarejelea watu hao kama wajinga katika ubeti 21. Hapa Mwanakupona anathihirisha utii wa utamaduni hasa namna ya kuishi na wanajamii na anayachagua maudhui haya ili kumfanya bintiye aujue namna utamaduni unavyomtaka atangamane na wanajamii wenzake.

Pia, anamshauri kuwa anapokaribishwa ale. Haya yanajitokeza katika ubeti wa 59 na 60.

Katika ubeti 59 mtunzi anamshauri bintiye kuwa chakula kinapoandikwa, hana budi kuanza kukila anapokaribishwa kukila. Anaongeza katika ubeti 60 kuwa bintiye asifanye kiburi iwapo hajashiba. Asije akasema kuwa hajashiba. Anamshauri ajifanye kuwa ameshiba iwapo wanataka kuondoa vyombo mezani. Kutokana na hilo, mtunzi anampa bintiye mawaidha ya jinsi ya kutangamana na wanajamii, haswa, katika masuala yanayohusu vyakula na makaribisho na majirani.

Vilevile, Mwanakupona anamwambia Binti Mattaka asifanye urafiki na watu asiowaamini. Haya yanajitokeza katika ubeti 61 na 62. Mtunzi katika ubeti 61 anaendelea kumshauri kuwa watu wote waumini bintiye awafanye wendani. Hapa mtunzi anamwambia kuwa afanye urafiki na watu wanaoamini Mungu. Anamwambia bintiye katika mshororo wa tatu kuwa asipende wasaliti au wagomvi. Anamwambia anapaswa kuwaepuka. Katika ubeti 62 vilevile anaongeza kuwa bintiye asipende wenye kupenda utukufu wa haiba. Pia, wenye kupenda utukufu wa mali na wenye kujisifia.

Isitoshe, anamshauri kupenda watu wote katika ubeti 63. Mwanakupona anamshauri Binti Mattaka kuwa apende anayempenda. Anayemkataa asimchukie. katika 64 anazungumzia suala la kusaidiana. Mtunzi anasema kuwa ajapo mwenye shida bintiye amsaidie. Anaongeza kuwa asimuulize maswali mengi mwenye kutaka usaidizi kwani atamfukuza. Bali awe hodari na kumtendea wema. Hili lilidhihirisha uhusiano uliokuwepo baina ya wanajamii kwani Mwanakupona alitaka bintiye atangamane na wanajamii kwa amani. Haya ni kwa kushauriwa kuhusiana na atakayempenda na kumsaidia. Vilevile anashauriwa asichukiane. Kutokana na hilo ni ilibainika kuwa jamii husika iliishi kwa amani na kama watu wamoja.

### 3.2.2 Itikadi ya Taasubi Ya Kiume pamoja na Itikadi ya Ukawaida Zilivyopelekea Uwasilishaji wa Maudhui

#### 3.2.2.1 Ndoa na familia

Majukumu ya bibi kwa mume wake yamesisitizwa kwa upana katika utenzi huu. Rodney (1972) anasema kuwa, jukumu la wanajamii wengi haswa za Kiafrika zimepangwa kwa kufuata uana na pia utamaduni. Jukumu la mwanamke kama anavyosawiriwa katika huu ni la mwanamke katika jamii husika katika mazingira na utamaduni wa Waswahili wa karne ya kumi na tisa. Kuambatana na mila na desturi za Kiafrika, ni jukumu la mke kumlea mtoto wa kike kwa njia bora. Ndungo (1985) anaafikiana na mawazo ya Kenyatta (1938) wanapodai kuwa mafunzo ya aina hii katika jamii ya Wakikuyu hutolewa wakati wa tohara katika kitabu chake cha Facing Mount Kenya. Mafunzo ya aina hii huthaminiwa sana na hufanywa katika mazingira ya unyagoni katika jamii ya Waswahili. Pia, utamaduni wa Waswahili hushikilia kuwa mtoto wa kike mwenye tabia njema huiletea aila yake sifa nzuri (Wanderi, 2021). Kwa hiyo, mwanawake Mswahili anapaswa kuolewa na mwanamume aliye katika kufu yake.

Kwa mujibu wa Wanderi (2021), wakati Mwanakupona alipotunga mawaidha haya, bintiye alikuwa na umri kuolewa kulingana mila za Waswahili. Mtunzi kama mzawa wa jamii inayozingatia ndoa ya kufu amepelekea pia kutuchorea mume wa binti yake atakuwa mume wa aina gani. Anatajaria kuwa huyo mume atashika dini na kufuata tamaduni za Waswahili. Huyo mume basi hataona ajabu na aibu kwa kutendewa mambo hayo, kwa kuwa anayafahamu tangu utotoni na anayaona kuwa ya kawaida na yamekubalika katika jamii. Hivyo Mtunzi anaoneka kutawaliwa na taasubi ya kiume kwani haoni hayo mawazo kama yanayoifinyilia jinsia ya kike na pia kwa kuona hizo fikra kama za kawaida na

zinazokubalika katika jamii.

Msichana Muislamu haruhusiwi kuolewa na mume asiye Mwislamu isipokuwa pale ambapo mume huyo yuko tayari kusilimishwa. Katika kurani sura ya 60 aya ya 10, panaelezwa: '*Enyi mlioamini! Watapokujieni wanawake Waislamu wanaohama, basi wafanyieni mtihani Yao. Mkiona kuwa wao ni Waislamu kweli basi msiwarudishe (Kwao Makka) kwa makafiri. (Wanawake) hawa si halali kwa hao (Wanaume makafiri), wala wao (wanaume makafiri) si halali kwao: na warudishieni (waume zao) mali zao, (mahari) walizotoa. Wala kwenu si hatia kuwaoa, ikiwa mtawapa mahari yao.*' Kufu hii inamaanisha kuwa lazima msichana na mvulana wanaooana wawe watu wanaotoshana kijamii. Kinachozingatiwa katika kutoshana huku si tabaka tu bali pia tabia na malezi.

Mwanakupona anautunga huu utenzi ili kumpa bintiye mawaidha ya kutunza ndoa yake. Tunapata kuwa utenzi umesheheni mawaidha katika sehemu kubwa. Anamwambia bintiye akaribie ili aweze kusikiliza wosia na pengine aweze kuuzingatia. Anaongeza kuwa ameshikwa na maradhi katika ubeti wa pili. Maradhi yale yamekaa mwaka na ndio maana hakupata kutamka. Hivyo, anampa bintiye wasia wakati ule. Kulingana na Mulokozi (1999), ni dhahiri kwamba Mwanakupona aliutunga utenzi wake wa wasia kwa bintiye kwa misingi ya maisha ya ndoa. Katika ubeti wa 11, anasema kuwa bintiye atakaposhika, yaani kutii ule wosia wake, hatasumbuka. Hivyo duniani ataishi vyema na ahera ataingia.

Katika ubeti wa 22 na 23, mtunzi anamshauri bintiye amheshimu mumewe. Mwanakupona anasema kuwa hilo ni miongoni mwa radhi tano za Waislamu. Kutokana na lile ataweza kupata utulivu katika ubeti wa 22. Hapa, dini ya Kiislamu inaamini kuwa, mpangilio wa hadhi na radhi uliopangwa ambao ni Mungu, Mtume, baba na mama na mwishowe mume (Wandera, 2021). Mwanamke hapa anatakiwa kuwamtiifu kwa Mungu wake na mafunzo

yake, kisha mtume. Mzazi wa kiume amepewa nafasi ya tatu na nne ni mzazi wa kike na nafasi ya nne ni ya mume. Katika hali hii, mzazi wa kike ana mamlaka juu ya mtoto wake wa kike ili kumfunza masuala ya utii wa mume. Hapa itikadi ya taasubi ya kiume tunaona ikiendelezwa na mtunzi na pia dini. Tunaona kuwa mwanamume hapa amepewa nafasi ya juu kuliko mwanamke na mwanamke anaambiwa amheshimu na awajibikie mumewe. Kutokana na hilo ni dhahiri kuwa mtunzi ametawaliwa na itikadi inayoendeleza ubabedume katika jamii husika na pia anayafanya anayoyazumgumza kuwa ya kawaida na yanayokubalika katika jamii, kwa usaidizi wa dini. Dini hapa ilitumika na mtunzi kumdunisha mwanamke.

...Naawe radhu mumeo
Siku zote mkaao
Siku mukhitariwao
Awe radhi mekuwea... (Mwanakupona 1858)

Katika ubeti wa 24 tunapata akiorodhesha mambo ambayo bintiye anapaswa kufuata ili kudumisha amani na mumewe na kutunza ndoa yake. Anaongeza katika ubeti wa 25 na 26 kuwa bintiye atafute radhi zake mume wake. Mwanakupona anamshauri bintiye amheshimu mume wake. Hii ni sababu ndiye atakayefanya uamuzi kuhusu mahali ataenda baada ya kufa. Mumewe ataulizwa analotaka na hilo ndilo litatendwa. Na kupitia hayo, ndivyo atakavyo pata njia. Hapa kuna itikadi ya taasubi ya kiume. Mtunzi anampa bintiye mawaidha ya kutunza ndoa yake ilhali hataji katika utenzi wake kuwa mume na mke ni watu wamoja na wanapaswa kuishi kwa furaha bila kuikandamiza jinsia moja (Gibbe, 1993). Jinsia ya kike imetwikwa jukumu la kutunza ndoa peke yake na haya yanaonyesha kuwa mtunzi hakuona anayoyasema kama yanakandamiza jinsia ya kike, yeye akiwemo.

Bali anapitisha zile imani kwa bintiye na kuziona kama za kawaida tu.

Katika ubeti 28 hadi 36 anaendelea kumshauri amtii mume wake. Anamwambia aketi na mume wake kwa adabu katika ubeti 28. Pia, asimtie mumewe ghadhabu. Akinena mume, Binti Mattaka asimjibu. Analopaswa kufanyia ni kujifunza na kujitahidi kunyamaa. Katika ubeti wa 29 anaongeza kuwa; akae na mumewe kwa imani. Atakalo mumewe asimkataze. Asijaribu kubishana naye kwani akishindana naye ataumia. Vilevile, katika ubeti wa 30 tunapata akimshauri bintiye anastahili kuagana na mume wake vizuri anapoamua kuondoka. Pia, akiingia asijitenge na mume wake. Akilala, anaongeza kuwa Binti mattaka asijitenge na mume wake. Anaambiwa amkaribie.

Katika ubeti wa 31, anamwambia pia kuwa simwondoe wala asinene kwa mayowe. Anastahili kukaa naye hapo. Katika huo ubeti pia tunapata Mwanakupona akimshauri bintiye aketi naye hadi mume wake akipata usingizi. Vilevile, anamwambia bintiye asichelewe kumpa maakuli katika ubeti wa 33. Mwisho, Binti Mattaka autunze mwili wa mume wake. Hapa taasubi ya kiume inajitokeza kwani mume anaweza kuutunza mwili wake yeye mwenyewe sababu yeye ni binadamu tu kama mwanamke lakini mtunzi anatwika jinsia ya kike tu lile jukumu. Anayoyasema kuhusiana na ndoa katika utenzi wake anayaona kama masuala ya kawaida ilhali yanamdhalilisha mwanamke. Mulokozi (1999), anasema kuwa mawazo ya Mwanakupona yanatokana na vyanzo vinne. Anaorodhesha kwanza ni mafundisho ya dini ya Kiislamu kama yanavyoelekezwa katika Kurani na Hadithi na itabu vingine. Pili, yanatokana na mila, desturi na imani za kitambo za Waswahili. Tatu, yanatokana na mila na desturi za Waarabu zinazofuatwa na baadhi ya wenyeji wa pwani waliosilimu. Nne, aliongozwa pakubwa na imani, desturi, mtazamo na uzoefu wa tabaka tawala la pwani. Haya yote yanaambatana na kupelekea fikra, uzoefu,

elimu na mtazamo wa Mwanakupona uliosheheni ubabedume, ambao yeye mwenyewe anaona kuwa ni ukawadia bali hakuona kuwa unamkandamiza Mwanamke mwenzake.

Kando na hayo, itikadi hizi zimepelekea kuwepo kwa maudhui haya ya ndoa katika ubeti 34. Hapa Mwanakupona anampa bintiye jukumu la kumnadhifisha mumewe. Anamshauri amuoshe na kumnadhifisha. Anasema;

...*Munyoe mpatitile*,

*Sharafa umtengeneze*,

*Na udi umfukize*,

*Bukuata ashia*... (Mwanakupona 1858)

Mtunzi anamwambia bintiye amtengeneze mumewe asubuhi na jioni. Anaongeza katika ubeti wa 35 kuwa amtunze kama kijana asiyejua kunena. Ikiwa na maana ya kijana mchanga. Vilevile, aangalie chote kinachotoka na kuingia katika mazingira ya mumewe. Hapa, binti anapewa jukumu la kuwa mlinzi wa mumewe. Anashauriwa amtunze na kumfanyia usafi. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa Mwanakupona anamfunza Binti Mattaka namna ya kutunza ndoa yake kwa kumchunga mumewe kama kijana. Tunapata katika ubeti wa 36 akiongeza kuwa ampumbaze kwa haya yote hadi mume anapomfanyia chochote kibaya, asinene naye wala kulipisha kisasi. Bali anashauriwa kuwa Mungu ndiye atakayemlipia. Mawazo ya kibabedume ya mtunzi yanamfanya mwanaume kama kiumbe dhaifu na wapumbavu kama ilivyojadiliwa na Mbele (1985). Kama ilivyojadiliwa na Mulokozi (1999), mbele ni miongoni mwa wanataaluma wa tapo la tatu lililokiri kuwa mwanamume anadunishwa katika utenzi huu na kuchorwa na mtu mdhaifu ambaye hawezi jifanyia chochote ilhali yeye ni mtu mzima.  Hivyo, mwanamke anapewa majukumu yanayomdhulumu. Mwanakupona anafasiri haya yote kama ukawaida, na alipitisha fikra

potofu za kibabedume zilizozidi kumnyanyasa mwanamke.

Isitoshe utii katika ndoa na familia pia unajitokeza pale Mwanakupona anamshauri bintiye jinsi ya kuendeleza uhusiano bora na mumewe katika ndoa kutoka ubeti wa 48 hadi 50. Hapa Mwanakupona anaanza katika ubeti wa 48 kwa kumshauri bintiye amtukuze mume wake. Haya ni ili sifa zake zienee. Wala asimlazimishe asichoweza kutoa. Kutokana na huo ubeti Binti Mattaka anashauriwa kunena sifa bora za mumewe ili watu au jamii ijue kuwa ndoa yao ni njema. Haya pia yanajitokeza katika ubeti 96. Hapa mtunzi anasema kuwa kila mahali ambapo bintiye aendako anapaswa kutangaza sifa zake meme kwa heshima na uzuri. Katika ubeti wa 49 Mwanakupona pia anaongeza kuwa mume anachompa apokee na afurahie. Asilolitenda hana haja kumwambia kwani hayo yataharibu uhusiano baina yake na mume wake kwani wataanza ugomvi baina yao. Anahitimisha sehemu ile katka ubeti wa 50 kwa kuongeza kuwa bintiye aonapo uso wa mume wake, atabasamu. Vilevile, ashike analoambwa na mumewe. Anamwambia asijaribu kuinua ulimi. Hapa ubabedume unatawala mawazo ya Mwanakupona kwani hajataja mahali popote ambapo mwanamme anampokea na kumfurahia mke wake, wala kunena sifa zake bora. Bali mwanamume tu ndiye anafanyiwa hayo yote na kuchorwa kama kiumbe kinachofaa kuheshimika, kufurahiwa na chenye mamlaka ya juu kuliko mwanamke.

Mwanakupona anazidi kumwambia bintiye auchukue mfano halisi wa mama yake na baba yake, ambao walioana kwa miaka mingi. Mume wake hakumfanyia ovu wa aina yoyote wala naye hakutenda chochote kibaya kwake katika ubeti wa 51 hadi 53. Mwanakupona anasema kuwa waliishi kwa furaha na vicheko. Kulingana na Karisa na Mwinyifaki (2017), mawaidha ya Mwanakupona kwa bintiye kuhusu maisha ya ndoa unatokana na mafundisho ya Kurani Tukufu na Sunnah. Katika ubeti wa 54 anaongeza kuwa mauti yalipotokea baina

yao, waliomba msamaha baina yao. Katika ubeti wa 55 anasema kuwa kutoka kitambo hadi leo hajanyamazisha kilio anapokumbuka jinsi walivyozoeana na mume wake. Hapa Mwanakupona anamtolea bintinye mfano wa ndoa yake mwenyewe. Anaeleza maisha ya ndoa na mume wake na matumaini kuwa bintiye ataufuatilia ule mkondo. Anayachora hayo yote kama mazoea ambayo yamekubalika katika jamii, kiasi ya kumtolea bintiye mfano wa ndoa yake, ili kuyafanya yazame akilini mwake na kuyaendeleza katika ndoa yake.

**3.2.2.2 Maudhui ya Utamaduni**

Mtunzi anaonekana kumshauri binti yake na wanawake kwa jumla katika jamii yake. Anamwambia ahakikishe kuwa kuna uhusiano mzuri na wanajamii wengine kwa kufuatia mahitaji utamaduni wa jamii yake. Tunapata kuwa jamii ya mtunzi ina migao ya kitabaka, kwa hivyo anamshauri binti yake pia kuhusu maingiliano yake na watu wa tabaka zote (Wandera, 1996). Haya yanamfunza Mattaka mazoea yaliyoko katika jamii ili aepuke shida na ugomvi. Yale mazoea ya utabaka anayapitisha kwa hiari yake kwani anayaona kama mazoefu ya kawaida. Kwa matajiri, bintiye anaambiwa anyenyekee mbele yao kwani unyenyekevu siku zote hutoa sura nzuri kwa watu. Mtunzi anamwambia pia awaheshimu wanajamii wakati wote, asidakie maneno ovyoovyo, na asibishana ovyo bila sababu. Mtunzi hapa hawatenganishi wanajamii hawa kwa misingi ya uana. Bali anamshauri binti awe mtiifu kwa watu wote wa tabaka la juu: wake kwa waume. Hapa mwanamke wa tabaka la juu anapewa heshima sawa na mwanamume. Ukawaida na ukubalifu wa kuwatii walio kwenye tabaka la juu, wake na waume lilipelekea mtunzi kuendeleza zile fikra na imani kwa bintiye. Vilevile, mwanamke wa tabaka la juu anaheshimiwa ila wa tabaka la chini haeshimiwi. Jambo hili pia linaendeleza taasubi ya kiume katika jamii haswa kwa walio kwenye tabaka la chini (ubeti za 15 hadi 18).

Mwanakupona anaendelea kumwambia bintiye asitangamane na watumwa. Hawa watumwa walijumuisha tabaka la chini. Watumwa hawa ni wanaume na wanawake kwa pamoja. Kwa hivyo huyu binti hakukanywa kutotangamana na watumwa wa kiume pekee, ilhali ashirikiane na wale wa kike (Ndungo, 1985). Haya mawaidha yanajitokeza katika ubeti 20:

*Sitangane na watumwa*
*illa mwida wa khuduma*
*watakuvutia tama*
*la buda nimekwambia* (Mwanakupona 1858, ubeti 20)

Maelezo ya ubeti huu yanaonyesha mtazamo na fikra walizokuwa nazo watu wa tabaka la juu kuwa hawakutangamana na masikini ila wakati walipokuwa wanahudumiwa. Mwanakupona anamwambia bintiye kuwa asitangamane na watumwa ila wakati wa kazi. Anaendelea kunena kuwa watampotosha bintiye. Hizi ni kaida ambazo jamii ya Mwanakupona iliziona kuwa za kawaida na zilikubalika na watu. Ndiposa mtunzi analihusisha katika wosia wake na alizipitisha kwa bintiye ili ziendelee kudumu. Ilhali hio mitazamo ilimkandamiza mwanamke tu.

#### 3.2.2.3 Maudhui ya Dini

Kwa mujibu wa Wandera (2021) tafiti nyingi kuhusu wanawake Waiislamu kama vile Maududi (1972) na Kateregga (1984), imebainika kuwa wale wanawake wamebobea katika uandishi ulioegemezwa kwa kipengele cha dini yao. Mfano bora zaidi hapa ni *Utenzi wa Mwanakupona*. Kupitia haya ni wazi kuwa dini ilitumika katika hizi tungo kama dira ya kuendeleza maisha ya Waislamu, haswa jinsia ya kike. Mtunzi katika ubeti 12 tunapata akisisitiza ubora wa dini kama mawaidha ya muhimu kwa mtoto wake: Anamwambia;

*...La kwanza kamata dini*

*Faradhi usiikhini*

*Na sunna ikimkini*

*Ni wajibu kuitiya...* (Mwanakupona 1858, ubeti 12)

Hapa mtunzi anamshauri bintiye aikamate dini na masuala yote yanayofungamana nayo. Pia, mtunzi anamwambia bintiye afuate na kufanya wajibu wake wote kama anavyokiri dini yao. Mwanakupona vilevile katika beti za 22 na 23 anaonyesha kuwa, katika urasimu wa madaraka na radhi katika dini ya Kiislamu. Huu ni ukawaida ambao umo katika dini hii na tunapata mtunzi akiupitisha kwa bintiye :

*...Mama pulika maneno*

*Kiumbe ni radhi tano*

*Ndipo apate usono*

*Wa akhera na duniya...* (Mwanakupona 1858, ubeti 22)

Kufuatia haya binti anawajibika kumheshimu mume ili apate maisha mema akhera na duniani. Haya yanaendeleza itikadi ya taasubi ya kiume kwani mwanamme amo katika radhi tano za dini ya Islam, na mke anaambiwa amheshimu na atapata maisha bora. Mtunzi anazidi kusema kuwa mume ndiye atakaye amua hatima ya mkewe. Kwa hivyo, dini hapa inampa mwanamume mamlaka ya juu kuliko mwanamke. Hizi ni kaida na fikra ambazo zinashusha nafasi ya mwanamke na zinapelekea mwanmake kuonekana kama kiume duni kuliko mwanamke. Hivyo itikadi ya taasubi ya kume na ule ukawaida wa dini kumpa mwanamume hadhi ya juu inaonekana kumsukuma mtunzi kushughulikia maudhui haya ya dini hapa.

Katika beti 13, 14 na 19, mtunzi anaendelea kumshauri bintiye afuate na kukamata

matakwa ya dini husika na afanye vitendo vyote vinayoambatana dini husika. Anamwambia awe na adabu nzuri, awe mnyenyekevu, asiwe mtu wa kuropokwa ovyo ovyo, asisengenye na pia asiandamane na wajinga na wasiotenda haki. Anaongeza pia kuwa awe na adabu na ulimi wa kunena yanayofaa na pia awe mtu wa kula anapopewa chakula na anapokaribishwa. Katika ubeti 14 anaendelea kumshauri awe mtu wa kuaminika, asiwe mtu muovu asioishi kwa haki na asiandamane na mtu wa aina hii njiani. Vilevile, katika ubeti 19 tunapata akimwambia kuwa asiwe mtu wa kuamini mambo asiyoyaona, atahadhari kusengenyana na asichanganyike na watu waovu. Mwanakupona anamwambia Binti Mataka kuwa akiyafuata maagizo hayo yote atakuwa mtu mwadilifu anayetenda haki kulingana na dini yake. Dini hapa inaonekana kuendeleza fikra na imani potofu zinazoegemea kwa jinsia moja tu badala ya mtunzi kuzungumia jinsia zote mbili zinavyofaa kuishi kwa umoja. Mwanakupona hapa anaonekana kuendeleza ubabedume kwa kumwambia bintiye ashikilie mafunzo ya dini na afanye mema yanayoambatana nayo badala ya kuwashauri wote, wake na waume.

Dini pia inapatikana katika beti 66 hadi 102. Beti hizi zinajumuisha maombi kwa Mungu (ubeti wa 6). Gibbe (1993: 35) anakadiria kuwa, asilimia 48.5 ya utenzi huu ni sala ya mwisho ya Mtunzi kwa Mungu.  Kama Mswahili na pia watunzi wa wakati wake, ameathiriwa mtunzi ameathirika sana na mitazamo ya kidini. Hii mitazmo tunapata kuwa ni mambo ambayo ni ya kawaida na yamekubalika na Waislamu na ndiposa Mwanakupona akaona ni bora ayapitishe kwa bintiye. Haya yanaafikiana na mawazo ya Bakari (1978) ya kuwa utenzi huu unasheheni mawaidha ya majukumu ya jinsia ya kike kwa waume wao, jamii yake na kwa Mola. Haya yanaonyesha uzito unaopewa dini husika.

Kwa vile msanii huyatoa maudhui yake kutoka kwa mazingira anamoishi, mtunzi hakuwa

na budi ila kushughulikia mambo aliyofahamu, kwa kuyaishi na kuyashuhudia katika maisha yake. Huu ni ukawaida ambao umepelekea kukubalika na jamii. Ndio maana pale ambapo vipengele vya dini, ndoa au tamaduni vinamkandamiza mwanamke, Mwanakupona aliona hayo yote kama tu wosia wakumsaidia bintiye kuwa na maisha bora yasioyokuwa na ugomvi, kuwa bibi bora kwa mumewe na kuepuka motoni. Bibi huyu angalikosa kufuata hayo, angalikuwa anasaliti jamii yake kwa kukiuka dini yake.

### 3.3 Ulinganishaji wa jinsi itikadi za watunzi zilivyopelekea uwasilishaji wa Mitindo vitofauti.

Katika sura hii tulishughulikia jinsi itikadi za Muyaka na Mwanakupona ziliathiri uteuzi wa maudhui. Watunzi hawa waliathirika pakubwa na itikadi zao kwani zile imani na fikra ndizo tulipata ziliendeleza vitushi katika kazi zao. Watunzi hawa tulipata walishughulikia masuala kwa namna tofauti ingawa walikuwa wa kipindi kimoja cha karne ya kumi na tisa. Masuala yaliyokuwa yakiendelea katika mazingira yao ndiyo tuliyapata katika kazi zao. Kwa mfano, Muyaka alishughulikia masuala ya vita na utawala na pia mambo kama vile mifumo ya kiuchumi na hata usaliti katika ndoa. Kwa upande mwingine, Mwanakupona alishughulikia utii wa dini, mume, uhusiano bora na wanajamii na hata udumishaji wa ndoa. Muyaka aliathirika na itikadi ya ukandamizaji, mapinduzi ya nguvu na hata uhuru wa kiakili. Itikadi ya ukandamizaji nayo ilichangia uwepo wa maudhui ya tamaa, umasikini na matabaka na hata magonjwa na kifo. Hapa mtunzi alituonyesha jinsi maudhui hayo yalipelekea mtu kukandamika kimwili, kifedha na pia mtu kumkandamiza mtu mwingine. Itikadi ya mapinduzi ya nguvu pia ilichangia maudhui ya uzalendo na vita ambapo mtunzi alituonyesha vita, mapambano na mapinduzi ya kiutwala katika kipindi chake cha kuondoa utawala wa mkoloni. Mwisho mtunzi aliathiriwa na itikadi ya uhuru wa kiakili pale

alishughulikia mambo mengi ambayo hayakupatikana katika utunzi wa karne yake. Utunzi wake uliegemea masuala ya sokoni na alishughulikia mifumo ya kiuchumi na pia usaliti na mapenzi wa dhati katika ndoa ambayo mengine hayakupaswa kuzungumizwa kwa uwazi. Kwa upande mwingine Mwanakupona aliathiriwa na itikadi ya utiifu, taasubi ya kiume na hata ukawaida. Itikadi yake kuu ya utii ilipelekea uteuzi wa maudhui ya dini, utamaduni na hata uhusiano wa wanajamii. Utii ulijitokeza kumtawala mtunzi kwani Mwanakupona ambaye alifuata hejemonia ya dini na pia tamaduni za Waswahili Waislamu. Mtunzi alionekana kutii hivi vipengele na alipitisha zile fikra na imani kwa bintiye bila hata kuziona kama zinazomnyanyasa mwanamke. Bali aliziona kama zitakazomsaidia mwanamke kuepuka ugomvi baina ya mumewe na wanajamii na pia kuwa na maisha mema. Vilevile, tulishughulikia jinsi itikadi ya taasubi ya kiume na itikadi ya ukawaida ziliathiri mtunzi katika kuteua maudhui ya ndoa na familia, utamaduni na pia dini. Hapa ilijitokeza jinsi mtunzi aliendeleza taasubi ya kiume katika jamii yake kupitia dini na utamaduni kwa kuyafanya mawaidha yake yakae kama masuala ya kawaida na yaliyokubalika. Hivyo, aliyapitisha kwa bintiye na bintiye alilazimika kuyafuata bila kupinga chochote ingawa yalimdunisha na kumdhalilisha.

### 3.4 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia jinsi itikadi zinazowaongoza Muyaka na Mwanakupona zilivyopelekea maudhui yao. Kutokana na data ilibainika kuwa itikadi za Muyaka kama ukandamizaji, mapinduzi ya nguvu na uhuru wa kiakili zilipelekea maudhui ya kukandamizwa na magonjwa, kifo na umasikini, mapinduzi ya nguvu yaliyosheheni vita wakati wa ukoloni na pia uandishi uliokiuka maudhui yaliyosheheni utunzi wa kishairi wa wakati wa urasimi mkongwe. Pia mtunzi anawasilisha maudhui yake vitofauti. Kwa

upande wa Mwanakupona ilibainika kuwa mtunzi alithihirisha utiifu wa hali ya juu kwa kuchora mazoea katika mazingira yake ambayo yalionekana kama ukawaida uliokubalika. Alishughulikia haya na kunuia kuyapitisha kwa bintiye kwa hiari yake mwenyewe bila kuona mengine kama yanayomkandamiza mwanamke.

Sura iliyofuata tuliangazia jinsi itikadi zilivyoathiri mtindo katika mashairi ya muyaka na *Utenzi wa mwanakupona*.

# SURA YA NNE

# JINSI ITIKADI ZILIVYOATHIRI MTINDO KATIKA MASHAIRI YA MUYAKA NA *UTENZI WA MWANAKUPONA*

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia namna ambayo itikadi za Muyaka na Mwanakupona zilivyoathiri mitindo watunzi wanayoteua kuitumia katika kazi zao. Muyaka na Mwanakupona waliongozwa na itikadi tofauti na hivyo kupelekea namna wanavyojenga beti na mishororo yao na pia lugha wanazoteua. Mtafiti alitumia nadharia ya itikadi kuonyesha namna watunzi hawa wawili waliwasilisha mitindo vitofauti ingawa walikuwa watunzi wa kipindi kimoja.

## 4.1 Ufafanuzi wa dhana ya Mtindo

Leech na Short (2007:9), wanasema mtindo hujihusisha na jinsi lugha hutumika katika muktadha maalum kwa mtu maalumu kwa lengo maalum, na kadhalika. Katika fasihi, hujitokeza tofauti katika nyanja za maana na msisitizo. Kuna wakati ambapo istilahi hii imetumika kumtofautisha mwandishi mmoja na mwingine katika kipindi maalum, muundo maalumu, namna ya uandishi au vyote kwa pamoja. Leech na Short katika kufasiri maana na neno hili wanagusia mawanda mapana sana. Wanauona mtindo katika fasihi kama jinsi mtunzi huweza kufanya mchezo wa maneno borake yale maneno yatumike katika muktadha sahihi na kwa lengo lengwa. Kwa kifupi, wanaufasiri mtindo kama upekee wa mwandishi

Kulingana na Shaaban Robert (1967) mtindo ni ujenzi dhahania wa wahusika na mandhari lakini wenye kusawiri taswira halisi ya matukio katika jamii lengwa. Hivyo, mtindo katika kazi za fasihi huwa mambo yote isipokuwa vipengele vingine vya kifani na maudhui.

Mtindo hutegemea kipindi cha mtunzi, malezi ya mwandishi na historia yake na mazingira alimoishi. Haya humfanya mwandishi kuwa na urahisi wa msamiati mwafaka unaopatikana katika ule ulimwengu wake.

Hivyo, uchambuzi wa mtindo unajumuisha lugha, muundo na mitindo ya uandishi iliyotumika katika kazi husika. Dhana hizi zinahusiana na kufungamana na zinapotenganishwa, maana iliyomo iliyokusudiwa na mtunzi katika shairi hupotea. Katika sura hii tulibainisha jinsi itikadi zilivyomwathiri Muyaka na Mwanakupona katika uteuzi wa mtindo waliotumia katika kazi zao. Kutokana na hayo tutaweza kuewelewa mbona Muyaka na Mwanakupona walitunga mashairi yao jinisi walivyo na utofauti unajitokeza wapi katika kazi hizi mbili.

## 4.1 Jinsi Itikadi Zilivyopelekea Uwasilishaji wa Mitindo Katika Mashairi Ya Muyaka

### 4.1.1 Itikadi ya Uhuru Wa Mtunzi ilivyopelekea Mitindo

Mashairi ya Muyaka yana mishororo minne ambayo kila mshororo una pande mbili. Kila upande una mizani minane. Kulingana na Abdulazizi (1979), Muyaka anawakilisha kipindi muhimu cha utunzi na mapendeleo ya utunzi wa mashairi. Mazrui (2007:19) anaongeza kuwa katika milki ya Muyaka, mashairi katika lugha ya Kiswahili yalifikia mwafaka wake kama utanzu adhimu katika uteuzi na utumizi maalumu wa maneno ya Kiswahili kishairi. Mashairi yake yalijengeka kwa mishororo minne inayotengeneza ubeti au beti, urari wa mizani 16 wenye kituo katikati ya mstari (kipande) na urari wa vina vya mwisho, mara nyingi ukihitaji umakinifu zaidi katika kuutumia ndani ya kazi husika.

Muyaka alianzisha mashairi yaliyodhihirisha upekee na jinsi anavyotawala utunzi wa ushairi juu ya matukio ya wakati huo wa kipindi chake. Uhuru wake wa kiakili ulipelekea

utunzi juu ya mapenzi na kujitambulisha, ustawi wa jamii yake, mapenzi yakilaghai ya watu kadhaa wa kipindi hicho na majanga yaliyokuwa yakiwakumba watu wa Mombasa. Hapa, Mazrui anajaribu kuelezea kwa kifupi umaarufu wa Muyaka katika utunzi wa mashairi.

Anamwonyesha kuwa ndiye mtunzi wa kwanza wa mashairi ya Kiswahili yaliyojitokeza katika urari wa vina na mizani na yenye mistari mine. Pia Mazrui anasema utunzi wake Muyaka wa mashairi ulizingatia zaidi mambo yanayoihusu jamii yake na yanayojitokeza papo hapo. Masuala ya majanga ya ukame na ustawi wa himaya ya Mombasa, mapenzi ya kilaghai ndani ya jamii n.k. Hivyo itikadi hii ya uhuru wa kiakili ya mtunzi ilichangia pakubwa katika kuanzia ushairi (mashairi) wa kirasimi wenye unne(tarbia) na kuuondoa ushairi wa Kiswahili msikitini na kuuingiza duniani yaani maudhui yake kuzungumzia masuala ya kiutamaduni, kisiasa, kijiografia, kijamii, kiuchumi n.k unajidhihirisha pia kwa mujibu wa Wafula (2007). Abdulaziz (1979) anaongeza kuwa Muyaka ni mtunzi wa karne ya kumi na tisa anayesifika sana kwa kuyaandika mashairi ya tarbia. Pia anajulikana kuwa miongoni mwa watunzi wa kwanza kuyaondoa mashairi ya arudhi nje ya msikiti. Methali nyingi katika lugha ya Kiswahili zinapatikana katika mashairi ya Muyaka....”

Hivyo, vipengele vingi vya kimtindo vilichanganuliwa kwa udondozi wa mifano mwafaka wa vipengele vya kimtindo ulifanywa ili kuelewa dhana hii ya mtindo katika mashairi ya Muyaka.

#### 4.1.1.1 Mtindo wa matumizi ya Kipokeo

Kulingana na Abdulaziz (1979), Muyaka anatumia kipokeo sana katika mashairi yake. Kipokeo kilitumika kusisitiza jambo muhimu ambalo lilinuiwa kupitishwa kwa kutumia lile shairi. Kipokeo kimejitokeza kwa namna tofauti: kwanza, kipokeo ambacho huwa

“mshororo mzima, upande mmoja wa mshororo au neno.’ Pia mashairi yake machache yalichukua muundo wa kipokeo kuwa viwili. Kipokeo kimoja katika upande mmoja wa mishororo au maneno katika ule upande; Muundo mwingine ni mishororo wa mwisho wote au upande wa mwisho katika ule mishororo. Haya yanajitokeza kama ifuatavyo:

*Mwanadani wako mwandani, ukitaka umjuwe,*
*Ngia naye safarini, wende mwendo wa kuwe,*
*Au muate nyumbani, ukatembee ukawe,*
*Ataopo kuwa mwewe, huyo ni wako mwandani.*

*Mwandani wako mwandani, ukitaka mfeeli,*
*Mtima utie K’ani, utumie yakwe mali,*
*Umuonapo haneni, hakuregeza kauli,*
*Ha-shabihi ha-mithili, huyo ni wako mwandani.*

Katika shairi hili, tunapata kuwa ‘Mwandani wako Mwandani,’ ambao ni ukwapi, katika mishororo wa kwanza na ‘ukitaka umjuwe,’ ambao ni utao wa mishororo wa nne, ni vipokeo. Hapa mtunzi anasisitiza kwanza, mwandani wako ni mwandani wako. Pili, anasisitiza mambo unayopaswa kufanya ili kujua kama ni mwandani. Mtunzi anaorodhesha sifa kama vile ; kumuacha nyumbani na kuenda safarini ndefu. Kama hatakuwa “mwewe” hivyo huyo ni mwandani wako. Pia, ukitumia hela zake bila ya kuteta na anayetafuta suluhisho baada ya kutembea naye kwenye njia iliyojaa miba na matope. Hapa uhuru wa mtunzi wa kiakili kutokana na amzingira yake ulimpelekea mtunzi kuandika vipokeo vyake kwa namna tofauti ikilinganishwa na Mwanakupona ambaye kipokeo kilitokana na neno lililorudiwa rudiwa.

Mtindo huu pia ulijitokeza pia kupitia pale neno moja linarudiwarudiwa katika mishororo. Haya yanajitokeza katika shairi la '*Panda*' ukurasa 190.

> *Panda, panda la mnazi I'anzalo kupapatua,*
> *Panda juu ya malazi moyo wako weshe ngowa,*
> *Panda mti wa mapenzi uwepushie na juwa,*
> *Panda ni wako uluwa. Panda darajani, panda !* (Abdulaziz 1979, ubt 1)

> *Panda juu ya farasi kwa haiba na sitawa,*
> *Panda kiwango mkwasi uukimbie ukiwa,*
> *Panda, situpe viasi wendako ukikujuwa,*
> *Panda, ni wako uluwa. Panda darajani, panda !* (Abdulaziz 1979, ubt 2)

> *Panda nganu na mpunga afudhali ya viliwa*
> *Panda wimbi na kimanga vipawa vya kupewa*
> *Panda usitunde ch'anga, tauwa mbivu tauwa*
> *Panda ni wakouluwa, panda darajani, panda !* ` (Abdulaziz 1979, ubt 3)

Shairi hili lilitungwa ili kuwatia moyo na kuwasifu wafuasi wake, yamkini mmoja wa viongozi mjini Mombasa. Mfano katika ubeti wa pili, mtunzi ametumia neno hili panda kumaanisha tendo la kukwea juu ya kitu kingine (farasi) katika mshororo wa kwanza. Katika mshororo wa pili mtunzi ametumia neno hili kumaanisha kupanda kiwango. Mshororo wa tatu anamaanisha tendo la kuendeleza juhudi zako, yaani mtu asikate tamaa (situpe viasi) katika safari ya maisha, hasa unapoanza kuelewa unakoelekea. Mshororo wa nne unarudia na kusisitiza tendo la kuendelea kupanda mimea, endelea kukua na kupanda

kwenye daraja. Yaani kuwa juu ya daraja.

Vilevile, kipokeo pia kimetumika na mtunzi ili kuonyesha upekee wa jambo linalosisitizwa katika kila ubeti.

*Dunia mti mkavu, kiumbe siulemele,*
*Ukaufanyia nguvu kuudhabiti kwa ndole;*
*Mtiwe ni mtakavu, mara ulikwangushile.*
*Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi.*

*Dunia mwendo wa ngisi, kamwe msililiwale,*
*Mkakithiri utesi kwenda mwenendo wa kule;*
*Na kutupiza viasi kwa hayana na hayale,*
*Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi.*

*Dunia kitu dhaifu, kiumbe siijetele,*
*Kwa kupata utukufu na furaha ya milele;*
*Kumbuka na uvundifu ujapo ni kama ndwele;*
*Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi.* (Abdulaziz 1979, uk 63)

Kila ubeti wa shairi hili unarejelea na kusisitiza kwa njia tofauti, lakini dhana moja ya usaliti na adhari zake kwa binadamu wengine. Hapa, ubeti mzima unajitokeza kama kipokeo cha shairi kwa ubeti kwa jumla unatumika kusisitiza dhana ya usaliti. Mtunzi anawaambia wasomaji kuwa dunia inaweza msaliti mtu hivyo waione wamesonga mbele au wameendelea kimaisha wakadhania wamefika kwani kurudi nyuma si kazi. Mtunzi katika ubeti wa kwanza anatumia mti mkavu kusiistiza ile dhana na usaliti. Anasema ule mti ni

mkavu hivyo mtu asije akajisitiri pale mtini. Kwani ule mti umeoza na unaweza mwangusha ardhini. Katika ubeti wa pili mtunzi ametumia ngisi. Anafananisha dunia na ngisi kwa kuwa na mwendo wa kasi na pia mwendo wake huwa wa mbele na pia nyuma. Hivyo ni vigumu kueleweka ngisi anapoenda. Ubeti wa tatu mtunzi anafananisha dunia na kiumbe dhaifu. Anasema mtu asije asidanganywe na kufumbwa macho na mafanikio aliyonayo na furaha inayoonekana kuwa ya milele. Bali mtu anapaswa kuwa makini na kutarajia lolote kwani dunia inaweza msaliti na kumvamia kama ugonjwa sugu.

Katika shairi hilo maana haiathiriki kwa kutoa ubeti wowote hapo ama kwa kubadilisha mpangilio wa zile beti. Kila ubeti unamaana tofauti ambayo inatumika kujenga ile dhana ya usaliti inayosisitizwa katika ushairi mzima. Beti zote hapa zinatumika kama kipokeo ili kusisitiza dhana kuu. Mtindo huu, unatumika kwa mashairi mafupi na yaliyorahisi kueleweka (Abdulaziz, 1979, 64).

Vilevile, upekee wa utunzi wa Muyaka pia ulijitokeza pale anatumia mtindo wa kuunganisha beti mbili kwa kutumia ukwapi wa mshororo wa mwisho kama ukwapi wa mshororo wa kwanza na ubeti unaofuata. Ukwapi wote au maneno machache katika ule ukwapi unatumika kusisitiza jambo fulani. Hapa ukwapi huo unatumika kama kipokeo. Abdulazizi (1979) katika ukurasa 64, anasema kuwa mtindo huu unafanana na ule uliotumika katika mashairi ya Kiingereza ya zama za kati kama anavyopatikana katika kazi ya Pearl (1963). Mfano (ukurasa 64) ;

*Yaulizeni ya leo mukumbuke na ya jana ;*

*Mambo jinsi yendao usikuwe na mtana,*

*Ulimwengu ni upeo, mamboye hadi hayana ;*

*Twachana kuambiyana, twangaliana kwa mato*

.

*Twachana kuambiyana, nenole limepoteya ;*

*Zamani zikidangana hugeuka watu niya ;*

*Wavyele huwa vijana mambo yakiwatatiya,*

*Ambapo yawele haya twangaliana kwa mato.* (Abdulaziz 1979)

Mfano mwingine (ukurasa 91);

*Ai kitendo na neno la ahadi na ziasi;*

*Lendeapo siku mno, ni haiba ya mpasi ;*

*Mwendo mtake kwa sono hata awe na nafasi,*

*Ai simba na farasi watakapokutana!*

*Ai farasi na simba wangiapo kwenda mbio;*

*Hutarakanya marimba na kukutakuta nyayo;*

*Na kunguruma ja mwamba, ukimbile utishao,*

*Ai mato na kioo kitakapokukutana!* (Abdulaziz 1979)

Kutokana na mifano hii ni wazi kuwa uandishi wa Muyaka ulidhihirisha uhuru wa kiakili wa kiakili. Hii ni sababu alivyocheza na maneno na kupanga vipokeo vyake vitofauti. Pia ikilinganishwa na Mwanakupona, Muyaka anatumia mitindo mingi katika tungo zake lakini Mwanakupona anatumia kipokeo cha kurudia neno ili kupelekea msisitizo wa wazo. Hivyo Muyaka anajiondoa katika ule 'ung'amuzi potofu,' wa kuunda vipokeo vya neno tu ila anacheza na maneno yake na kuibuka na mitindo iliyo na maneno, upande mmoja wa mshororo na hata kubadilishana pande za mishororo.

#### 4.1.1.2 Mtindo wa Ugonganishaji wa Wahusika Kihalisia

Uhuru wa utunzi wa Muyaka ulimpelekea kuibua baadhi ya dhamira zake kwa kutumia kuwagonganisha wahusika kihalisia ili kuleta uhalisia katika utungo wake. Kwa Mfano, Muyaka alitumia mtindo wa kutumia wahusika ambao wanajulikana kuwa hasimu katika ulimwengu halisia ili kuichora ile mivutano na uadui katika tungo zake. K.v, dhana ya mapenzi ya ulaghai na umalaya kwa wanawake wa mji wa Mombasa kwa kipindi hicho anayadokeza kwa kumtumia mwanamke mmoja aliyewagonganisha wanaume watatu akiwemo Muyaka mwenyewe.

Pia kulingana na Abdulaziz (1979:92) akimnukuu ubeti wa Muyaka anasema;

*Mbwene mwinda na t'aza, kuemewa ni tomezi,*

*Mno vikanishangaza, hapatwa na makuuzi,*

*Hafikiri nikiwaza, mola ndiye muwawazi,*

*Tui na mani na mbuzi, huvushwaje dau moja.*

Muyaka hapa vilevile anatumia mtindo wa kuvileta pamoja vitu hasimu mfano, tui (chui) na mbuzi katika ubeti huu, ili kuona kama vitu hivyo vinawezekana kutangamana lakini anakusudia kusema kuwa fahari wawili hawakai zizi moja. Mtindo wa aina hii ni upekee wa mtunzi ambao ulichangiwa na uhuru wa kufanya utungo wa aina yake. Uandishi wa aina hii ulimtofautisha Muyaka kwa watunzi wengine.

#### 4.1.1.3 Mtindo wa Matumizi wa Lugha ya Picha na Taswira.

Huu pia ni mojawapo wa upekee unaopatikana katika tungo za Muyaka ikilinganishwa na Mwanakupona. Katika kipindi hicho, uandishi mwingi haukuchora taswira au picha halisi za matukio ya kihalisia katika jamii lakini tunapata upekee huu sana katika uandishi wa Muyaka. Mtunzi alitumia vitu mbalimbali vinavyopatikana katika jamii yake kupunguza

ukali wa suala anaolokusudiwa katika jamii yake. Kulingana na Abdulaziz (1979 ; 98-99), baadhi ya maneno aliyotumia Muyaka ni kama ;

Simba/mato badala ya mume,

Farasi badala ya mke,

Majani makavu ya mnazi badala ya wazee/watu au kizazi tangulizi,

Majani mabichi ya mnazi kumaanisha kizazikichanga/ chipukizi,

Dau kumaanisha mwanamke,

Karatasi kumanisha mtume/ujumbe n. k.

Mfano halisi;

*Ai <u>farasi na simba</u>, wangiapo kwenda mbio;*

*Hutarakanya marimba na kukutakuta nyayo;*

*Na kunguruma ja mwamba ukimbile utishao,*

*Ai mato na kioo kitakapo kuk'utana! (ubeti wa pili ukurasa.91)*

Katika ukurasa 99 pia tunapata akisema:

*Risala mwenye adabu, tumishi mwenye maana;*

*Fika kwa wangu muhibu, kanisalimiye sana;*

*Mwambie ata ghadhabu, watetao hupatana;*

*P'endo za juzi na jana timiza usizondowe.*

*<u>Karatasi</u> nakutuma leo unitumikiye;*

*Kabalegheshe kalima, uzidi kusema naye;*

*Kudanganyana si kwema, kula jambo kwa ndiaye ;*

*Yalekeze yalekee tusambiane uwongo.* (Abdulaziz 1979)

Neno karatasi limetumika hapa kumanisha mtume/ujumbe. Uhuru wa mtunzi wa kiakili ulimfanya mtunzi kuchagua yaliyofaafu katika mazingira yake na kuyatumia katika utunzi ili kueleweka kwa urahisi na hadhira yake. Haya yalionyesha kuwa mtunzi hakujifunga kwa maudhui yaliyotaala utunzi wakati ule tu na mitindo ya wakati ule bali alitunga kuhusu yaliyoko katika jamii kwa ujumla. Ndiposa anatumia maneno ya vitu halisia ili watu waelewe anayoyasema kama anavyotumia neno karatasi kumaanisha mtume au ujumbe katika shairi la risala. Mtunzi alitumia maneno yake kuwakilisha neno lingine ili kuleta ule mchezo wa maneno na pia uelewa.

Vilevile, lugha ya picha pia imetumia ili kufafanua zaidi maana ya ndani ya anachozungumzia mtunzi. Mfano ulipatikana katika shairi la "*Panda,*" ukurasa 190. Ubeti wa pili unasema:

*Panda juu ya farasi kwa haiba na sitawa,*

*Panda kiwango mkwasi uukimbie ukiwa,*

*Panda, situpe viasi wendako ukikujuwa,*

*Panda, ni wako uluwa. Panda darajani, panda !* (Abdulaziz 1979)

Katika mshororo wa kwanza neno panda linatumika kumaanisha kupanda mnayama (farasi), lakini kitaswira ni kuinuka juu kwa heshima, haiba na utulivu. Farasi anatumika hapa kuashiria nguvu na mamlaka. Hivyo kuwahimiza watu kujiinua kwa hadhi na nidhamu. Mshororo wa pili nao neno pande linatumika ikiwa na maana kujiboresha au kujiendeleza kimaisha. 'Mkwasi' ni tajiri hapa na 'ukiwa' ni hali ya upweke au umasikini. Hapa mtunzi anawahimiza watu waondoke katika hali ya chini kuelekea hali ya juu (mafanikio).

Mshororo wa tatu neno panda linamaanisha kuendeleza juhudi zako. Mtunzi anawahimiza

watu wasikate tamaa ‘situpe viasi,’ katika safari ya maisha, hasa unapoanza kuelewa unakoelekea. Hapa anawatia moyo watu waendelee bilia kurudi nyuma. Mshororo wa nne neno panda kusisitiza maana ya kuendelea kupanda, kukua na kukwea kwenye daraja. Ikiwa na maana ya daraja ya maendelea, mafanikio au neema.  Lugha inayotumika hapa ni lugha ya kitaswira. Inatumika na mtunzi kama ishara ya maendeleo na ushindi.

Mfano mwingine upo katika shairi la “Dunia Mti Mkavu” (Abdulaziz, 1979, Uk 63) ;

*Dunia mti mkavu, kiumbe siulemele,*
*Ukaufanyia nguvu, kuudhibiti kwa ndole,*
*Mtiwe ni mtakavu, mara ulikwangushile,*
*Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi.*

Hapa mtunzi anatumia taswira ya mti mkavu kwa ustadi wa hali ya juu kufikisha ujumbe wa maisha, hatari, na hali ya kutotegemewa kwa dunia. Mshororo wa kwanza unatumia taswira ya kuona kwa kufananisha dunia na mti mkavu ambao hauwezi tegemewa wala si dhabiti wala salama. Katika mshororo wa pili tulipata taswira ya kiburi cha binadamu, kwani anadhani anaweza kudhibiti ulimwengu kwa ‘udole.’ Pia kuna kuna taswira ya mguso na kiburi pale anasema binadamu anajiona mwenye uwezo wa kuutawala ulimwengu kwa urahisi, lakini huo ni ujinga wa kibinadamu, kwa sababu dunia haina uimara wa kweli (ni mti mkavu). Katika mshororo wa tatu kuna taswira ya ghafla ya maanguko : ‘mtakavu’ (mti mkavu kabisa) unaanguka kwa ghafla tu mtu anapojaribu kuutumia. Anawaonya watu kuwa dunia yaweza kuangusha mtu wakati wowote.  Katika mshororo wa nne kuna taswiraya maisha kama safari, ambako ‘kuenda mbele’ si lazima kuwa jambo jema kila mara.  ‘Kurudi nyuma’ ni taswira ya kutafakari, kujirekebisha na kujiondoa katika njia hatari. Ubeti huu unatuonyesha picha halisi ya kuonya na maadili.

Mtunzi hapa alitawaliwa na itikadi ya uhuru wa uandishi unaotumia maneno faafu yanayowalisisha au kutupea picha fulani. Ustadi huu wa maneno ulimfanya mtunzi kuwasilisha makali mengine katika jamii kwa lugha rahisi isiyo na makali ya aina yoyote. K.m; Dunia mti mkavu, hapa ametumia \mti mkavu\ kuwakilisha hatari au hali ya dunia kudhoofika kiasi cha kutotegemewa.

### 4.1.2 Jinsi Itikadi Ya Mapinduzi Ya Nguvu ilivyopelekea mitindo

#### 4.1.2.1 Matumizi ya lugha iliyosheheni Maneno ya Kilahaja na Kuchanganya Lugha za Kigeni.

Japokuwa watunzi wengi hata wale wa kipindi cha Muyaka wamekuwa wakiutumia mtindo huu katika tungo zao, Muyaka pia katika usanaji wa kazi yake hakuchelea kwani hii inaaminika kuwa humtambulisha mtunzi na utamaduni wake na maingiliano na tamaduni zingine.

Kando na hayo, Abdulazizi (1979) anasema kuwa lugha iliyotumika na mtunzi katika mashairi yake ilikuwa na utata kwani haikueleweka kwa uwazi. Makala ya lugha mahususi iliyotumika wakati wa Muyaka hayakuwa hivyo ilikuwa vigumu kujua ni lugha ipi haswa iliyotumika Mombasa mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa. Abdulazizi akimnukuu Mwalimu sikujua, anasema kuwa Sikujua alikusanya na kuzinakili kazi za Muyaka ili kumpa Taylor na alisema huenda mashairi yale yalisheheni sana maneno ya lahaja ya kingozi. Abdulaziz anasema kuwa ilikuwa ngumu kujua ni nini haswa Sikujua alichomaanisha kwa kusema hivyo, lakini anadokeza kuwa Kingozi ni lahaja iliyotumika na inayotumika, ambayo inayodhaniwa kuwa ndio lahaja kuu katika mashairi ya mji wa Mombasa na Lamu ya karne ile.

Abdulaziz pia anaendelea kusema kuwa haikujulikana ni lahaja gani haswa ambayo mtunzi

aliyoitumia katika mashairi yake kwani kazi nyingi za karne na kumi na tisa zilisheheni lahaja ya kiamu na pia kimvita. Hivyo mtunzi alichanganya hizi lahaja.

1. **Namna Maneno ya kilahaja yalivyojitokeza**

Mtunzi ameyatumia maneno mengi sana ya kilahaja haswa lahaja ya kimvita ambayo ndiyo iliyomlea. Hapa mtunzi alitumia lugha ya sokoni, lahaja ya Kimvita na misamiati ya kawaida kama njia ya kuwasiliana na tabaka la chini. Hii inaakisi kile ambacho Marx (1977) anaeleza kuwa hatua za kujikomboa hutangulia na watu kutaka kujiondoa katika hali inayowakumba na kufanya mabadiliko. Hapa uhuru wa kiakili wa Muyaka unamfanya atumie upekee wa kuwasilisha ujumbe wake kwa lugha za kilahaja, hasa lahaja tatu, ambazo zinaeleweka na watu. Tena ilibainika kuwa mtunzi alitumia mtindo usio wa kidini kuwakilisha upinzani kwa itikadi ya kidini iliyotawala wakati huo, hivyo akajenga sauti mbadala ya kihistoria ambayo inasheheni lahaja za kiamu, kimvita na hata maneno ya kigeni, kutokana na mazingira ya wakati wake.

Mtunzi alitumia lugha ya iliyosheheni matamshi ya kiamu. Katika lahaja ya kimvita na kiamu, Abdulaziz amezungumzia tofauti zifuatazo;

| **Kiamu** | **kimvita** | **sauti katika mashairi ya Muyaka** |
|---|---|---|
| Y | j | j |
| S | sh | sh |
| Ny | ng’ | ng’ |

Pia mahali kuna /l/ na /r/ katika Kimvita sauti hizi zinatupiliwa mbali katika Kiamu na hili linapelekea neno linalotumika kwa jumla kwenye mashairi ya Muyaka kuwa lenye lahaja ya Kimvita

Mfano;

| **Kiamu** | **kimvita** | **neno katika mashairi ya Muyaka** |
|---|---|---|
| Kae | kale | kale |
| Nguu | nguru | nguru |
| Nyee | nyele | nywele |
| Kuusha | kurusha | kurusha. |

Pia, mahali kuna sauti /e/ mbili zikifuatana katika Kiamu, sauti /l/ au /r/ zinaekwa kati katika lahaja ya Kimvita. Mfano;

| **Kiamu** | **kimvita** | **neno katika mashairi ya Muyaka** |
|---|---|---|
| Mbee | mbele | mbele |
| Mtee | mtele | mchele (/t/ inatamkwa kama /ch/) |

/g/ katikati ya vokali mbili wakati mwingine pia inaondolewa katika Kiamu.

| | | |
|---|---|---|
| Nduu | ndugu | ndugu |
| Kuteua | kutegua | kuchagua. |

Tofauti nyingine kati ya lahaja hizi ni pale sauti /m/ iko katika Kimvi na neno la kijumla huku katika Kiamu inakuwa /Mu/. Mfano ;

| | | |
|---|---|---|
| Mui | mji (Kimvita) | mji |
| Muyumbe | mjumbe | mjumbe |

Pia katika Kimvita, maneno yanayoanza na /yu/ huondolewa /y/ katika Kiamu. Mfano ;

| | | |
|---|---|---|
| Upo | yupo | yupo |

Tunapata Muyaka aliathiriwa sana na lahaja mbalimbali za Kiswahili, ikiwa ni pamoja na kiamu, kwa sababu ya mwingiliano wa kitamaduni kati ya Mombasa na Lamu. Maneno ya Kiamu yanayojitokeza katika mashairi yake ni kama vile ;

Mbari- maana yake ikuwa familia au ukoo.

Mwana – maana yake ikuwa mtoto au mwa

Viru – maana yake ikuwa mambo au hali.

Ng'ambo- maana yake ikuwa nje ya nchi au sehemu nyingine.

Chuo- ikuwa na maana ya madrasa au shule.

Mfano mahususi unajitokeza katika shairi la '*Kuku wa Mkata*' (ukurasa 218). Hapa Muyaka anatumia maneno ya athri ya Kiamu, kama vile 'Kata' kumaanisha 'kuzuia au kizuia.' Neno 'Mkata' linaweza kuwa na maana pana zaidi ya mtu aliyekatazwa kufanya jambo fulani, kama vile Wapwani walidhibitiwa na watawala wa kigeni. Mtunzi anamfananisha yule myu na kiki anayefungwa lakini hana uwezo wa kujitafutia chakula. Hii inamaanisha jamii inayoshibitiwa na haina uhuru wa kujitegemea.

Mfano mwingine unajitokeza katika shairi la '*Natamani vuta nyanje'* ukurasa 244. Hapa mtunzi ametumia neno la kiamu – nyanje- lenye maana ya uwanja wa vita au sehemu ya wazi ambako vita hufanyika. Hili ni neno lenye athri ya kiamu, ambalo linatumiwa pia katika lahaja za kaskazini mwa Pwani. Hio ndio baadhi ya mifano miongoni mwa mifano mingine inayoshihirisha kuwa Muyaka alitumia lahaja ya Kiamu katika mashairi yake. Hivyo ilibainisha uhuru wa mtunzi wa uchezaji wa maneno ya lahaja ya kiamu na kimvita katika tungo zake.

Vilevile, lahaja zote mbili, za Kiamu na Kimvita, zilipatikana katika mashairi ya Muyaka. Wakati mwingine hadi kwenye shairi moja. Mfano ;

*Mpiga mai makanda ni kutaka kuyatuwa ;*

*Ndilo sumbuko la kwanda kupenda asotambuwa.*

*Lairi niwele konda na ladhaye haiyuwa,*

*Nguvu zangu na takuwa zinishizile nyangwani.*

Kwa Mujibu wa Abdulaziz (1979) maji na *haiyuwa* ni Kimvita. Inamaanisha maji na haijuwa. Na kwanda ni neno la Kimvita lenye maana ya kwanza. Mifano hii inaonyesha kuwa mtunzi alitumia lahaja zote mbili katika kazi yake lakini alipendelea lahaja ya kimvita dhidi ya kiamu. Hichens (1940) tunapata akiafikiana na haya na anataja mifano kama ;

*"Yatweukile mashaka, mashaka yatweukile,*

*Ja ndwele kutuepuka, kutuepuka ja ndwele,*

*Tutendele kwa haraka! Kwa haraka titendele!*

*Huzuni, situlichile ! Situlichile huzuni !"* (Abdulaziz 1979, uk.89)

Yaliyobainika katika sehemu hii ni kuwa uhuru wa kiakili na wa utunzi wa Muyaka ulimpelekea kuteua mtindo wa kucheza na maneno ya kiamu na Kimvita. Mtunzi alitumia maneno yanayofahamika na wanajamii na pia kueleweka ili wtu wapate kuelewa anayosema na kupata ujumbe mwafaka uliokusudiwa. Haya yalionyesha kuwa mtunzi alitawaliwa na itikadi ya uhuru katika uandishi wake, ambao ulipelekea uhuru wa kuchanganya lahaja ya kiamu na kimvita.

2. **Maneno ya Kiarabu:**

Uhuru wa Muyaka katika uandishi pia ulipelekea matumizi ya maneno ya kigeni katika tungo zake. Haya yanadhihirisha utangamano wa tamaduni zingine ndani ya jamii yake na haya yalipelekea mwingiliano wa lugha za Kireno na Kiarabu na kupelekea kutumika katika Kiswahili. Hii ni sababu taifa husika zilisafiri Mombasa na kuishi sehemu za Mombasa. Tunapata Muyaka alitumia maneno na sentensi za Kiarabu katika tungo zake. Haya yalitokea kutokana na uzoefu wake wa kutangamana na Waarabu waliotoka Mazrui; alitangamana nao haswa katika ngome (Abdulaziz, 1979). Anaongeza pia kuwa huenda Muyaka alitaka kuonyesha umaarufu na uweledi wake wa lugha geni ikifahamika kuwa

kufahamu lugha geni wakati ule, ilikuwa njia moja ya kubobea kimaarifa na kitamaduni. K.m;

*"Ilahi wa Maulaya Sayyidi wa Sayyidahu*

*Naomba hinyenyekea, ya Rabbi afuwahu*

*Mawi Ngwatubaidia yaliyo na ikrahu*

*"Faqadarnahu, fa nii'malqadiruna".* (Abdulaziz, 1979, uk 88)

Hapa ni wazi kuwa Muyaka alimzungumzia kiongozi wa Wamazrui Salim bin Hemed (mbaye alifariki mwaka 1835). Mtunzi alitunga shairi hili ili kumfariji kwa utawala wake uliosheheni misukosuko kama gavana wa Mombasa.

Njia hii ya kutumia lugha nyingine katika ushairi, hapa Kiarabu, iliweza kutumika na ule utaratibu wa vina na mizani ya ufasihi wa Kiajemi. Hili lililetwa na Waarabu. Mtindo huu unajulikana kama 'uingizaji wa beti za mtunzi mwingine ndani la shairi la mtunzi mwingine,' (Browne, 1928). Anaongeza kuwa Waarabu walitumia maneno kutoka kwenye Kurani na pia maneno ya watunzi wengine katika utunzi wao. Anawataja watunzi kama Hafiz-al-shirazi, Jalaluddin al-Rumi, Sa'ad na pia Jami.

Katika shairi hilo hapo juu mtunzi anatumia maneno ya Kiarabu kama:

"Ilahi wa Maulaya Sayyid wa Sayyidahu" ikiwa na maana ya "Ewe Mungu, Mungu wangu, mwalimu wangu na Mwalimu wao."

"faqadarnahu, fa nii'malqadiruna." Ikiwa na maana ya "sisi ndio tulio Kadiri, na sisi ndio wakubwa wa wanao amuru."

"Fa kam li n'nabii waliopita radahu." Ikiwa na maana ya "Ni manabii wangapi waliteseka katika dunia hii kwa sababu aliamuru."

Kutokana na hayo ilithihirika kuwa itikadi ya uhuru wa Muyaka ilimfanya kushughulikia

mambo katika mazingira yake kwa kutumia mtindo wa maneno ya kilahaja na pia lugha ngeni. Hii ni ili hata wale wageni waelewe utunzi wake. Uhuru huu ulimfanya acheze na maneno mageni na ya kilahaja sababu alinuia kuleta mabadiliko katika jamii kama Marx (1977) anavyokiri. Mabadiliko haya ya mtunzi yalihusisha kujumuisha yote yanayofanyika katika jamii kwa lugha zilizoko katika jamii.

**3. Maneno ya Kireno:**

Vilevile, uhuru wa kiakili wa Muyaka ulimpelekea mtunzi kutumia maneno ya Kireno yaliyobadilishwa kidogo. Itikadi ya uhuru wa Muyaka ilimfanya pia kuhusisha lugha ya Kireno katika tungo zake sababu ni lugha iliyozungumzwa wakati wake, lakini yale maneno yalibadilishwa kidogo. Kulingana na Abdulaziz (1979) hati zilizokuwa katika kazi za Taylor zinajumuisha kazi za Faliki au "Felix" kwa Kiingereza, ambaye aliishi Mombasa katika kipindi cha Wamazrui. Katika kazi ya Abdulaziz (1979) katika ukurasa 90, anaorodhesha mishororo ambayo ilijumuisha maneno ya Kireno. Maneno haya ni k.v;

*Portugesi afala, Faliki afala velo,*

*Baziada Spanyola, wa tarafai busolo,*

*Si nyana za kuanila, dafedhati dafedhalo,*

*Vinyu inakusumbula, xx ina butizalo.*

Katika ubeti huu, mshororo wa kwanza Muyaka anasema kuwa kireno ameshindwa, faliki naye ameshindwa pia haraka. anamaanisha wazungu wa Kireno na wa mataifa mengine wameshindwa. Katika mshororo wa pili anatumia anasema spanyoka kumaanisha Wahispania wa maeneo ya mbali (busoli ikimaanisha kaskazini). Anazungumzia Waspania waliokuwa sehemu nyingine za dunia, pengine akimaanisha nguvu zao. Mshororo wa tatu anasema si nyana za kuanila kumaanisha si jambo la kuchezea, na defedhati kumaanisha

kwa hakika. Hivyo anasisitiza ukweli wa yaliyotokea. Mshororo wa nne anatumia vinyu kimaanisha pombe au divai ya kizungu. Hapa maneno kama afala, velo, baziada, Spanyola, busalo, defedhati, vinyu, dafedhalo na butizo ni maneno ya Kireno.

Maneno ya msamiati wa Kimvita, Kiarabu na Kireno kama inavyoonekana kwa mfululizo hapo juu yalijitokeza kama mtindo wa Muyaka. Hii inaonyesha kuwa, mtunzi aliishi katika mazingira ambamo lugha hizo zilikuwa aidha lugha mama au lugha za wageni na hivyo kutumika akilinganishwa na Mwanakupona. Haya yalionyesha mwingiliano wa kitamaduni uliokuwepo pwani ya Afrika Mashariki katika karne ya 19. Mtindo huu wa kuchanganya lugha tatu katika kazi yake ni upekee wake Muyaka na unaThihirisha kuwa itikadi ya uhuru wa kiakili ilichangia pakubwa katika mtunzi kutunga mashairi yenye lugha hizo.

#### 4.1.2.2 Mtindo wa Udokezi wa Dhana Mahususi katika Mstari wa Mwisho wa Ubeti

Muyaka pia katika tungo zake alionyesha ustawi wake katika mtindo wa udokezi wa ujumbe mahususi katika mstari mmoja tu wa ubeti. Ubeti huo hubeba dhana mbalimbali kiasi cha kumchanganya mhakiki chipukizi kung'amua lengo la mwandishi au mtunzi. Ufanisi wa kuhakiki kazi zenye mtindo huu humhitaji mhakiki awe na uelewa na juu wa jambo linaloongelewa. Pia kutumia mtindo wa aina hii ulihitaji upekee. Muyaka hivyo alibainika kutumia mtindo huu na haya yaliyokana na uhuru wa kujumuisha huu ustadi katika utunzi wake. Mtindo huu katika tungo za mtunzi unajitokeza zaidi katika shairi la "*litakapo kukutana*" (Hichens,1940:55- 58);

*Ai kioo na mato, tia nuru takatifu,*

*Hujaalia jisito baadaye ukashufu,*

*Ni mshabaha wa kito yaakuti masherafu.*

*Ai, pua na harufu ! Itakapo kukutana !*

Hapa Mtunzi anajaribu kuchora mazingira ya nini kitatokea hasa baada ya mahasimu au swaiba wawili kukutana mfano pua na harufu, kiti na tawangu (tako), mkono na kazi n.k. Kwa hakika namna hii ya utunzi ni upekee wa Muyaka na ulidhihirisha uhuru wa kiakili wa mtunzi. Mtindo huu unamtofautisha sana Muyaka na Mwanakupona.

Abdulaziz (1979) anasema kuwa uchunguzi wake katika *Utenzi wa Mwanakuopona*, Utendi wa Ayubu, Utendi wa Masahibu kama unavyojitokeza katika Allen (1971) katika kurasa zake mbalimbali, unadhihirisha mtindo huu kuwa ni upekee wa Muyaka tu kwani haumithiliki.

Beti zinginezo za lile shairi zinazoonyesha ule mtindo pia ni ;

*Ai kitendo na neno la ahadi na ziasi ;*

*Lendeapo siku mno, ni haiba ya mpasi ;*

*Mwendo mtake kwa sono hata awe na nafasi,*

*Ai simba na farasi watakapokutana!*

*Ai farasi na simba wangiapo kwenda mbio;*

*Hutarakanya marimba na kukutakuta nyayo;*

*Na kunguruma ja mwamba, ukimbile utishao,*

*Ai mato na kioo kitakapokukutana! (Abdulaziz 1979)*

**4.1.2.3 Mtindo wa Matumizi ya Mashairi Mafupi.**

Namna hii ya utunzi pia imetawala sana tungo za Muyaka kwani mashairi mengi yake yana beti chache. Itikadi ya uhuru wa mtunzi ulimpa ule msukumo na pia ustadi wa kutunga

tungo nyingi zinazozungumzia mazingira yake. Na sababu alijihusisha na masuala mengi kama biashara, vita vya kiutawala, uongozi na hata mifumo ya kiuchumi, mtunzi alikumbana na mambo mengi na kutoa tungo zingine zenye beti mbili au ubeti mmoja ili awasilishe ujumbe uliokusudiwa. Hivyo kupelekea huu upekee wake. Kuna mashairi mengine yana ubeti mmoja mifano ya mashairi;

Ai Ulimwengu! (ukurasa 137).

*Ai, ulimwengu jifa, jifa Uchao k'ongea!*

*Kizima hutenda ufa, ugawe ukendelea,*

*Wenyi fahari na sifa wondoshile K'ongowea!*

*Wamezinga kama p'ia! Wasemi tutasemani?* (Abdulaziz 1979)

Si wanawake wa huja (ukurasa 172)

*Ukiwaona kwa mbali kwa vik'uku na vinganja,*

*Wamba ni wake wa kweli ukenda wakidhi haja,*

*Kanama ni batili swiswi na wao mamoja,*

*Si wanawake wa huja yalla ni yale mavao.* (Abdulaziz 1979)

Mifano mingine ya mashairi yenye ubeti mmoja ni*:*

Tanzi za nyama (ukurasa 172*),* Uovu (ukurasa.105), Karatasi ya kishami (uk.178), Tao la nyanje (ukurasa 180), Sichi (ukurasa 184), Mahaba (ukurasa 184), Wingu la masika (ukurasa 206), Mwanadamu kupani (ukurasa 216), Ai Mambo (ukurasa 216), Ua la manga (ukurasa 218), Mbwene shundwa (ukurasa 218), Natamani vuta nyanje (ukurasa 244), Tima na ima (ukurasa 244), Ulimwengu ni mkuu (ukurasa 258), miongoni mwa shairi nyinginezo.

Pia mtunzi ametunga mashairi yenye beti mbili. Mfano; "*Kimbiji changu*" (uk.168);

*Nastahabu kimbiji, kidau changu cha kwanza,*

*Kingawa mlejileji k'welea haikupanza,*

*Na kufa Ngozoa-maji, yali usiku wa kiza,*

*Ndipo leo hakiwaza haangama Kazekea.*

*Kiwinzo changu kiwinzo nilipo hakioleza,*

*Chalikuwa cha mateso nami kikinipumbaza,*

*Hatusa nacho ufunzo mawimbi kutoa kweza,*

*Ndipo leo hakiweza haangama Kazekea.* (Abdulaziz 1979)

Mifano mingine ni;

Kifo kikimbiza funza (ukurasa 172), Ndimi Muinda (ukurasa 176), Nazi na maji si mbata (ukurasa 192), Ugosi (ukurasa 210), Kuku wa mkata (ukurasa 218), Ulimwengu usiungie (ukurasa 258), Kesho utanitendendaje (ukurasa 292) na Bao naligwa (ukurasa 292)

Mtunzi pia ametumia beti tatu mfano;

Upweke (uk.298)

Papo waiyona ndia (ukurasa 268)

Wenda lionea tumba (ukurasa 272)

Uvuroni wa mademu (ukurasa 288)

Simuwati muwatiwa (ukurasa 296)

Nafikiri na ya nyuma (ukurasa 302)

Kalimambi yanonga (ukurasa 306) (Abdulaziz. 1979).

Isitoshe, kwa mujibu wa Hichens (1940), mtunzi pia ametumia shairi lililo refu zaidi ni lile lenye beti 19 "Litakapo kukutana" (uk 55). Matumizi ya ubeti moja, beti mbili na hata tatu

ni upekee wa mtunzi unaomtofautisha na Mwanakupona. Pengine mtindo huu ulisababishwa na majukumu ya kibiashara aliyokuwa nayo au ile tabia yake ya utunzi wa papo hapo kutegemeana na tukio ndani ya jamii kwa wakati huo. Utunzi wa aina hii ulichangiwa sana na itikadi ya uhuru wa kiakili kwani aliandika tungo zenye beti chache kando na uandishi wa mwanzo wa karne ya kumi na tisa.

#### 4.1.2.4 Matumizi ya Tamathali Mbalimbali za Usemi

Muyaka anaonekana kuitawala sana lugha katika uandishi wake kwani lugha yake imejumuisha tamathali mbalimbali za semi kama vile takriri, tashihisi, tashibiha na kejeli;

**Takriri**: Takriri ni urudiaji wa kifungu kimoja cha maneno mara kadhaa (BAKITA, 2015). Takriri ilijitokeza katika sehemu kubwa sana ya kazi ya mtunzi. Hii inaashiria kuwa, Muyaka katika ujumbe aliokuwa akitaka kuusisitiza kwa jamii alitumia mbinu hii ya takriri au alitumia takriri kuyapamba tu mashairi yake. Baadhi ya mifano ya takriri iliyojitokeza kwa Muyaka ni kurudiwa rudiwa kwa neno katika shairi zima. Maneno yamerudiwa mwanzoni mwa kila mstari wa mshororo. Haya yamejitokeza katika shairi la "*Oa*" katika ukurasa 182 (Hichens, 1940). Katika aina hii ya takriri neno oa limeweza kurudiwa. Neno "oa" linalojitokeza mwanzoni mwa kila mstari, limeendelea kutokea hadi mwisho wa shairi la OA. Hapa lengo kubwa la msanii ni kuonesha msisitizo wa kitendo cha kuoa kwa mhusika. Yaani kitendo cha kufanya makubaliano kati ya mwanamume na mwanamke kuishi pamoja kama mume na mke. Muyaka anasema:

*Oa, ndiwe muolezi, uzoeleo kuowa,*
*Oa, sifumbe maozi, maninga uchiyavuma,*
*Oa, uzaze uzazi kama ulivyozaliwa,*
*Oa, sizi ndizi ndowa. Aso kuoa ni yupi?* (Hichens 1940, uk 182)

Muundo wa aina hii pia ulipatikana katika shairi la ‘*Sichi*’ katika ukurasa 184. Hapa mtunzi anamaana ya hiki katika mshororo wa kwanza na wa pili, siki katika mshororo wa tatu na siogopi katika mshororo wa nne. Anasema:

*Sichi nlichokiona nilicho chandika icho,*

*Sichi sikiwati tena naradhiwa kufa nacho,*

*Sichi ni cha waungwana ndicho chakula walacho,*

*Sichi wala sina kicho sitili moyo huzuni.* (Abdulaziz 1979)

Pia takriri ya neno la kwanza katika mstari kujirudia kwa kila mwanzo wa mstari ndani ya ubeti ilijitokeza katika shairi la “*Mahaba*” katika ukurasa 184. Muyaka anasema :

*Mahaba ni maangavu, yakishitadi yaua ;*

*Mahaba ni meemevu, yemapo yana takua ;*

*Mahaba ni mapumbavu, bayaoni penye tua ;*

*Mahaba hayachi dua, hayahofu matukano*. (Abdulaziz 1979)

Neno “mahaba” limejitokeza mwanzoni tu mwa kila mstari wa ubeti mmoja tu wa shairi likidokeza msisitizo bayana pia katika jambo hilo. Hapa mtunzi ana maana ya hisia za mvuto zinazojengeka kwa mtu mwingine kutokana na kupendezwa naye (BAKITA, 2015). Takriri ya aina hii pia inapatikana katika shairi la *‘Jinga*’ katika ukurasa 186. Jinga inamaana ya kinga kikubwa na pia asiye na maarifa au uelewa wa jambo fulani. Kulingana na Abdulaziz (1979) inasemekana kuwa mmoja wa washindani mashuhuri wa Muyaka katika ushairi aliitwa Jinga.

Takriri ya aina hii pia ilijitokeza katika shairi la *‘Aha !*’ katika ukurasa 188. Mtunzi kulingana na Abdulaziz (1979) alikuwa katika kitanda cha mauti. Mtunzi mwenyewe anasema kuwa ndwele yamuuma na yale maumivu ndiyo yanayofanya aseme Aha ! Mtunzi

anasema :

*Aha ! Sengambile, Aha ! Ndwele yaniuma,*

*Aha ! N'ambie, sina siha, muwili wangu mzima,*

*Aha ! Kutoona raha, ndipo aha ! nikasema,*

*Aha ! Sambile kwa wema, nasema, kwa ndwele sii. (Abdulaziz 1979)*

Aina hii ya takriri pia imo katika shairi la '*Moyo*' katika ukurasa 188. Hapa Muyaka amesisitiza neno moyo kwa kulirudia katika kila mshororo. Shairi hili ni mapambano baina ya akili na mwili. Anasema :

*Moyo wanambia, "Kwamba, jambo la mtu usambe !"*

*Moyo wanambia, "Omba, kitu cha mtu siombe !"*

*Moyo wanambia, "Ramba, t'et'e ya moto sirambe!"*

*Moyo watamani p'embe ili na ndovu kitwani.* (Abdulaziz 1979)

Mwisho, haya yamo katika shairi la '*Panda*' katika ukurasa 190 na 192. Mtunzi anasema:

*Panda futa na mtama upate kuvumbikia,*

*panda juu ya mkoma vijana wakuolea,*

*panda dua kwa Karima kwa utakaso wa nia,*

*Panda, utafikilia, Panda, darajani panda* (Abdulaziz 1979, ubeti 6)

Takriri nyingine ni ile ya neno la mwisho wa kipande cha kwanza cha mstari kuwa neno la kwanza kwa kipandecha pili cha mstari huo. Mfano ;

*Usijitile kikaka, kikaka na sikitiko,*

*Utazidi kupulika, upulikile puliko ;*

*Utakalo ukitaka, ukitaka ndilo tako,*

*Subirisha moyo wako, mzoevu wa saburi.* (Abdulaziz 1979)

Hapa Muyaka pamoja na kutaka kusisitiza lakini pia anajaribu kuipamba kazi yake na kuonesha umahiri wake wa kuyachezea maneno ili kuleta ruwaza nzuri ndani ya kazi na mantiki.

**Tanakali-** sauti: Hii ni ile hali ya kurudiwa rudiwa kwa sauti au neno kutokanako na sauti au neno hilo kusikika tena. Senkoro (1983:17) akimnukuu Muyaka katika shairi lake la "*sichi*" katika ukurasa 184 anatubainishia aina hiyo ya tamathali. Hapa mtunzi anatumia neno sichi kumaanisha hiki katika mshororo wa kwanza na wa pili. Katika mshororo wa tatu anamaanisha siki na mshororo wa nne anamaanisha siogopi. Haya ni kama ifuatavyo:

*Sichi nlichokiona nilicho chandika icho,*

*Sichi sikiwati tena naradhiwa kufa nacho,*

*Sichi ni cha waungwana ndicho chakula walacho,*

*Sichi wala sina kicho sitili moyo huzuni.* (Abdulaziz 1979)

**Tashihisi** : Tashihisi ni mbinu ya kifani inayotumia uhuishaji wa vitu na uhai kwa kuvipa sifa za kibinadamu. Katika mashairi ya Muyaka bin Haji, tashihisi imetumika na mtunzi kuleta uhai, mvuto na maana ya kina katika maudhui anayowasilisha. Muyaka kama mshairi mahiri wa Kiswahili cha Mwambao wa Kenya, alitumia mbinu hii ya lugha kuzungumzia masuala ya kijamii, kiasiasa na kiutamaduni. Baadhi ya mifano ;

Abdulaziz (1979) ; "kumbile lambile witi, kimbelembele waume…" Hapa majani yalozeeka ya mnazi yanayasemesha yale majani chipukizi ya mnazi yakimbie. Hapa kwa ujumla Muyaka anayatumia majani makomavu kumaanisha wazee na majani chipukizi kumaanisha vijana na hivyo vitu hivi anavipa hadhi yakutenda sawa na binadamu.

Pia kuna shairi la '*Kimya*' katika ukurasa 194. Hapa mtunzi anapea kimya za kibinadamu kama vile "kina mshawishi kwa daima na milele na pia kina mambo mbele." Vilevile,

Mtunzi amekipea uwezo wa kutawala, kana kwamba ni kiongozi au mfalme. Muyaka anaonyesha kuwa wakati mwingine, mtu anaponyamaza, anakuwa namamlaka zaidi kuliko anayezungumza. Mtunzi hapa anaonyesha upee wake kwa kuleta maana nzito kwa kutumia lugha ya picha. Kwa kufanya kimya kuwa kitu chenye uhai, mshairi anasisitiza uzito wake katika maisha ya binadamu- kwamba kuna wakati ambapo kimya kina nguvu zaidi kuliko kelele au mabishano.

Mfano mwingine unajitokeza katika shairi la '*Ndimi muinda'* ukurasa 176. Hapa mtunzi anaanza mshairi kwa kusema'ndimi muinda mkuu mjini mwenu mzima.' Hapa, anatumia ndimi kumaanisha lugha, huku akiipea sifa za muinda. Yaani mwindaji. Ikimaanisha kuwa lugha inaweza kuwa na madhara makubwa kama vile uwindaji wa binadamu au hata simba. Hii inaonyesha jinsi maneno yanavyoweza kuwa hatari na yenye nguvu. Muyaka anatumia tashihisi hii kwa njia ya kuipa lugha uwezo wa kutenda kama binadamu au kiumbe uhai. Anasisitiza tahadhari kwa watu kuhusu jinsi wanavyotumia maneno yao, akionya kuwa lugha inaweza kuwa silaha yenye madhara au chombo cha kuleta amani. Tahihisi hii inasaidia kuleta uzito wa ujumbe wake kwa njia ya lugha ya picha inayoeleweka kwa urahisi.

Mfano mwingine umo katika shairi la '*Kongowea yaugua'* ukurasa 202. Mtunzi anaanza hilo shairi kwa kusema kuwa Kongowea yaugua kwa vilio vya uchungu na uuguzi. Hapa, Muyaka anaupa mji wa Kongowea sifa za kibinadamu kwa kusema kuwa 'yaugua' na inapitia machungu na inalia.' Hili linaashiria kuwa mji unakumbwa na matatizo makubwa, huenda ni hali mbaya ya kiuchumi, kisiasa au kijamii. Muyaka anatumia mbinu hii ili kusiistiza athari za mabadiliko yaliyoko mjini huo. Hii inasaidia kuleta mvuto, hisia na ufahamu wa kina kwa msomaji kuhusu hali halisi ya Kongowea wakati huo.

**Tashibiha :** Tamathali hii ya usemi pia imejitokeza kwa wingi katika mashairi mbalimbali yaMuyaka. Mifano katika Abduliaziz (1979 :85) anathibitisha hili katika moja ya beti za shairi la Muyaka.

*"Kumbifu lambile witi, "kimbelembele waume"*

*Mja mwanzo hajuti, majuto huja kinyume;*

*Mvundat'i ni mwanat'i mgeni mzo mpime!"*

*Yu utukuni Mngwame huza k'apu kwa miyaa.* (Abdulaziz 1979)

Hapa, "kumbifu lambile witi" ni ulinganishi wa majani makavu na yale mabichi katika muktadha wakiutendaji. Wanaohusishwa hapa ni watu hasa vijana kwa wazee. Pia neno "Mja" limetumika kitashibiha zaidilikimaanisha mjukuu. Pia ". Dunia mti mkavu, Dunia mwendo wa ngisi..."

**4.1.2.5 Mtindo wa Maneno katika Ukwapi kugeuzwa katika Utao.**

Upekee wa mtunzi pia ulipatikana pale alibadilisha mpangilio wa maneno katika beti zake. Maneno katika ukwapi yaligeuzwa utao, yaani maneno katika pande zote ni sawa lakini yamebadilishana. Itikadi ya uhuru wa mtunzi na hata mapinduzi ya nguvu yalipelekea haya sababu mtunzi alinuia kucheza na maneno yake ili tunzo zake kuvutia hadhira. Itikadi hii zimetokana na hali y jinsi mtunzi alitangamana na masuala mengi hivyo alitaka shairi zake zijumuishe yaliyoendelea katika jamii. Pia itikadi ya mapinduzi kutokana na mtazamo wa Karl (1977) ulioakisi mapinduzi katika jamii, ulimpelekea mtunzi kutaka kuibuka na tungo za kipekee kando na ufuataji wa kanuni za uandishi wa kifasihi wa urasimi Mkongwe. Kwanza ni pale mtunzi anageuza maneno yote katika ukwapi yanageuzwa katika utao. Mfano; pale mtunzi anatumia maana iliyo kwenye ukwapi na kuendeleza ile maana katika utao akuwa ameubadilisha kimpangilio wa maneno. Maana hapa inapelekea kujitokeza

kupitia maneno yale yale, au mtunzi anayabadilisha kimpangilio. Yaani, neno la kwanza katika ukwapi kuwa la mwisho katika utao na la mwisho katika ukwapi kuwa la kwanza katika utao. Kwa mujibu wa Abdulaziz (1979, 95), Muyaka alitumia mtindo huu ili kusisitiza jambo bila kukaa ni kama ameyarudia maneno yake. Mfano ulioko hapa chini unaelezea haya. Hivyo imebainika kuwa utao kwa kila mshororo ni ukwapi ukuwa umebadilishwa.

*Yetweukile mashaka, mashaka yatweukile;*

*Ja ndwel kutuepuka, kutuepuka ja ndwele;*

*Tutendele kwa haraka, kwa haraka tutendele;*

*Huzuni situlichile, situlichile huzuni.* (Abdulaziz 1979)

Pili, mtunzi anadhihirisha mtindo huu kwa kucheza na maneno kwa kuyageuza katika shairi. Haya yamo katika ubeti mzima au katika mshororo tu. Mifano mingine ;

Shairi la '*oa*' ukurasa 184, neno /oa/ limegeuzwa kutengeneza jina unoweze na pia unowezapo : *oa, unoweze nami, unowezapo t'akoya* (ubeti 7)

Shairi la '*Mapisi yalipisile*' ukurasa 124. Mtunzi anageuza neno mapisi kutengeneza neno yalipisile ili kumaanisha yaliyopita. Shairi la '*wajuvywa hawajajuvile'* katika ukurasa 143 pia linachukua huu mtindo. Vilevile, kuna shairi la '*Nishikapo nishikile'* ukurasa 316. Mtunzi pia anabadilisha nishikapo na kuunda neno nishikile lenye maana ya kushikilia.

Shairi la '*Ba cheni, mngwa !'* ukurasa 286 pia lina huu mtindo. Hapa anabadilisha neno hutendeka na kuwa na neno vikitendeka kama ifuatavyo katika ubeti wa pili.

*Ni watenzi wachangamwe <u>hutenda vikitendeka,</u>*

*Wajipatishile sime zatinda kama kitoka,*

*Ni kweli wake si wamwe, siombe wakipotoka,*

*Ba Cheni walimshika wakimtinda mngwa!* (Abdulaziz 1979)

## 4.2 Mitindo katika *Utenzi Wa Mwanakupona* Ilivyojitokeza Kusababishwa na Itikadi za Mtunzi

### 4.2.1 Jinsi Itikadi ya Utiifu Wa Mwanakupona ilivyopelekea Mitindo

Itikadi ya utiifu katika utenzi wa Mwanakupona inaathiri mtindo wa mtunzi kwa kiasi kikubwa. Mwanakupona anaamini kuwa mwanamke anapaswa kuwa mtii kwa mumewe, familia yake na jamii. Itikadi hii inaathiri jinsi anavyotumia lugha, mtindo wa mawaidha, urudiaji wa maneno na matumizi ya mifano, ili kupitisha wosia kwa bintiye. Itikadi hii inaathiri uteuzi wa mtindo ifuatavyo;

#### 4.2.1.1 Mtindo wa Mawaidha au Didatiki

Mtindo huu unamaanisha utunzi uliona dhamira ya kufundisha, kuelekeza au kutoa mafunzo. Katika fasihi, hususani katika ushairi na maandishi ya kifasihi, didatiki inahusu kazi za fasihi zenye lengo la kutoa mafunzo ya maadili, elimu au mafundisho fulani ya kijamii. Mwanakupona anatumia mtindo wa kuagiza na kueleza, akitoa mawaidha ya moja kwa moja kuhusu utii wa mwanamke.

Mtunzi anaanza kwa kumshauri bintiye amkaribie ili aweza kusikia wosia na kuuzingatia. Anamwambia atilie mawaidha yake maanani ili aweze kuepuka balaa katika ubeti wa 7. Hapa mtunzi anasisitiza kwa binti yake asikilize maneno yake kwa makini. Hapa inadhihirika kuwa utiifu kwa wazazi lilikuwa jambo muhimu sana katika jamii ya Mwanakupona ndiposa kupitia itikadi hii ya utiifu inampelekea kumwambia bintiye kuwa kumsikiliza mzazi wake ni hatua ya kwanza ya kuwa mke mwema.

Mwanakupona anaendelea anamshauri bintiye kuzingatia na kutii mafunzo ya dini ya Kiislamu. Anamwambia amtii Mungu na Mtume wake, apende na atende haki kama

inavyotafsirika kidini na kumtii mumewe na kuishi naye kama dini inavyoagiza. Haya yanapatikana katika ubeti wa;

*la Kwanda kama dini*
*Faradhi usiikhini*
*Na sunna ikimkini*
*Ni wajibu kuitia (Mwanakupona 1858, ub 12)*

*Mama pulika maneno*
*Kiumbe ni radhi tano*
*Ndipo apate usono*
*Wa akhera na dunia (Mwanakupona 1858, ub 22)*

*Nda Mngu na Mtumewe*
*Baba na mama wayuwe*
*Na ya tao nda mumewe*
*Mno imekaririwa. (Mwanakupona 1858, ub 23)*

Hizo ndizo ngazi za mamlaka zinazotambuliwa kidini, kwani zimekaririwa na vitabu vya dini. Hapa mtunzi anakuwa ni mwangwi tu wa mawaidha haya na kuongeza ‘aya’ zake mwenyewe anapomshauri binti yake kuwa hata huko ahera mwanamume ndiye atakayeulizwa kama mkewe aende peponi.

Mwanakupona anazidi kumpa bintiye mawaidha ya jinsi ya kudumisha ndoa yake. Anamwambia ampe mumewe maakuli, amsugue mwili na pia kumuogesha (ubeti 33).

Pia, katika ubeti 28 anamwambia aketi na muewe kwa dabu, asimtie ghadhabu, akinena asimjibu na ajifunze kunyamaza. Katika ubeti 34 anaendelea kumshauri amnyoe mumewe nywele, amtengeneze sharafa na amfukize udi. Anamwambia kuwa anapaswa kumtii mumewe kwani ndiye atakaye chagua atakapoenda afapo. Anasema;

*Kipenda wende peponi*

*Utakwenda dalhini*

*Kinena wende motoni*

*Huna bundi utatiwa. (Mwanakupona 1858)*

Vilevile, anaendelea kumpa mawaidha ya kutunza ndoa yake kutoka ubeti wa 37 hadi ubeti wa 52. Anapelekea kumtolea mfano wake mwenyewe katika ndoa yake. Katika ubeti wa 52 anamwambia, katika ndoa yake Mwanakupona na baba yake binti Mattaka, waliishi kwa vicheko na furaha na hawakuvunjiana heshima. Mtunzi anasema;

*Alinioa babako,*

*Kwa furaha na ziteko*

*Tusondoleane mbeko*

*Siku zote twaiokaa. (Mwanakupona 1858)*

Itikadi tuliyoiona hapa ni ile ya kukubali na kuheshimu ngazi za mamlaka kama zilivyo, bila kuzisaili. Hii ni sababu ni amri ya Mungu na pia utamaduni. Hivyo, itikadi ya utiifu ilichangia pakubwa mtindo wa mawaidha.

**4.2.1.2 Uradidi**

Mwanakupona katika utenzi wake pia anatumia mtindo wa urudiaji ili kusisitiza utiifu. Anarudia maneno na dhana muhimu ili kuhakikisha ujumbe wake wa utii unakaa akilini

mwa msomaji.

Katika beti nyingi, Mwanakupona anatumia maneno yanayorudiwa ili kusisitiza umuhimu wa jambo fulani ili kumfanya bintiye atii anayoyasema.

Ubeti 6 :

*Mwanaadamu si kitu*

*Na ulimwengu si wetu*

*Walau hakuna mtu*

*Ambao atasalia. (Mwanakupona 1858)*

Hapa mtunzi anamshauri bintiye asikilize kwa kina anachomwambia. Katika ubeti wa 5 anasema kuwa alitangaze jina la Mola muweza kwani ndiye mwenye wingi wa neema ili aweze kumjalia. Ndipo anasisitiza katika ubeti wa 6 kuwa mwanadamu si kitu na ulimwengu si wetu. Hapa anatumia /si/ kuleta ule uradidi. Anasema kuwa aamini Mola na radhi zake tano (ubeti 7) kwani hakuna ambaye atakayeishi milele. Katika mshororo wa tatu na nne ubeti wa sita anasema kuwa hakuna mtu ambaye atakayesalia ulimwenguni. Hapa anasisitiza utiifu wa mawaidha anayosema.

#### 4.2.1.3 Matumizi ya Vina na Mizani

Mwanakupona pia anahakikisha kuwa vina na mwisho na mizani vinaendana ili kuongeza nguvu kwa ujumbe wake wa utiifu.

**Urari wa vina:** Vina ni ule mpangilio wa sauti za mwisho wa mistari ya shairi ili kupata urari wa sauti za shairi. Katika *Utenzi wa Mwanakupona*, vina vinadumisha mtiririko wa utenzi na kuongeza ladha ya kisanaa. Haya yanapelekea mawaidha yake kueleweka kwa uwazi na pia kusisitiza utiifu wa anayoyasema.

Mtunzi anatumia vina vya mwisho. Vina hivi vinaleta urari wa sauti. Mwanakupona

ametumia vina vya kurudiarudia mwishoni mwa kila mstari ili kutengeneza mwangwi mzuri wa kisauti ili mawaidha yake yaweze kueleweka kwa msomaji. Mfano ;

*Twaa nikupe hirizi*

*Uifungeto kwa uzi*

*Uipe na taazizi*

*Upate kuyangalia. (Mwanakupona 1858, ubeti 8)*

Katika mfano huu, vina vya -zi- vimetumika ili kusisitiza utiifu wa anayoyasema. Katika ubeti huu, mtunzi ameweza kueleweka kwa uwazi anachosema hivo wosia wake kueleweka vizuri. Anasema kuwa bintiye aufuate yale mawaidha yake. Anamwambie aelewe anachosema na kuwa maneno yake ni kama hirizi. Aifunge kwa uzi, aipe utukufu na apate kuangalia. Yaani, afuate na atilie anayosema maanani. Haya pia yanapatikana katika beti kama 13 ;

*Pili uwe na adabu*

*Na ulimi wa thawabu*

*Uwe mtu mahabubu*

*Kula utakapoingia (Mwanakupona 1858)*

Hapa kuna urari wa vina vya mwisho -bu-. Mtunzi anatumia vina hivi ilikusisitiza kuwa bintiye awe na adabu na awe, ulimi wa kunena yanayofaa na mwenye kupendeka na watu. Katika ubeti 19, mtunzi anarudia vina vya mwisho -na-. Anasema kuwa bintiye asiwe mtu wa kuamini mambo asiyoyaona, wala asichukue maoni ya kudhania na tena atahadhari kusengenyana. Hapa mtunzi anatumia urari huo wa vina ili ujumbe wake kuweza kueleweka kwa uwazi.

Katika ubeti 33, pia kuna urari wa vina vya mwisho – li-. Anamshauri bintiye asichelewe

kumpa mumewe maakuli na asikose kumtunza mwili. Hapa mwanakupona anatumia vina hivyo vya mwisho ili ujumbe wake wa mke kumtunza mume kuweza kueleweka kwa uwazi.

Katika ubeti 27 na 28 pia, mtunzi ametumia vina vya mwisho -ni- na -bu-. Vina hivi vimefanya bei hizo kueleweka kwa uwazi. Ikiwa na maana ya kuwa bintiye amheshimu mumewe kwa akipende aende peponi anakwenda mara moja. Na akisema aende motoni ataende. Katika ubeti 28 anasema kuwa Binti Mattaka aketi na mumewe kwa adabu, asimtie ghadhabu na akinena asimjibu. Ikiwa na maana ya kuwa amsimjibu mumewe isivyovyaa ama kwa ukali. Vina hivi vya mwisho miongoni mwa mifano mingine, ni baadhi ya mifano ambayo mtunzi anatumia katika kazi yake ili kupelekea muundo wa kushikamana katika mistari yake ili ujumbe wake kueleweka. Kufuatia uandishi wa shairi za Kirasimi, vina vilitumika sana katika uandishi na haya yalidhihirisha kuwa Mwanakupona alitii uandishi wa kipindi chake. Pia, vina hivi vilihakikisha kuwa ujumbe wake ulijitokeza na kueleweka ipasavyo.

**Mizani:** Mizani katika kazi ya Mwanakupona ilipelekea ujumbe kusisitizwa kwa uzuri wa kisanaa. Haya hupelekea kuongeza nguvu mawaidha au ujumbe anaopitisha wa utiifu. Mizani ni mpangilio wa idadi ya silabi katika mshororo wa shairi (BAKITA, 2015). Mtunzi anahakikisha kuna mpangilio bora wa vipande vya maneno ndani ya kila mstari wa shairi ili kuleta urari wa kisanaa. Mwanakupona anafuata muundo wa utenzi wa Kiswahili wa kisanaa kwa kutumia mizani yenye idadi sawa ya silabi kwa mistari mingi. Jambo hili limepelekea uwiano wa sauti na mtiririko wa kifasihi. Mfano;

*Pete sikose zandani*

*Hina sikome nyaani*

*Wanda sitoe matoni*

*Na nshini kuitia (Mwanakupona 1858, ubeti 41)*

Hapa mtunzi anatumia mizani 8 katika kila mshororo ili kuleta urari wa mawazo na ujumbe kueleweka. Mizani hii husaidia kuendeleza mtindo wa utenzi kwa kulinganisha vipande vya mawazo katika mistari tofauti. Pia, urari huu wa vina umefanya shairi lake kuwa na mwangwi wa kifasihi wa kuvutia. Haya yalisisitiza utiifu katika utenzi wake.

### 4.2.2 Itikadi Ya Taasubi Ya Kiume Na Itikadi ya Ukawaida

#### 4.2.2.1 Lugha ya Kinaya

Kinaya ni hali inayotokea tofauti na matarajio ambayo sanasana hutumika kumtania mtu (BAKITA, 2015). Mwanakupona anatumia kinaya katika lugha yake ili kupitisha itikadi yake ya utii kwa bintiye bila kuyafanya anayoyasema yakae yanamkandamiza yeye kama mwanamke. Anatumia lugha ya kinaya ili kumfanya bintiye aone ushauri wake wote katika utenzi kama matukio ya kawaida katika jamii kisha yeye mwenyewe ayafuate. Anafikia kiwango cha ata kumtolea mfano wake yeye mwenyewe katika ndoa yake ili kuyafanya yakae masuala ya kawaida. Haya yalionyesha kuwa Mwanakupona aliongozwa pakubwa na itikadi ya ukawaida na pia taasubi ya kiume.

Mwanakupona anatumia kinaya ili kuonyesha hali aliyoko mwanamke katika ndoa, akionekana kushauri utii wa hali ya juu wa mume, Lakini kwa undani anaonyesha hali ya unyenyekevu wa kupitia kiasi kama njia ya kuficha changamoto za mfumo dume. Hapa mtunzi aliongozwa na itikadi ya ubabedume anamlimbikizia mwanamke chungu mzima bila kutaja majukumu ya mwanmme. Pia utenzi mzima ulithihirisha itikadi ya ukawaida kwa kutuchorea kila kitu kama ukawaida katika jamii uliofaa kufuatwa bila kupinga chochote. K.m Mwanakupona anamwambia bintiye afuate ujumbe wake kuhusu ndoa ili

kusimamaisha ndoa na kuwa na maisha mema.

Mwanakupona kwa kiasi kikubwa anamshauri binti yake kuwa awe mtiifu kwa mume hata wakati wa dhuluma. Hapa mtunzi anapiga debe utiifu wa mwanamke lakini kwa kweli anafichua jinsi wanawake wanavyotakiwa kujinyima na kustahimili hata hali zisizofaa. Hapa kinaya kinajitokeza kwani mwanamke anaendeleza mambo yanayoonekana kuikandamiza jinsia ya kile. Hapa Mwanakupona alitawaliwa na ubabedume na hata ukawaida. Wosia wake umejaa mawaidha ya kutii mume katika ndoa, kuendeleza amani katika ndoa, kumnadhifisha mume na ata anakiri kuwa mume ndiye anayeamua hatima ya mwanamke. Anachora hayo yote kama masuala ya kawaida katika jamii ambayo yanastahili kufuatwa sababu ni mambo aliyopata yakiendelezwa. K.m, anapomtolea mfano wake halisi wa jinsi ndoa yake ilivyokuwa na alivyoishi na mumewe. Haya yanapatika kwa uwazi kutoka ubeti 24 hadi ubeti 52. Mfano;

*Keti naye kwa adabu*
*Usimtie ghadhabu*
*Akinena simjibu*
*Itahidi kunyamaa (Mwanakupona 1858, ubeti 28)*

Hiki ni kinaya katika maisha ya ndoa kwani wapenzi wafungapo ndoa, wanapaswa kupendana kwa dhati na kuishi pamoja hadi wafapo. Hii inaonyesha kukubaliana katika kila jambo kama mume na mke. Hivyo basi kila mmoja anastahili kuwa na uhuru wa kuzungumza maoni na hisia zake. Ujumbe mwingi unaosisitizwa katika utenzi huu unaonyesha unyanyasaji wa wanawake ndani ya ndoa, kwa kuwa inamfanya mwanamke kudhulimiwa kimya kimya huku akionekana kuwa mwema.

Mulokozi (1999), anaonyesha jinsi utenzi huu umeibua mijadala mingi miongoni mwa

wanataaluma wa Kiswahili. Anasema kuwa kuna tapo la kwanza ambalo linaakisi kuwa Mwanakupona anadhalilisha mwanamke, anamgeuza pambo na mtumishi wa mwanamume na hivyo kuendeleza itikadi ya taasubi ya kiume katika jamii. Mulokozi amewataja wanataaluma kama Mulokozi (1982). Ndulute (1987) na Senkoro (1988) ambao wanaafikiana na hilo. Vilevile, unyanyasaji huu wa mwanamke tunapata Mwanakupona akiuona kama ukawaida katika jamii na anayapitisha yale yale kwa bintiye. Haya yaliendelezwa kwani jamii ya wanawake wa Uswahilini iliitikia vizuri wito huu wa kuugeuza utungo huu kwa badala ya asasi ya kale ya unyago na kukaririrwa na wanawake wengi katika upwa wa Kenya (Mulokozi, 1999). Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa mtunzi alitumia kinaya kwa upana katika utenzi wake ili kufanya mambo yanayodhihirisha dhuluma kwa mwanamke kuwa mambo yasiyomdhulumu mwanamke. Mifano zaidi ni kama;

Katika ubeti 31, anamshauri bintiye ampee mumewe upepo ili alale. Hapa mwanamke kumfanyia mumee hivi ni kama kumtumikisha na kumkosea heshima kwa kumwonyesha kuwa mume ndiye muhimu. Haya ni kinyume na matarajio ya jinsi ndio inavyopaswa kuwa.

*...kilala siikukuse*
*Mwegeme umpapase*
*Na upepo asikose*
*Mtu wa kumpepea. (Mwanakupona 1858, ubeti 31)*

Katika ubeti 34, Mwanakupona anazidi kumshauri bintiye amnyoe mumwe ndevu. Haya ni kinyume na matarajio kwani mume anastahilii kujifanyia mwenyewe. Mume anapoota ndevu anapaswa kujua jinsi ya kujinadhifisha kwa sababu hilo halimuhusishi mke. Lakini

tunapata Mwanakupona akiendeleza itikadi potofu za kunyoa ndevu, kumuongesha mume, kumtengeneza sharafa, kumfukiza udi asubuhi na jioni, kumtunza kama kijana mchanga, kumpumbaza apumbae, kutii amri za mumena afanyapo hapo, Mungu atamlipia (ubeti 34 hadi 36). Mwanakupona anapomwambia kuwa Mungu atamlipia pia inadhalilisha mwanamke na kumyima haki kwa kutumia dini. Hapa dini ilitumika kama kizuizi cha kuuficha uovu unaofanyiwa mwanamke.

Vilevile, kinaya kinajitokeza kutoka ubeti 37 hadi 42. Hapa mwanamke anashauriwa kuwa msafi na kujipamba. Haya ni ili kumfurahisha mumewe. Mwanakupona anamwambia ajipambe na avae vizuri kama siku ya harusi (ubeti 39). Anamshauri miguu atie kugesi na mikono atie makoa. Anaendelea kumwambia avae kidani na kibano katika shingo, apake marashi na daiia, avae pete vidoleni, apake hina kwenye kucha za mikono, awe na wanda machoni na pia kunadhifisha nyumba. Hili lote ni ili kumfurahisha na kumvutia mume ila hafanyi haya yote ili kufurahia urembe wala usafi wake. Mwanakupona hajataja mahali popote kuwa Mwanamke anakuwa nadhifu ili kujifurahia yeye mwenyewe.

Katika ubeti 44, pia mwanamke anachorwa kama ambaye hana uhuru.

*...Na ukitaka kutoka*
*Sharuti rukhusa taka*
*Wonapo meudhika*
*Rudi na kuikalia... (Mwanakupona 1858)*

Katika huu ubeti Mwanakupona anamshauri bintiye kuwa akitaka kutoka kwenda nje amuombe mumewe ruhusa. Akiona mume ameudhika na jambo hilo, asibishane naye wala kwenda cha lazima, bali arudi nyumbani na kujikalia. Hapa mwanamke hapaswi

kutoka bila ruhusa ya mumewe. Na iwapo mumewe anakataa atoke basi arudi kwa utulivu nyumbali. Haya yalidhihirisha kinaya kwani Mwanakupona ndiye anayendeleza imani potofu zinazomdhalilisha mwanamke ingawa pia yeye ni mwanamke. Hivyo kutokana na itikadi za taasubi ya kiume na ukawaida, ni dhahiri kuwa itikadi hizi zilipelekea mtunzi kutumia mtindo wa kinaya katika utenzi wake.

#### 4.2.2.2 Matumizi Ya Taswira

Katika utenzi wa Mwanakupona, mtunzi ametumia taswira kwa ustadi ili kuwasilisha mafunzo yake kwa bintiye, huku akionyesha nafasi ya mwanamke katika ndoa na jamii. Mwanakupona ametumia taswira ili kutuchorea picha halisi ya jinsi mwanamke alivyopaswa kudumisha ndoa yake kwa kumtii mume, jinsi ya kudumisha amani katika ndoa na ata jinsi mwanamke Mwasihili alivyopaswa kuwa katika jamii husika. Vitushi hivi vinapelekea kutuonyesha jinsi mwanamke alivyonyanyaswa na dini na utamaduni husika bila yeye kujua kiasi cha kuendeleza hayo kwa bintiye katika jamii ilivyojaa ubabedume. Taswira hizi ziliweza kuongeza uzito wa maana na hata kusaidia bintiye Mattaka na hata msomaji au msikilizaji kuelewa maadili yayosisitizwa.

**Taswira ya ufalme na utumwa:**

Mwanakupona anatumia taswira ya mume kama sultani na mke kama mtumwa ili kuonyesha mamlka aliyonayo mume katika ndoa. Hii inatoa picha ya mume kama mtawala mwenye mamlka na mke kama mwatawala na uhuru, akisisitiza utii wa mwanamke kwa mumewe. Hapa yanajitokeza pale Mwanakupona anasisitiza mwanamke amtii mume wake katika ndoa kiasi cha utii huu kuwa miongoni mwa radhi tano za Kiislamu. Pia tunapata Mwanakupona akisema kuwa mwanamume ndiye atakaye chagua

hatima ya mwanamke. Akitaka aende peponi ataenda na akitaka aende motoni ndiko mwanamke atakoenda. Hapa Mwanamke anachorwa kama kiumbe duni kisicho na uwezo na kilichopewa nafasi chini ya mwanamume.

Tunapata Mwanakupona akiendelea kutoka ubeti wa 51 hadi 56 kumchorea taswira ya jinsi waliishi ya baba yake. Anamwambia bintiye kuwa amuige mama yake alivyoishi na mumewe kwa miaka kumi bila ugomvi wa aina yoyote kwa kuwa alifuata mawaidha anayoyasema. Anasema kuwa babake alipomuoa Mwanakupona, waliishi kwa furaha na vicheko. Hawakuvunjiana heshima siku zote walizokaa. Hawakuteta na hawakuwaa na ovu lolote. Na anamwambia kuwa hataki kusikia ovu katika ndoa yake. Hivyo mwoyo wake Mwanakupona utatosheka kwani bintiye amefuata mawaidha ya mama yake. Anamalizia katika ubeti 56 kwa kusema kuwa watu wakisikilizana milele hukumbukana na vilevile watu katika ndoa wakishindana watajijutia daima. Taswira hii ilitumia na mtunzi ili kutilia mkazo anayoyasema kwani bintiye amefanywa kuona kuwa yale mawaidha kama ukawaida katika ndoa.

**Taswira ya mwili na urembo :**

Mwanakupona anatumia taswira ya mwili na urembo kuelezea jinsi mwanamke anavyopaswa kujiheshimu na kujitunza kwa ajili ya ndoa yake. Anaambiwa asafishe nguo zake na kujipamba. Mtunzi anamshauri bintiye katika ubeti 37 asiupuuze usafi wa choo. Katika ubeti 38 anaendelea kumwambia aoge na kujisugua, afunge nywele, aeke asmini na kutia firashani kweye matandiko. Kutoka ubeti 39 hadi 41 Mwanakupona asema bintiye aeke mapambo kama vile kugesi kwenye miguu, makoa kwenye mikono, kidani na kibano kwenye shingo, pete vidoleni, hina kwenye kucha za mkono, wanda machoni na pia kupaka marashi na daiia. Katika ubeti 42 anaendelea kumshauri bintiye kuwa

nyumba iwe nadhifu. Hii inatoa picha ya mwanamke anayevutia na mwenye heshima kwa kuvaa nguo safi na kujisitiri. Inaonyesha umuhimu wa mwanamke kuwa msafi, kuvaa nguo safi na kujipamba ili aweze kumvutia mumewe na huu usafi umechorwa kama ukawaida unaopaswa kufuatwa na wanawake.

**Taswira ya chakula na mapishi :**

Mwanakupona anatumia picha ya chakula na mapishi kuonyesha wajibu wa mwanamke katika kuhakikisha nyumba yake ni mahali pa amani na starehe kwa mume wake. Mtunzi anasema :

*...Chamka siimuli*

*Mwandikie maakuli*

*Na kumtunda muili*

*Kumsinga na kumwoa* (Mwanakupona 1858, ubeti 33)

Taswira hii inatoa picha ya mwanamke anayepika na kumkaribisha mume wake kwa furaha, akionyesha umuhimu wa huduma katika ndoa. Anamwambia bintiye ampe mumewe chakula na asimcheleweshe maakuli. Anazidi kusema mume akaribishwe na amani na bashasha. Haya yanaonyesha uhusiano kati ya upendo wa mke na matendo yake ya kumhudumia mume. Yaani, kama mke anampenda mumewe basi anatarajiwa kuhudumia mumewe kwa furaha na amani, kama vile kumwandalia chakula bila kuchelewa.

Taswira hizi zilipelekea kulainisha lugha. Ina maana ya kuwa zinarahisisha kuelewa yale mawaidha kwa njia ya picha zinazoeleweka kwa msomaji. Pia, taswira zinazidisha mivuto ya kisanaa. Taswira hapa ilitumika kufanya utenzi kuvutia na wenye ladha ya kifasihi. Tena, taswira ilionyesha hali halisi ya maisha kwa kutumia taswira halisi kama

chakula, ufalme, urembo, nafasi ya mwanamke na majukumu yake katika jamii. Hapa Mwanakupona alihusisha mawaidha yake na maisha ya kila siku ya jamii babedume. Haya ni kupitia yale ambayo anayaona kuwa matukio ya kawaida katika jamii bali hayafasiri kama matukio ya kumkandamiza mwanamke. Hivyo ni wazi kuwa itikadi ya ukawaida ilimwongoza Mwanakupona katika matumizi ya taswira. Mtunzi anachora ujumbe kama ukawaida uliozoeleka katika jamii ambao unapaswa kutiliwa maanani, kujulikana na kila mwanamke na kufuatwa. Anatumia mawaidha yake kuonyesha namna mazingira yake yalikuwa bila kuonyesha kama ulimwengu unaomkandamiza au kumnyanyasa mwanamke.

**4.3. Ulinganishaji wa jinsi itikadi za watunzi zilivyopelekea mitindo vitofauti.**

Muyaka bin Haji na Mwanakupona binti Msham walitumia mitindo tofauti katika mashairi yao kutokana na itikadi mbalimbali zilizowaongoza. Haya yalisababishwa na mazingira yao ya kijamii. Muyaka kutokana na itikadi ya uhuru alitumia mtindo wa kipokeo pale ambapo alisisitiza jambo muhimu. Pia aligonganisha wahusika kihalisia ili dhana yake kueleweka kwa uwazi. Muyaka pia alitumia lugha iliyosheheni matumizi ya picha au taswira ili jambo kueleweka. Itikadi ya mapinduzi ya Muyaka pia ilipelekea upekee wa mtunzi kupitia mtindo wa matumizi ya maneno ya kilahaja na hata matumizi ya lugha za kigeni. Haya yalitokana na watu aliotangamana nao wakati wake. Umaarufu huu ulimfanya mtunzi kuweza ata kuchanganya lugha husika katika kazi zake. Vilevile, itikadi hii ya mapinduzi ilimfanya Muyaka kutumia mtindo wa kipekee wa kudokeza dhana muhimu katika mstari wa mwisho wa ubeti kando na Mwanakupona ambaye dhana zake ziko wazi katika mistari yote katika utenzi wake. Pia, itikadi ya mapinduzi ilimfanya mtunzi kutumia mtindo wa kipekee wa mashairi mafupi huku Mwanakupona akitumia

utenzi mmoja wenye beti 102. Itikadi ya mapinduzi vilevile ilipelekea mtundo wa lugha tamathali za usemi kama takriri, tashbihi, tashbiha na tanakali za sauti. Lugha yake ni rahisi ili kueleweka na ni ya moja kwa moja, yenye msamiati wa mitaani.

Kwa upande mwingine tunapata kuwa Mwanakupona alitumia lugha rasmi yenye heshima na taadhima. Itikadi ya utiifu ya Mwanakupona ilipelekea mtindo wa didatiki kwani ulisheheni mawaidha au wosia, mtindo wa uradidi wa maneno au dhana muhimu na pia mtindo wa urari wa vina na mizani ili kuleta uelewa wa anayoyasema kwa bintiye na hata hadhira lengwa. Itikadi ta taasubi ya kiume na hata ukawaida ya Mwanakupona pia ilipelekea mtindo wa lugha ya kinaya ili ananyoyasema kuonekana kama mazoea na kukubalika na hadhira yake bali yasionekane kama mambo makali kwa jinsia ya kike na kutupiliwa mbali. Upekee huu ulijitokeza katika utenzi wake na hatuupati katika mashairi ya Muyaka kwani Muyaka anasema mambo kwa uwazi na kusisitiza mapinduzi dhidi ya watawala wa jamii na maovu katika jamii. Mwisho, itikadi ya taasubi ya kiume na ukawaida ilipelekea mtindo wa matumizi ya taswira pia kwa hali ya juu ili kusisitiza imani ya maadili ya ndoa na nafasi ya mwanamke. Huku Muyaka akishughulikia masuala mengi kwa jumla yakiwemo masuala ya kijamii, kisiasa na hata mapenzi. Mwanakupona kupitia taswira alituchorea mafunzo ya kujamii ya heshima na nasaha. Ilhali Muyaka kazi yake inasheheni kazi za kihisia, zenye ukosoaji wa wazi. Ingawa wote wawili wanatumia vina, mizani, taswira, Muyaka alitumia mashairi kama silaha ya ukosoaji, wakati Mwanakupona alitumia utenzi wake kama chombo cha mafundisho na maadili. Hivyo, ilibainika kuwa watunzi hawa wawili waliongozwa na itikadi tofauti katika kazi zao. Vilevile, hizo itikadi ziliathiri pakubwa uteuzi wa mitindo ili kazi zao kueleweka na hadhira zao kwa urahisi ingawa walikuwa watunzi wa kipindi kimoja.

## 4.4 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kubainisha namna ambayo itikadi za Muyaka na Mwanakupona zilivyopelekea mitindo yao vitofauti. Watunzi hawa wote ni wa kipindi kimoja cha uandishi lakini matukio ya maizngira yao yanaonekana kuwa tofauti.

Sura iliyofuata ilishughulikia mukhtasri, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Katika sura ya nne, mtafiti alionyesha jinsi itikadi zinavyoathiri mitindo ambayo ilitumika na Muyaka katika mashairi yake na pia Mwanakupona katika utenzi wake. Ilibainika kuwa watunzi hawa waliathirika pakubwa na imani, mitazamo na pia mawazo mbalimbali, na haya yalipelekea kazi zao kuwa na utofauti ingawa walikuwa watunzi wa kipindi cha kirasimi.  Katika sura hii mtafiti alijadili muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, matokeo na kueleza mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusu itikadi, mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*.

### 5.1 Muhtasari Wa Tasnifu

Katika tasnifu hii, mtafiti alichanganua na kulinganisha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona.* Katika sura ya kwanza, mtafiti alijadili utangulizi wa utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Alionyesha swali ambalo alishughulikia katika utafiti ambapo alichunguza itikadi na utofauti wa kiitikadi unaojitokeza katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Aliweza kubaini kuwa watunzi hawa wawili waliathirika pakubwa na itikadi zinazowaongoza na pia kuna tofauti za kiitikadi na zinaathiri maudhui na mtindo, ingawa walikuwa watunzi wa kipindi cha kirasimi (Gibbe, 1993,25).  Aidha, mtafiti alijadili upeo na mipaka ya kazi hii ambapo alibaini kuwa mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* ndizo kazi mwafaka katika kufanya utafiti huu kwani zilikuwa kazi za kipindi kimoja na tena zimeandikwa na jinsia tofauti. Malengo ya utafiti pia yalishughulikiwa ambayo ni kuonyesha utofauti wa kiitikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* na kuonyesha jinsi itikadi husika

zilivyowaathiri Mwanakupona na Muyaka katika uwasilishaji wa maudhui na pia kuonyesha jinsi itikadi husika zilivyowaathiri Mwanakupona na Muyaka katika uwasilishaji wa mtindo.

Katika sura ya pili mtafiti alichanganua na kulinganisha itikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*. Ilibainika kuwa kuna utofauti wa kiitikadi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona* na uchanganuzi huu ulifuatia nadharia ya Kiitikadi ; mrengo wa Karl Marx (1977), Louis Althusser (1981) na pia Antonio Gramsci (1981). Ilibainika kuwa Muyaka aliongozwa na itikadi ya uhuru kwa kushughulikia masuala mbalimbali yaliyoko katika mazingira yake. Muyaka pia alionyesha itikadi ya ukandamizaji kwa kushughulikia jinsi kikundi kimoja kulinyimwa haki na wengine. Mwisho, Muyaka alidhihirisha itikadi ya mapinduzi ya nguvu pale alishughulikia mivutano ya kisiasa, mivutano baina ya miji na jinsi za kujinasua kwa mikono ya mkoloni. Mwanakupona naye, ilibainika kuwa aliongozwa na itikadi ya utiifu kwa utiifu wake wa hejemonia ya dini, utamaduni, ndoa na familia na jinsi alivyoichora fasihi yake. Isitoshe, itikadi ya taasubi za kiume na ukawaida ziliweza kubainika kwa jinsi alivyochora mawaidha yake kwa bintiye kama masuala ya kawaida katika jamii ambayo yalifaa kufuatwa bila pingamizi. Mwanakupona aliitwika jinsia moja majukumu mengi bila kumpa mwanamme jukumu lolote. Mfano, mwanamke ameshauriwa kuitii dini ili awe na maisha mema ya peponi na ili adunishe amani katika ndoa na jamii.

Katika sura ya tatu mtafiti alichanganua jinsi itikadi husika zilivyowaathiri Muyaka na Mwanakupona katika uwasilishaji wa maudhui. Mtafiti alionyesha jinsi itikadi ziliwaathiri watafiti vitofauti katika uteuzi wa maudhui kwani Muyaka aliathirika na itikadi ya ukandamizaji kuteua maudhui ya tamaa, utabaka na magonjwa na kifo na

umasikini. Itikadi ya mapinduzi ya nguvu pia ilichangia maudhui ya uzalendo na vita na itikadi ya uhuru ilipelekea maudhui ya mifumo ya kiuchumi, usaliti katika ndoa na mapenzi ya dhati. Mwanakupona naye aliathirika na itikadi ya utiifu ambayo ilipelekea maudhui ya utii wa dini, utamaduni na mahusiano katika jamii. Pia kuna itikadi ya taasubi ya kiume na itikadi ya ukawaida ambayo ilipelekea kuteua maudhui ya ndoa na familia, utamaduni na dini. Hivyo Mwanakupona na Muyaka waliathirika na itikadi vitofauti kwani walieleza masula vitofauti. K.m Mwanakupona anazungumzia utii ya ndoa lakini Muyaka anazungumzia usaliti katika ndoa. Muyaka pia anazungumzia vita, uongozi na mifumo ya kiuchumi ilihali Mwanakupona alishughulikia utii wa dini, utamaduni na ndoa.

Katika sura ya nne mtafiti alijadili jinsi itikadi zilivyowaathiri Muyaka na Mwanakupona katika uteuzi wa mtindo katika kazi zao. Vilevile, mtunzi aliweza kubaini tofauti za kimtindo zilizojitokeza katika mashairi ya Muyaka na katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Iliweza kubainika kuwa itikadi ya uhuru wa Muyaka iliyomwongoza mtunzi, ilipelekea uteuzi wa mtindo wa matumizi ya kipokeo, kugonganisha wahusika na matumizi ya taswira. Vilevile, itikadi ya mapinduzi ilipelekea mtunzi kuteua mtindo unaosheheni matumizi ya lugha iliyosheheni maneno ya kilahaja na lugha za kigeni. Pia itikadi hii ilipelekea uteuzi wa mtindo wa udokezi wa dhana mahususi katika mstari ya mwisho wa ubeti, mtindo wa kutumia nafsi zote na wahusika wasio hai, mtindo wa mashairi mafupi, mtindo wa maneno katika ukwapi kugeuzwa katika utao na pia matumizi ya tamathali za usemi kama tashhisi, tashbihi na tanakali za sauti. Kwa upande mwingine, Mwanakupona aliathirika na itikadi ya utiifu ambayo ilipelekea mtindo wa urudiaji na mtindo wa vina na mizani. Itikadi ya taasubi ya kiume na ukawaida vilevile ilipelekea mtindo wa kinaya

na taswira. Hivyo, ilibainika kuwa itikadi za Mwanakupona na Muyaka ziliathiri pakubwa uteuzi wa mitindo ili kazi zao kueleweka na hadhira zao kwa urahisi ingawa walikuwa watunzi wa kipindi kimoja. Hii ni sababu waliathirika na mazingira yao kwa namna tofauti.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti alidhamiria kuyajibu maswali ; kulinganisha itikadi zilizowaongoza watunzi katika mashairi ya Muyaka na *Utenzi wa Mwanakupona*, jinsi itikadi husika zilivyowaathiri watunzi katika uteuzi wa maudhui yao na pia jinsi itikadi husika ziliwaathiri watunzi katika uteuzi wa mitindo yao. Mtafiti alionyesha kuwa Muyaka na Mwanakupona waliongozwa na itikadi tofauti. Itikadi husika zilipelekea uandishi unaolenga mambo tofauti na pia ziliathiri mitindo tofauti. Muyaka ilibainika kuwa mazingira yake yalisheheni masuala mengi kama vile vita na mapinduzi ya nguvu ya kiutawala, biashara, miongoni mwa mambo mengine, na haya yalipelekea utunzi ulioshughulikia masuala yote katika ulimwengu na mazingira yake, yaani mambo ya sokoni. Hii ikiwa na maana ya kuwa utunzi wake ulishughulikia mambo mengi ambayo mengi yalileta upekee ikilinganishwa na kazi zingine za kipindi cha kirasimi haswa utenzi wa Mwanakupona.

Kwa upande mwingine kuna utofauti kati ya Muyaka na Mwanakupona ambaye alithihirisha utiifu wa upana katika utenzi wake. Mwanakupona alifuata utunzi wa kirasimi. Maudhui makuu katika kazi yake ni kama vile utiifu wa dini na ndoa, jinsi ya kudumisha amani katika ndoa na pia mahusiano ya kijamii. Hivyo, Mwanakupona alimpa bintiye Binti Mattaka wosia wa kushika dini ya Islamu, kumtii mume pamoja, kumng’arisha na pia kudumisha amani katika ndoa. Mwanakupona aliendeleza itikadi

hizi za kibabedume kwa kumuonyesha bintiye kuwa anayoyasema ni mambo ya kawaida na ambayo yalikubalika katika jamii husika, ambayo mwanamke anapaswa kufuata kwa utiifu bila kukiuka.

Itikadi za Muyaka zilipelekea mitindo ya kugonganisha wahusika, matumizi ya kipokeo, matumizi ya maneno ya kale, mashairi mafupi, matumizi ya nafsi zote na wahusika wasio hai na pia udokezi wa dhana muhimu katika mstari wa mwisho wa ubeti. Haya yalipelekea upekee wa utunzi wa Muyaka ikilinganishwa na kazi zingine za kirasimi na hata utenzi wa Mwanakupona. Mwanakupona tulipata itikadi zake zilipelekea mitindo wa mawaidha ya didatiki, uradidi wa dhana muhimu, urari wa vina na mizani na pia kinaya. Kutokana na hayo ilibainika kuwa watunzi hawa waliongozwa na itikadi tofauti na itikadi husika zilipelekea upekee wa kimaudhui na kimtindo ingawa walikuwa watunzi wa kirasimi.

### 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na matokeo ya utafiti huu mtafiti ameweza kutoa mapendekezo yafuatayo : Kwanza, kuna haja ya kufanya tahakiki za baadaye za fasihi zinazohusu itikadi, haswa katika mashairi, zinaweza kufanywa kuhusu tenzi za mwanzoni kama vile Fumo Liyongo (1913), Al-Inkishafi (1800), Vita vya wadachi kutamalaki Mrima (1895) na Vita vya majimaji (1910), na pia kuzilinganisha. Pili, mikabala mingine ya itikadi pia inaweza kutafitiwa ili kuona kama inajitokeza katika kazi hii. Utafiti pia unaweza kufanywa kuhusu vipengele vinginevyo kama ploti, muundo na mandhari na kuona namna vipengele hivyo vinaadhihiriwa na itikadi ya mtunzi. Tatu, tafiti zaidi pia unaweza kufanywa kuhusu *Utenzi wa Mwanakupona* kuhusu wataalamu wanaodai kuwa undani wa wosia wa Mwanakupona ni kuwa wanaume wamesawiriwa kama viumbe dhaifu na wapumbavu, wenye kupenda kuengwaengwa na kusifiwa, na mwanamke ni mwenye akili anayeweza kuwamudu na kuwatawala wanaume. Hivyo basi kuna haja ya tafiti

zingine zinazolenga sehemu hii.

## 5.4 Hitimisho

Utafiti huu umeshughulia mtazamo linganishi wa itikadi katika *Utenzi wa mwanakupona* na mashairi ya Muyaka. Imebainika kuwa itikadi zilizowaongoza Muyaka na Mwanakupona ni tofauti ingawa walikuwa watunzi wa kipindi kimoja cha urasimi mkongwe. Utofauti huu ulitokana na mazingira waliokuwemo watunzi. Vilevile, itikadi hizo tofauti zilipelekea uwasilishaji wa maudhui na mitindo kwa njia tofauti. Pia sura hii imetoa muhtasari wa yale mtafiti ameshughulikia katika kila sura ya utafiti. Pia imeweza kueleza matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti. Isitoshe, mapendekezo ya utafiti huu yalibainishwa ambapo tafiti zingine za baadaye ziliorodheshwa ili kuongeza maarifa zaidi.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (1973) *Sauti ya Dhiki*. Oxford University Press, Nairobi.

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry*. Kenya Literature Bereau, Nairobi.

Adler, N. (1997). *International Dimensions of Organizational Behavior*. (3rd ed). South- Western College Publishing, Ohio.

Allen, A.J.W & Thomas, T. (1936). *Swahili Poetry: A study in Structure and Form.* Oxford University Press, London.

Althusser, L. (1981). *Ideology and Ideological State Apparatuses.* Katika Lenin and Other Essays. (B. Brewster, Mtaf.). New Left Books, London.

Bakari, M. (1978). *The State of the Art: Swahili Literature in the Nineteeth Century*. Journal of Historical Association of Kenya.

Bakita (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Limited, Nairobi.

Beja, S. Karisa, B. S na Mwinyifaki, A (2017). *Iktibasi' katika Tenzi za Mwanakupona na Al- Inkishafi*. Kioo cha Lugha Juz. 11. Bureau, Nairobi.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Dar es Salaam.

Creswell, J.M (2014). Research designs: Qualitative, quantitative, and mixed method approaches (4th ed.) Thousand Oaks, CA: Sage.

Evans, M. O (2015). *Mamlaka ya itikadi katika Nyimbo teule za Taarab.* Tasnifu ya uzamili katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi. http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/93442/Makhulo,%20%20Evans%

Finnegan, R (1970). *Oral literature in Africa*. Oxford University press: Cambridge.

Gramsci, A. (1985). *Selections from Cultural Writings*. London: Lawrence and Wishart.

Gibbe, A. (1993). *Women and the Making of Literature in East Africa*. OSSREA, Addis Ababa.

Hegel, G. (1977). *Phenomenology of Spirit.* (A.V. Miller, Mtaf.). Oxford: Oxford University Press.

Hichens, W. (1939). *Swahili Literature and History*. Sheldon Press, London.

Hichens, W. (l940). *Diwani ya Muyaka*. University of Witwatersand, Johannesburg.

Hoare, Q na Smith, G. N (1971). *Selections from the Prison Notebooks of Antonio Gramsci.* Lawrence and Wishart, London.

Kenyatta, J. (1938). *Facing Mount Kenya: The Tribal Life of the Kikuyu*. Secker and Warbug, London.

Kezilahabi E. (1983). *The concept of The Hero in African Fiction.* Retrieved from: http://catalog.hathitrust.org/api/volumes/oclc/96

Khamis, A. (2016). *Utandawazi katika Utamaduni wa Vijana wa Kizanzibari*. Jana, 1(1), 1-16.

King'ei, G. K. (2007): "*Athari za Washairi Wakongwe juu ya Washairi wa Kisasa: Mfano wa Muyaka bin Haji na Ahmed Nassir*." Kioo cha Lugha, 5(1). Retrieved from https://doi.org/10.4314/kcl.v5i1.61426

King'ei, K. (2000). *Language in development research in 21st century Africa*. African Studies Quarterly, 3(3), 25-30.

Kombo, K. D. and Tromp, L. A. D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Pauline Publications Africa, Nairobi.

Kothari C. R (2004). *Research methodology: Methods and Techniques* (2nd ed.). New Delhi: New Age international publishers.

Leech, G. N. na Short, M. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. 2nd Edition Harlow: Longman Group Ltd.

Marx, K. (1977). *A Contribution to the Critique of Political Economy.* Progress Publishers, Moscow.

Marx, K. na Engels, F. (1977). *The German Ideology*. London: Lawrence and Wishart.

Masinde, E. (2003). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui.* Tasnifu ya Uzamifu katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mazrui na Syambo, B.K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mazrui, A. (2007). *Swahili Beyond the Boundaries*. Ohio University Press, Athens.

Mbaabu I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd, Nairobi.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili: Kenya.* Publishing and Book Marketing C.O ltd,

Mohammed, S.A (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi fupi*. E.A.E.P, Nairobi.

Momanyi, C (2012). *Usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili.*Tasnifu ya Uzamifu katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha kenyatta.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantative and Qualitative Approaches.* Act Press. Nairobi.

Mulokozi, M. M, Sengo, T. S. Y na Chuo Kikuu cha dar es Salaam. (1995). *History of Kiswahili Poetry*. a.d 1000- 2000: A report. Institute of Kiswahili research University of Dar es Salam.

Mulokozi, M.M. (1986). *The Nanga Epos of the Bahaya: A Case Study in African Epic Characteristics.* A PhD Thesis, University of Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1996). *Historia ya Fasihi ya Kiswahili*. DUP, Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. TUKI, Dar es salaam.

Munyole, S. D (2017). *Usomaji na ufasiri sasa wa Utenzi wa Mwanakupona.* Kutoka: http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/18245

Murithi, J (2018). *Uhusinao wa Itikadi na mtazamo wa mtunzi*. 23 (9), 75-83. Retrieved from:https://www.iosrjournals.org/iosrjhss/papers/Vol.%2023%20Issue9/Versio n 4/J2309047583.pdf

Murithi, J (2021). *Mtazamo linganishi wa muundo na maudhui ya Tenzi Mbili kuu za kale na ushairi wa Muyaka. Kiswahili.* 84 (1), 99-112. Retrieved: https://www.ajol.info>article>view

Murithi, J. (2017). *Itikadi Katika Riwaya za Said A. Mohamed*. Tasnifu ya uzamifu katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo kikuu cha Kenyatta.

Mwanakupona Binti Msham (1858). Utenzi wa Mwanakupona. Oxford University Press, Nairobi.

Mwinyi, M. (2020). *Kilingo cha Utenzi wa Mwanakupona katika Usawiri wa Mwanamke wa Pwani:* Mifano kutoka Kisiwa cha Tumbatu na Lamu. Tasnifu ya Uzamifu

katika Kiswahili(Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ndungo, C. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Njogu, K na Chimera, R (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar.* U.O.N Press, Nairobi.

Njozi, H. (1990). *Utendi wa Mwanakupona and Reception Aesthetics*. Kiswahili. Juz. 57: 55-67.

Oatey, S. H. (2008). *Culturally Speaking: Culture, Communication and Politeness* Theory. 2nd edition. Continuum, London.

Pembe, H. (2019). *Ufeministi katika utenzi wa Mwanakupona.* Kiswahili. 82(1), 174 – 184. Retrieved from: https://www.ajol.info/index.php/ksh/article/view/194891.

Perry, A. (1976) *"The Antinomies of Antonio Gramsci*." *New Left Review* 100: 5-78.

Robert, S (1967). *Diwani ya Shaaban: Insha na Mashairi*. Nelson, Nairobi.

Rossiland, F. (1990). *Marxism and Ideology*. Clarendon press, Oxford.

Senkoro, F. E. M. K. (1983). *Fasihi.* Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Swaleh, A. (1993, October 25). *Maudhui katika Utenzi wa Mwanakupona.* Tasnifu ya uzamifu katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi. Kutoka: http://erespository.uonbi.ac.ke/handle/11295/53467.

Tecla, K. P (2014, October 25). *Uyakinifu wa maudhui makuu katika Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani.* Tasnifu ya uzamili katika Kiswahili (Haijachapishwa.), Chuo Kikuu cha Nairobi. Kutoka: http://erespository.uonbi.ac.ke

Wafula, R. M na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wafula, R. M (2015, September 1). *Itikadi na ufundishaji wa nadharia za uhakiki wa fasihi.* Wasilisho la mkutano kutoka : https://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/13417?show=full

Wamitila, K. (2010). *Kazi ya fasihi : Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide – Muwa,

Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi Ya Fasihi : Istilahi na Nadharia*. Focus Publications Ltd, Nairobi.

Wandera, S. P. (1996). *Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili : 1800-1900 : Uhalisi au Ugandamizwaji* ? Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Egerton.

Wandera-Simwa, S. P. (2021). *Mwanamke wa Kiswahili katika Utenzi wa Mwanakupona.* East African Journal of Swahili Studies, 4(1), 82-98. Kutoka: https://doi.org/10.37284/eajss.4.1.422.

Williams, R. (1985). *Keywords: A Vocabulary of Culture and Society*. Revised Edition. Oxford University Press, New York.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho A: Kibali Cha Kukubalika Kwa Pendekezo

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 810901 Ext. 4150**

**Internal Memo**

**FROM:** Executive Dean, Graduate School

**DATE:** 15th January, 2025

**TO:** **Doreen Nkatha Mutembei**
**C/o Kiswahili Dept.**

**REF:** C50/20038/2021

**SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

We acknowledge receipt of your revised Research Proposal as per our recommendations raised by the Graduate School Board of 15th November, 2024 entitled **"Mtazamo Linganishi wa Itikadi katika Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka."**

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking and Progress Report Forms per semester. The Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

**ELIJAH MUTUA**
**FOR: EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL**

C.c. Chairman, Department of Kiswahili.

Supervisors:

1. Dr. Jessee Murithi
C/o Idara ya Kiswahili
**Kenyatta University**

*EM/mo*

*Transforming Higher Education… Enhancing Lives*
Kenyatta University is ISO 9001:2015 Certified

Page **1** of **1**

**Kiambatisho B: Kibali Cha Idhini Ya Kutekeleza Utafiti**

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 8710901 Ext. 57530**

**Our Ref:** C50/20038/2021

**DATE:** 15th January, 2025

Director General,
National Commission for Science, Technology and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR DOREEN NKATHA MUTEMBEI – REG. NO. C50/20038/2021**

I write to introduce **Doreen Nkatha Mutembei** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili.**

**Doreen** intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, **"Mtazamo Linganishi wa Itikadi katika Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

**PROF. ELIUD NJAGI**
**EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL**

*EM/mo*

*Transforming Higher Education… Enhancing Lives*
Kenyatta University is ISO 9001:2015 Certified

Page **1** of **1**

**Kiambatisho C: Kibali cha NACOSTI**


REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **508799**

Date of Issue: **26/November/2024**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Miss.. DOREEN NKATHA of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nairobi on the topic: MTAZAMO LINGANISHI WA ITIKADI KATIKA UTENZI WA MWANAKUPONA NA MASHAIRI YA MUYAKA for the period ending : 26/November/2025.**

License No: **NACOSTI/P/25/4175227**

**508799**

Applicant Identification Number

Deputy Director
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to.
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
   i. Endanger national security
   ii. Adversely affect the lives of Kenyans
   iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
   iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
   v. Adversely affect the environment
   vi. Adversely affect the rights of communities
   vii. Endanger public safety and national cohesion
   viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. Neither the license nor any rights thereunder are transferable.
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke